ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake

38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
52.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
54.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
55.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
56.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
57.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
59. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini

60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
62.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
63.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
64.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
66.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
69.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
70.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Ishirini na Tatu – Tarehe 17 Julai, 2012

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mahmoud Mohammed Mussa) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba sasa kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2012/2013. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Nassor Salim Ali (Kny: Mhe. Amina Idd Mabrouk, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2012/2013. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujaendelea na maswali naomba nikufahamisheni kuwa leo tumepata ugeni hapa wa Wanafunzi kutoka Skuli ya Mkwajuni wako pale juu, tuna wanafunzi 37 pamoja na walimu wao watano. Wanafunzi karibuni muweze kuona shughuli zetu zinaendelea vipi ahsanteni.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 76

Kukithiri kwa Watumiaji wa Dawa za Kulevya Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Zanzibar hivi sasa inakabliwa na wimbi kubwa la vijana walioathirika na matumizi ya dawa za kulevya na kujishirikisha na vitendo vya uhalifu.

(a) Serikali ina mpango gani wa kujenga kituo cha matibabu na ushauri nasaha kama kilichojengwa Mombasa nchini Kenya.

(b) Kwa kuwa vijana hao huiba vitu mbali mbali ikiwemo chuma chakavu, madirisha na mbao hasa katika Mji Mkongwe. Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti biashara ya vitu vya wizi kupitia vijana hao walioathirika na matumizi ya dawa za kulevya.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 76 lenye kifungu (a), na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, nia na azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwa na kituo cha Marekebisho ya Tabia kwa watumiaji wa dawa za kulevya bado ipo pale pale. Hatua mbalimbali huko nyuma ziliwahi kuchukuliwa za kutafuta washirika wa maendeleo katika kufikia lengo hilo ambazo hazikuweza kuzaa matunda.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjuilisha Mhe. Mjumbe na Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa ujumla, kwamba hatua za awali za ujenzi wa kituo hicho zinatarajiwa kuanza kwa mwaka huu wa fedha. Ujenzi wa kituo hicho umetiwa katika programu za Miradi ya Maendelo ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ambapo jumla ya shilingi milioni mia moja (100,000,000/-) zimetengwa mwaka huu kwa ajili ya shughuli hiyo.

(b) Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjulisha Mhe. Mjumbe na Baraza lako kwamba Serikali tayari imechukua hatua za kuwaita wafanyabiashara wa vyuma chakavu ili kuwaonya na kuacha kununua vifaa vya miundombinu kutoka kwa vijana hao, lakini pia kutoka kwa mtu yeyote yule. Hili limefanywa kupitia Mhe. Mkuu wa Mkoa akiwashirikisha Mkuu wa Polisi Wilaya ya Mjini, Mkurugenzi Bandari, Mkurugenzi Manispaa na wanunuzi wa mali chakavu wote. Aidha, uanzishwaji wa Polisi Jamii ambao kwa kiasi kikubwa umekuwa ukiwahusisha wanajamii kujilinda na kupambana na uhalifu katika maeneo yao pia ni katika juhudi za Serikali za kupambana na vitendo hivyo vya uhalifu. Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu nitoe pongezi zangu za dhati kwa shehia ya eneo la Mji Mkongwe, eneo ambalo limepiga hatua kubwa katika kupambana na aina zote za uhalifu kupitia vikosi vyake vya ulinzi shirikishi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu yake mazuri sana kabisa yaliokidhi swali la msingi nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kituo cha Ushauri Nasaha cha Waathirika wa dawa za kulevya kinatarajiwa kujengwa katika eneo gani na baada ya miaka mingapi kitamalizika.

Pili, kwa maeneo mengi yameibiwa mafuniko ya makaro. Je, Wizara yako ina mpango gani kuyarejesha tukizingatia ni hatari hasa kipindi hiki cha mvua kwa watoto na watu wazima.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kituo hiki cha kurekebisha tabia kinategemewa kujengwa kwenye eneo letu ambalo tunalo muda mrefu, tuna *plot* ya karibu ekari 3.5 katika eneo la Tunguu na kumalizika kwake kutategemea uingizwaji wa fedha ambao pia utategemea kupatikana kwa mapato kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Katika bajeti hii tumepata kidogo sana na ni shilingi milioni mia moja tu ambayo itaanza kuanzisha ujenzi wenyewe.

Suala la pili nimwambie ofisi yangu itashirikiana na taasisi husika ambayo ni Baraza la Mji katika kuhakikisha kwamba maeneo ambayo yako wazi ambayo pia ni hatari katika mazingira yetu yanawekewa mifuniko hiyo kwa kadiri inavyoondoka basi inawekwa ili kuondoa hatari kwa watoto wetu lakini pia athari za kimazingira ambazo zinaweza kutokea.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, napenda kumuuliza Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa wapo waathirika kutoka Kenya na Oman wamejiunga na wenzao wa Zanzibar kupata ushauri wa kuacha dawa za kulevya. Je, Mhe. Waziri kuna utaratibu gani walioufanya wa kuingia hapa Zanzibar ili kujiunga na wenzao kuacha dawa hizo za kulevya.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli katika vituo ambavyo ni *Sober House* vinavyoendeshwa na taasisi ambazo si za kiserikali, lakini navyo serikali inashirikiana navyo sana katika kurekebisha tabia za vijana wetu ambao wameamua kuacha dawa za kulevya wapo vijana kutoka nchini Oman.

Napenda nimhakikishie kwamba vijana hawa kama wasafiri wengine wameingia nchini hapa kihalali na wanakaa hapa kihalali kwa kufuata taratibu na sheria zote za uhamiaji.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri

kwamba zimeshatengwa shilingi milioni mia moja kwa ajili ya matibabu na ushauri nasaha wa waathirika wa dawa za kulevya. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa waathirika wa madawa ya kulevya mara nyingi huwa wanapata tatizo la akili (*psychiatry problem*) na kwa kuwa juzi tu katika bajeti ya Wizara ya Afya tuliambiwa ni ma-*specialist* wawili tu ambao mmoja yuko Tanganyika na mwengine yuko Cuba walio-*specialize* mambo ya *psychiatry*. Kwa hivyo, Zanzibar ina upungufu mkubwa wa madaktari wa akili (*Psychiatrist*) baada ya kustaafu Dr. Wakili.

Je, Wizara yako kwa kushirikiana na hawa Wizara ya Afya ina mpango gani wa kuwanasihi hawa vijana wetu wanaomaliza *MD*, yaani *degree* ya mwanzo katika mambo ya *medicine* ku-*specialize* katika suala zima la mambo ya *psychiatry* ili kuweza kuwasaidia hawa vijana wetu walioathirika na mambo ya dawa za kulevya.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba kwanza nimrudishe kwenye majibu yangu, tulichozungumza hapa ni kwamba zimetengwa shilingi milioni mia moja kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Kutoa Matibabu na Ushauri nasaha kwa watoto wetu na vijana ambao wanaamua kuacha kutumia dawa za kulevya lakini sio kwa ajili ya matibabu ya vijana hao.

Kuhusu suala lake ni kweli kama zilivyo kada nyengine ambazo zinahusika na utibabu wa aina mbali mbali tuna upungufu mkubwa katika eneo hili na ni nia ya Serikali kuendelea kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhakikisha kwamba tunapata vijana ambao tutaweza kuwashawishi kwa sababu kitu cha mwisho katika binadamu au mwananchi mwenyewe ni kuamua kitu gani anataka kusomea. Nia yetu ni kuweza kuwashawishi ili waingie katika kada hii muhimu ili nasi tuweze kuwapata katika kutusaidia katika jamii yetu.

Nam. 3

Kukosekana kwa Nyumba ya Kupumzikia Rais Mkoa wa Kusini - Unguja.

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 176

Usumbufu wa Usafiri baina ya Unguja na Pemba

Mhe. Asha Abdu Haji - Aliuliza:-

Si vizuri kukumbusha msiba katika matanga, lakini Waswahili wanasema, "Lisilobudi hutendwa". Tangu ilipotokea ajali ya *MV Spice Islanders* yameshajitokeza matukio mengine ya hatari katika bahari baina ya Visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

(a) Je, ni sababu zipi zinazosababisha usumbufu na ajali kwa wasafiri baina ya Visiwa vya Unguja na Pemba.

(b) Je, ni hatua gani zinazochukuliwa kuondosha usumbufu huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nambari 176 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla suala la usafiri kati ya Unguja na Pemba umekuwa ni tatizo la muda mrefu tokea Meli kubwa za Serikali kuchakaa na kuharibika mara kwa mara. Aidha, pamoja na nia njema ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuruhusu biashara huria kwa upande wa safari hizo mwamko wa wafanyabiashara wetu bado ni ndogo. Hata hivyo, tunashukuru wale waliioonesha nia ya kukubaliana na azma ya Serikali kwa kuanzisha *route* ya kwenda Pemba na Unguja kwa ajili ya kusafirisha wananchi wetu.

Katika safari hizo ingawa kumekuwa na matokeo yasiyoridhisha na kufurahisha bado Serikali itaendelea kuratibu na kuhakikisha kwamba huduma hizo zinaimarika kwa kuwa na vyombo vipya na vya kisasa, kwa kuendelea kuwashajiisha wafanyabiashara wetu ili kuona umuhimu wa kununua meli mpya na zilizosalama zaidi kama taratibu za usafiri baharini zinavyoelekeza. Katika kukabiliana na changamoto zinazojitokeza, serikali imekuwa ikichukua hatua kadhaa ili kuimarisha huduma hizo za usafiri. Ni matarajio yetu tukipata meli hizo mpya, kubwa na za kisasa changamoto ziliopo zitaondoka. Sababu za usumbufu ni nyingi likiwemo suala la uchakavu, ubovu, masuala ya kiufundi, lakini

pia hali ya hewa nayo huwa ni chanzo cha usumbufu kwa wasafiri wetu.

b) Hatua zinazochukuliwa na Serikali ni kuondoa usumbufu huo ni kuhakikisha wale wote wahusika wanafuata sheria husika ya masuala ya usafiri baharini. Kwa upande mwengine Serikali inaendelea kuwshajihisha wafanyabiashara wetu kuitikia wito wa kuwekeza katika eneo hilo huku serikali ikiwa mbioni ili kupata meli mpya kubwa na ya kisasa itakayokidhi mahitaji ya huduma za usafiri kati ya Unguja na Pemba.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nashukuru kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza kwa Mhe. Naibu Waziri. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri kuwashajihisha wafanyabiashara kununua meli na kuondoa tatizo hili la usafiri baina ya Kisiwa cha Unguja na Pemba. Kwa kuwa suala hili la matatizo ya usafiri limekuwa ni la muda mrefu kisiwani hapa, kwa kuwa asubuhi hii tumepata taarifa kwamba Meli ya *Sepideh* imekwama na kubururwa na Meli ya Serengeti yaani wafu kwa wafu wanakokotana. Na kwa kuwa ni wiki chache zilizopita hivi juzi kuna Meli ya *Seagull* nayo ilikwama njiani.

Mhe. Waziri kwa kuwa Serikali ndio yenye jukumu kubwa kuwalea wananchi wake na kuwaondolea matatizo mbali mbali. Je, wizara yako ina mipango gani ya kutafuta meli ya Serikali kuwaondolea wananchi wa Zanzibar kero hii ukizingatia kwamba Zanzibar ilikuwa na meli zake za Serikali. Hilo la kwanza.

Pili, kwa sababu tunakumbuka kilio kilichotokea hapo nyuma. Je, tatizo hili likitokea tena katika kipindi hiki Serikali yetu itawaambia vipi wananchi wa Zanzibar na mataifa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli nakubaliana na mawazo ya Mhe. Mwakilishi kwamba wakati umefika wa kuweza kuona kwamba pamoja na jitihada ya Serikali ya kuwashajihisha wafanyabiashara wetu kuwekeza kwa kuwa na meli kubwa, nzuri na za kisasa Serikali imefika wakati nayo kuwa na meli yake mpya. Azma hiyo Serikali imedhamiria na naomba sana Mhe. Mwenyekiti na Baraza lako tukufu tutakapokuja na bajeti yetu watupitishie tukakamilishe mipango ya kupatikana kwa meli mpya.

Lakini la pili Mhe. Mwenyekiti, napenda nikiri kwamba kweli kuna chombo ambacho kilikuwa kinafanya safari kikapatwa na matatizo na ni kweli kimefungwa kimerejeshwa lakini jambo la kuendelea ni kumshukuru

Mwenyezi Mungu kwamba kimefika kule salama na watu wameshuka taratibu nyengine za kisheria zinafuata. Kwa hivyo, matarajio yangu kwamba serikali mpango ni kununua meli, lakini katika kipindi hiki lazima tuendelee kuwashajihisha wafanyabiashara wetu na wao walione hilo soko ili kuweza kutoa huduma kwa wananchi wetu.
Mhe. Mwenyekiti, matarajio yangu, ya wananchi wenzangu kwamba tatizo kama lile lililotokea sidhani kama kuna mtu anaomba litokee na litapotokea tatizo basi serikali itatoa muongozo wake na maamuzi ya Serikali yatawafikia wananchi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, kupata nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuuliza swali ni kuwa Mhe. Waziri amesema yaliyotokea hatarajii kutokea tena, lakini kabla ya kutokea tulikuwa tukipiga makelele ya juu kabisa na kauli yetu ikadharauliwa mpaka yakatokea yaliyotokea. Swali, Mhe. Mwenyekiti, ninavyojua serikali hii kwa kupitia Shirika la Meli imeuza Meli ya Afrika, imeuza Meli ya Jamhuri na imeuza Meli ya Mapinduzi. Ni kitu gani hasa kilichosababisha baada ya kuuza meli zote hizi tatu wakashindwa kuweka meli moja inayofaa kwa kusafirisha abiria kutoka Pemba kwenda Unguja na kadhalika.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali ilikuwa ikimiliki meli hizo na ni kweli kwamba Serikali meli hizo imeziuza. Lakini Serikali kati kati ilifungua mlango wa biashara huria kwa wananchi na mtu yoyote mwenye uwezo wa kuja kuwekeza katika eneo hilo, shida ya meli iliyopo Serikali imeliona na imejipanga, na katika hili serikali itafanikisha ili kuondoa hilo tatizo. Napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi na Baraza lako tukufu kwamba nawaomba sana tutakapokuja na bajeti yetu tupitishiwe tukakamilishe mpango wa upatikanaji wa meli.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi hii na naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza lenye vifungu a na b.

(a) Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Wazanzibari mara zote pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamekuwa wakitoa tahadhari kwa Wizara hii juu ya ubovu wa meli zetu, na kwa kuwa matokeo haya ya kuzimika kwa meli baharini yamekuwa yakitokea mfululiozo, na kwa kuwa matajiri wanaendelea kufanya huduma hii ya usafiri wa baharini. Je, Mhe. Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba Wizara yake inawatumikia zaidi matajiri kuliko wanyonge.

(b) Kwa kuwa Wizara hii imekuwa na sikio gumu haisikii na kwa kuwa Wazanzibari wanaendelea kuumia asubuhi hii *Sepideh* iko Tanga kwa ajili ya kupotea baada ya kuzimika, atakubaliana nami kwamba Wawakilishi hawana haja ya kumpa fungu la fedha yoyote kwa ajili ya Wizara hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, samahani swali lake la kwanza sikulisikia ile *content* yake.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, swali la kwanza ni kwamba Wazanzibari pamoja na Wawakilishi tumekuwa tukitoa tahadhari juu ya ubovu wa meli na matukio ya kuzima kwa meli yanatokea kila wiki au mwezi. Mhe. Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba Wizara yake inajali matajiri zaidi kuliko wanyonge.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba mara nyingi Waheshimiwa Wawakilishi wanaungana na wananchi wengine katika kutoa tahadhati. Na sisi kama Wizara tunazichukua tahadhari hizo na kuzifanyia kazi ili kuona majanga hayo yanayotolewa tahadhari hayatokei. Lakini Mhe. Mwenyekiti, tulichokieleza ni kwamba matatizo haya yanayotokea katika vyombo vya usafiri yana sababu nyingi, tumeeleza kwamba uchakavu, ubovu, lakini pia hali ya hewa nayo ni chanzo kinachopelekea matatizo ya usafiri katika vyombo vya baharini.

Mimi imani yangu kwamba wizara yetu ni sehemu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na madhumuni ya Serikali ni kuwahudumia zaidi wananchi na sio matajiri. Kwa hivyo, wizara yetu inatekeleza maelekezo ya Serikali na katika serikali yetu hakuna matabaka wananchi wote wako katika kiwango sawa hakuna anayejaliwa zaidi ya mwengine, kwa hiyo namuomba Mhe. Mwakilishi aendelee kujenga imani na Wizara hii, aendelee kujenga imani na Serikali hii, hakuna anayepewa huduma kwa kuonekana yeye mbora kuliko mwengine. Kwa hivyo, hatuwajali matajiri kulikoni wananchi wetu, kipaumbele chetu sisi ni wananchi kwa kuamini kwamba wananchi wote wako sawa katika kupata huduma za Serikali yao.

Swali la pili, Mhe. Mwenyekiti, napenda kumwambia Mhe. Mwakilishi aondoe kauli yake Meli ya Sepideh haijafika Tanga, pamoja na matatizo yaliyotokea usiku kuanzia saa sita na nusu tulipigiwa simu tukazungumza na wenzetu walioko katika vituo tukafanya mawasiliano na kepteni wa chombo kile, tukaweza kufanya mawasiliano na kepteni wa chombo cha Serengeti akafika na chombo akakifunga na kiko Pemba. Sasa Mhe. Mwakilishi

atwambie huko Tanga iko sehemu gani hiyo meli, mana taarifa tulizonazo sisi kwamba watu wameshashuka katika chombo hicho. Sasa Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe, Mwakilishi aondoe hii kauli ya kusema chombo kiko Tanga anawapotosha watu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati mbaya mimi si baharia nilipokea taarifa kama ambavyo yeye amepokea, simu yangu ina *message* za watu ambao wamo ndani ya Sepideh na kusema kwamba muda huu tuko Tanga. Sasa Mhe. Mwenyekiti, siku zote *information is power*, nimepokea taarifa na yeye kapokea taarifa, hoja ya wapiga kura wangu kwamba walikuwa safarini Tanga kwa ajili ya meli kuzimika, sasa kama wanataka nithibitishe basi tuwafuate wapiga kura wangu tukawahoji mlikuwa wapi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe hoja ya Naibu Waziri ilikuwa ni suala la kwamba hii taarifa ambayo imekuja wewe umesema kwamba iko Tanga wakati chombo kutokana na vyombo ambavyo vimekwenda kusaidia wamekuta hicho chombo kiko Pemba na Mhe. Naibu Waziri anaomba kwamba ufute kauli ya kusema kuwa kile chombo kiko Tanga badala ya kwamba kiko Pemba. Sasa naona hujafanya hivyo isipokuwa umetoa maelekezo mengine juu ya upokeaji wa taarifa hiyo. Taarifa ni taarifa inaweza kuja katika misingi yoyote, lakini wao wapo katika utaratibu wa hili tukio lililotokea. Naomba umuelewe Mhe. Naibu Waziri kile anachokizungumza.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nadhani sina haja ya kubishana na wewe nakuheshimu sana, ninachosema abiria walioko kwenye meli hadi wananiandikia *message* mimi walikuwa Tanga, ikiwa muda huu meli iko Mkoani maana yake imevutwa kutoka Tanga, ninachosema abiria walikuwa Tanga baada ya meli kuzimika kama Naibu Waziri anatwambia sasa hivi meli iko Mkoani nshukuru kwa niaba ya wapiga kura wangu.

Nam. 177

Ubovu wa Barabara ya Kibonde Mzungu

Mhe. Asha Abdu Haji - Aliuliza:-

Pamoja na mambo mengine yanayosababisha ajali, ubovu wa barabara ni miongoni mwa mambo hayo. Kuna ubovu mkubwa sana katika daraja la Kibonde Mzungu liliopo karibu na jaa kubwa la Jumbi katika Wilaya ya Magharibi, Madereva pamoja na abiria wanakuwa na hofu kubwa wakati gari zikipita katika eneo hilo.

(a) Je, kwa nini njia hiyo haijakarabatiwa hadi leo.

(c) Kwa kuwa ubovu huo upo na unaendelea kukua Serikali ina mikakati gani ya kukarabati njia hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:
Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 177 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, eneo la Kibonde Mzungu ni eneo la bonde ambapo maji ya mvua hukusanyika na hutuama kwa wingi na kwa muda mrefu, hivyo kusababisha kutitia kwa barabara mara kwa mara katika eneo hilo na kusababisha usumbufu kwa watumiaji wake.

Wizara yangu kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara tayari imeshachukua hatua ya matengenezo katika eneo ambapo hadi muda huu kifusi kimeshawekwa na lami ya awali imeshawekwa. Matarajio yetu katika siku mbili tatu zinazofuata lami ngumu ya kokoto itawekwa ili kumaliza changamoto hiyo.

Mhe. Asha Abdu Haji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa kakiri kwamba sehemu ile mara kwa mara inatengenezwa, lakini ni sehemu kubwa ya kupitia maji. Kwa kuwa keshakiri haoni kwamba ipo haja ya kujenga daraja sehemu ile.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli maelezo anayosema Mhe. Mwakilishi, kwamba ukitazama kwa upana unaweza kuona kwamba kuna haja ya kujenga daraja. Lakini daraja kikawaida huwa linajengwa katika maeneo ambayo yana maji yanakatisha ya kudumu. Eneo analolizungumzia ni eneo linalokatisha maji wakati wa mvua. Kwa hivyo, imani yetu kwamba *culvert* iliopo bado inatosha na kutitia kunatokana na maumbile ya ardhi yenyewe na sio kwamba maji yanashindwa *ku-flow.*

Kwa hivyo ninapenda kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba *culvert* iliopo inatosha kutoa huduma ya kukatisha maji kutoka upande wa kaskazini kwenda kusini. Kwa msingi huo hatujaona umuhimu wa kulazimika kujenga daraja kwa kipindi hiki.

Nam. 129

Ukosefu wa Huduma ya X-ray Hospitali ya Micheweni

Mhe. Bikame Yussuf Hamad – Aliuliza:

Kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Micheweni wanalazimika kufuata huduma ya X-ray katika hospitali ya Wete, Chake-Chake na hata Mkoani kwa kusomwa X-ray hizo.

Na kwa kuwa serikali kwa kipindi kirefu imepeleka mashine hiyo ya X-ray katika hospitali ya Micheweni *Cottage* kwa kuwaondolea wananchi wake usumbufu wa kufuata huduma hiyo masafa marefu. Lakini hadi leo hii huduma hiyo bado haijapatikana katika hospitali hiyo.

Jee, Mhe. Waziri ni sababu gani mpaka leo chombo hicho hakifanyi kazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 129 kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli madhumuni ya kupelekwa mashine za X-ray katika hospitali zote za Wilaya na Mikoa, ni kuwasogezea huduma wananchi na kuwaondolea usumbufu wananchi wa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, chombo cha X-ray cha Micheweni ni kizima na kinafanya kazi, ila upungufu wa picha za X-ray umesababisha kupatikana mfanyakazi wa kutoa huduma kwa hospitali ya Micheweni.

Kwa hivyo mfanyakazi hutoka hospitali ya Wete amepangiwa kwenda Micheweni mara moja kwa wiki. Daktari mtaalamu wa kusoma picha kwa Pemba yupo Mkoani.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali dogo sana la nyongeza.

Kwa kuwa X-ray zinapigwa hospitali ya Micheweni, Chake-Chake na Wete lakini msomaji yupo hospitali ya Mkoani. Jee wizara yako Mhe. Naibu Waziri itaandaa utaratibu gani wa kuwapunguzia gharama wale watu wa Micheweni, Wete na Chake-Chake kwenda Mkoani.

La pili jee, isingekuwa vyema kwa huyu msomaji akawa ni *rotating*, akawa wakati mwengine anasoma Chake-Chake, anapewa mafuta anakwenda Micheweni na Wete ili kutupunguzia gharama wananchi ukitilia maanani kwamba huko Pemba kila siku tunapigwa X-ray mara tumeshaanguka mikarafuu almuradi sisi mashaka tuliyonayo si madogo.

Jee, isingekuwa vyema huyu msomaji aliyepo Mkoani akawa ana-*rotate* Pemba nzima akawezeshwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, ninapenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Ni kweli hayo unayoyasema lakini utaratibu upo hivi kwamba yule Mchina aliyepo ambaye ndiye msomaji yeye anakaa Mkoani, na ile ndio *station* yake. Picha zinapigwa Micheweni, Vitongoni, Chake-Chake na Wete.

Utaratibu uliokuwa umewekwa kwamba zikishapigwa picha zinakusanywa zinapelekwa Mkoani kwa ajili ya kusomwa. Lakini si wananchi wote ambao wanakuwa wanastahamala kungojea utaratibu huu. Kila siku zinakusanywa na kupelekwa, wengine wanasema tutapeleka wenyewe, kwa hivyo wanaposema kuwa watapeleka wenyewe hapo ndipo wanapoingia gharama.

Lakini utaratibu haupo hivyo. Lakini ukishasema kwamba utapeleka mwenyewe hawawezi wakakuzuia, lakini baada ya kuyaona hayo unayoyasema wewe sasa tumeamua kwamba hivi, picha zote kama taratibu zilivyo zitakusanywa na kupelekwa Mkoani kwenda kusomwa na kurudishiwa watu katika sehemu zao. Hilo ni la kwanza.

Lakini la pili sio kila picha inahitaji mtaalamu kusoma. Picha nyengine zinaweza zikasomwa pale pale na wale wale wapiga picha. Kwa mfano picha za kuvunjika hiyo mtaalamu wa kusoma wa picha yeyote anaweza akasoma, lakini kuna picha maalum kwa maradhi maalum ambapo yanahitaji msoma picha aweze kusoma, au kuna picha maalum ambazo zinahitaji mgonjwa kupelekwa kwa yule msoma picha kwa sababu hizo haziwezi zikafanyika katika utaratibu wa kawaida.

Sasa huo ndio utaratibu. Baada ya kulijadili hili tumewaambia kwamba sasa wasiwaruhusu watu kuchukua picha zao zipelekwe kwa utaratibu ulioandaliwa, na watu sasa wastahamili ili wasiweze kuingia hizo gharama ambazo si za lazima wao kuingia.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Ninakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri amekiri kama msomaji wa X-ray ni mmoja kwa Pemba nzima. Kwanza ninamuuliza Mhe. Naibu Waziri atakubaliana na mimi kama hilo ni tatizo kwa sababu mwanadamu ni mwanadamu, kuna siku ni mzima pengine siku nyengine anaweza kuumwa.

Jee, kuwa msomaji X-ray mmoja haoni kama hilo ni tatizo, na jee kama anakiri hilo ni tatizo, kwa Unguja kuna wasomaji X-ray wangapi, na kama wapo wengi kwa nini hamchukui mmoja akampeleka mmoja kule Pemba wakawa wawili angalau mmoja akiumwa anamsaidia mwenzake.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo.

Suala la msoma picha popote pale ni tatizo si Unguja si Pemba. Pemba kuna Mchina mmoja, Unguja kuna Mchina mmoja na mzalendo mmoja. Kwa hivyo Unguja kuna wawili, Pemba kuna mmoja.

Huyo mmoja aliyepo Unguja anafanya kazi katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ambaye anasoma picha zote ambazo zinafanyika kwenye Hospitali ya Mnazi Mmoja. Huyo mwengine anasoma picha zote zinazotoka kwenye vituo na baadhi ya picha nyenginezo.

Kwa hivyo hakuna yule wa kumchukua kumpeleka Pemba kutokana na uzito wa kazi iliopo Unguja.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Kwa kuwa katika siku za hivi karibuni wananchi wanaohitaji huduma ya X-ray wakienda kwenye Hospitali ya Chake-Chake wanaambiwa wafuate huduma hiyo Hospitali hiyo Wete, kitu ambacho kinawapa usumbufu kwa sababu ni gharama kubwa sana kutoka Chake-Chake kwenda Wete, siku nyengine anaweza akatumia mpaka shilingi thamanini elfu kwa kukodi gari.

Jee kuna sababu zipi zinazopelekea huduma hiyo ikawa haipatikani Chake-Chake hivi sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako ninapenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo.

Chake-Chake nako kulikuwa na mpiga picha mmoja. Yeye sasa hivi kachukua likizo bila ya malipo, kwa hivyo pale pamebaki hapana mpiga picha. Lakini juzi mimi nilikuwa Pemba kuna mtu ambaye anatoka huko Mkoani anakuja pale kwa baadhi ya siku.

Na. 114

Sera ya Kujenga Viwanda katika Kupunguza Tatizo la Ajira

Mhe. Mohamed Mbwana (Kny: Mhe. Abdi Mosi Kombo) - Aliuliza**:-**

Hivi sasa Serikali yetu imetoa kipaumbele katika zao la Karafuu, Mwani na Utalii. Kwa vile nchi yetu imekuwa na wananchi wengi ambao hawana ajira hususan vijana.

Je, Serikali haioni kuwa imefika wakati wa kuweka kipaumbele sera ya kujenga viwanda ili kuziba pengo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu**:-**

Mhe. Mwenyekiti**,** naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nambari 114 linalohusiana na Sera ya Kujenga Viwanda kama ifuatavyo:-

Katika suala zima la kuinua uchumi wananchi wetu, SMZ kwa sasa imetoa kipaumbele kwa zao la karafuu, mwani pamoja na utalii.

Lakini sambamba na hilo, SMZ pia imeona kuwa suala la viwanda nalo lina umuhimu wa pekee, hasa baada ya kujitokeza tatizo la ukosefu wa ajira kwa wananchi na zaidi vijana.

Mhe. Mwenyekiti**,** katika kulifanyia kazi suala hili SMZ kupitia Wizara yake ya BVM inaifanyia mapitio (*review*) sera ya Viwanda ya Mwaka 1998 ili iendane na wakati, lakini zaidi kuweka vivutio maalum ili wawekezaji waweze kuja kuwekeza katika viwanda pia.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Naibu Waziri unaweza kutwambia vivutio vya namna gani ndio unavyotafuta wawekezaji ili waje haraka ili vijana wetu waweze kupata kazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuata

Mhe. Mwenyekiti, vivutio kwa uhalisia wake si rahisi kuvijua, na ndio maana tunasema sera hii iliopo ni lazima ifanyiwe *review* ili tuweze kujua na tuweze kwenda na wakati.

Lakini kwa ujumla wake vivutio vinahusiana pamoja na suala zima la uhakika wa umeme, suala zima la upatikanaji wa maji lakini pia mapungufu ya masuala ya kodi, lakini zaidi mapitio haya ya sera yataelekeza Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Ninashukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza Mhe. Naibu Waziri.

Pamoja na majibu mazuri aliyojibu Mhe. Naibu Waziri ya kueleza kama serikali imeweka vivutio kwa ajili ya wawekezaji kuja kuekeza hiyo huduma ya viwanda au sheria ya viwanda.

Lakini ninapenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri kama atakubaliana na mimi kuwa serikali ilitangaza maeneo huru kwa ajili ya wawekezaji kuja kuekeza katika maeneo huru, kama viwanda na mambo mengine.

Lakini katika hizo huduma za kuwavutia wawekezaji atakubaliana na mimi katika maeneo hayo kama hakuna barabara, maji na umeme. Sasa ni lini zitapelekwa huduma hizo ili wawekezaji wavutike na kuekeza katika maeneo hayo.

Na jee, kwa sababu sadaka huanza nyumbani, ni lini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaanza kuekeza angalau kiwanda kimoja tu kidogo katika maeneo hayo ili wawekezaji wavutike na wao kuweka huduma zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, nimesema katika jibu langu wakati nikijibu swali la nyongeza la Mhe. Jaku kwamba, moja ya vivutio ni pamoja na kuweka miundombinu ambayo yeye ameitaja, lakini na mimi pia niliitaja kabla.

Uwekaji wa miundombinu hiyo Mhe. Mwenyekiti, utaendana na kumalizika sera hii ya viwanda, lakini kwa mashirikiano ya wizara zinazohusika na masuala ya barabara, umeme na maji.

Sina mashaka Mhe. Mwenyekiti, kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar italifanyia kazi suala hili, kwa sababu ni lengo la serikali yetu kuona kwamba vijana wetu wanapata ajira.

UTARATIBU

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri kajitahidi kujibu lakini swali moja hakunijibu, kajibu moja tu.

Nilimuuliza ni lini Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itaanza kuekeza kiwanda japo kidogo ili wawekezaji wengine wapate nguvu za kuekeza na wao, waone kama mfano. Lakini hilo kasahau hajanijibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, nimejibu labda nifafanue zaidi.

Nimesema kwamba tutashirikiana na wizara zinazohusika na kuweka miundombinu. Maana yake bila ya miundombinu hiyo ya barabara, umeme na maji ya uhakika, uwekezaji kwenye viwanda bado unakuwa ni suala gumu, kwa sababu huwezi kuweka viwanda kama barabara ya uhakika haipo, huwezi kuweka viwanda kama umeme haupo, na mwenyewe Mheshimiwa anafahamu hivyo na maji ya uhakika kama hayapo viwanda hivyo Mhe. Mwenyekiti, si rahisi kuviendesha, Mheshimiwa anafahamu hivyo.

Kwa hivyo nimesema serikali inafahamu tatizo la ajira, na kwa hivyo itashirikiana na wizara hizo kupitia Wizara yangu kuhakikisha kwamba viwanda vinaekwa.

Lakini labda nimuongeze Mhe. Mwakilishi kwamba kwa sasa hivi sio kama viwanda havipo, vipo Mhe. Mwenyekiti. Mpaka sasa kufuatana na sensa ya 2010 Zanzibar kumeonekana kuna viwanda 129.

Na ajira wakati huo kwenye viwanda kulikuwa na ajira kwenye viwanda ambavyo vinafanya kazi zaidi ya kumi, ambapo ni 129 tuna wafanyakazi zaidi ya 3000.

Kwa hivyo, kwa kuwa viwanda ni vidogo vidogo lakini lengo la serikali ni kuona kwamba tunaekeza kwenye viwanda vikubwa, ili tuweze kupata vijana

wengi zaidi katika kuwatatulia suala la ajira au ukosefu wa ajira Mhe. Mwenyekiti.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 20122013

(Majadiliano yanaendelea)

TAARIFA

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, jana Mhe. Naibu Spika, alipoondoka aliahidi kwamba asubuhi angelianza kuchangia Mhe. Hija. Kwa hivyo naomba Mhe Hija apewe nafasi achangie.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa mujibu wa orodha ambayo nimeikuta hapa, naona inaniongoza nianze na Mhe. Saleh Nassor Juma, halafu Mhe Hija utaendelea.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipatia fursa ya kutoa mawazo yangu kuhusu hoja hii iliopo mbele yetu.

Awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwa hai na kutupa uwezo wa kuondoka katika maeneo yetu mpaka katika jengo hili la Kutunga Sheria. Hii ni hazina kubwa aliyotujaalia Allah, na kwa hivyo vile hatuna budi kumshukuru.

Mhe. Mwenyekiti, ninadhani nitakuwa mchache wa shukurani kama sijakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na ibara ya 11 ya kitabu hiki, na nitaanza na mahakama. Mhe. Mwenyekiti, mahakama ni moja katika mihimili mitatu ya dola. Jukumu lake kubwa mahakama ni kutafsiri sheria za nchi pamoja na kutoa haki sawa kwa wananchi wote kwa kufuata Katiba na sheria za nchi.

Mhe. Mwenyekiti, mahakama, Baraza la Wawakilishi pamoja na serikali, hii mihimili ni sawa sawa. Kwa bahati tunaiendesha kwa kodi za wananchi. Mihimili yote mitatu inafanya kazi kupitia kodi za wananchi.

Lakini jambo la kusikitisha Mhe. Mwenyekiti, inaonekana serikali, sitaki niseme wanaibana hii mihimili miwili lakini kwa kiasi kikubwa inaonekana serikali hawawafanyii haki kwa kiasi kikubwa hii mihimili miwili, kwa maana ya mahakama pamoja na sisi Baraza la Kutunga Sheria.

Tunataka tuangalie mahakama kwa kusifu wasifu wa nje. Mhe. Mwenyekiti, katika wasifu wa nje wa Mahakama za Zanzibari zina mapungufu mengi. Kwa mfano tukiangalia majengo yote ni ya kurithi. Magofu ya Wahindi ndio yaliyorithiwa. Ukianza tangu Pemba mpaka ukifika Unguja unaona Mahakama majengo yake hayaridhishi kabisa.

Lakini ukiangalia majengo ya serikali kila wizara. Ninamsifu hapa Waziri kasema kwamba tunajenga jengo la Makao Makuu, lakini jengo lile ni Wizara ya Katiba na Sheria ni la serikali. Mimi nilifikiria kwamba tunajenga jengo kubwa la Mahakama Kuu, jipya la kisasa kumbe ni la wizara. Ni wale wale *executive*.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli serikali inakuwa *bias* katika kuhakikisha kuwa hii mihimili mengine inaimarika. Majengo yaliopo Mhe. Mwenyekiti, hayakidhi haja. Kwa mfano pale Mahakama ya Chake-Chake ambapo ndio mahakama ya mkoa pale, pale ndio panakwenda kesi za Mahakama Kuu haparidhishi.

Mhe. Mwenyekiti, kesi za Mahakama Kuu za Pemba nzima zinafanyika Chake-Chake. Ukienda kwenye Mahakama ya Chake-Chake ile ni Mahakama tuliyorithi tangu alipokuwa wale majaji wa Mzee Karume, akina Jaji Ramadhan na huyu Mzee Macarious.

Hawa majaji hata skuli hawakusoma, ndio waliokuwa wakihukumu mule. Pale ukikaa kwenye kiti cha jaji pana lile feni linalia zogo. Mahakamani ni pahala panapotaka utulivu Mhe. Mwenyekiti.

Pale Hakimu anatakiwa achunge haki, anatakiwa atulie, mshitaki anatakiwa ajenge hoja kudai haki yake. Mshitakiwa anatakiwa awe katulia kujitetea, lakini mahakama ile aliyokuwa akihukumu Jaji Ramadhan, yeye hata skuli hakusoma na *site of reference* alizokuwa akizitumia Jaji Ramadhan ni *decrees* za Mzee Karume siku zile pamoja na *circumstance evidence* basi.

Yeye akishafika anakwita mshitakiwa njoo tizama kule nje, umewaona wale, eeh! mbona hawajaletwa hapa, wewe ndio umefanya kosa wewe, unasemaje bwana Haji Kombo, anamuuliza Mkuu wa Mashtaka, ni kweli. Mzee Karume alipohutubia alisema musigeme na nyinyi mumegema, basi ninakufunga miaka kumi au unasemaje bwana Haji, na yeye anasema mimi niongezee mmoja, wote hawakwenda skuli.

Sasa mahakama zile ndizo walizokuwa wakitumia hao. Lakini sasa majaji wanatakiwa wawe wametulia pahala na pametulia, *well equiped, site of*

reference wanazozitumia ni kwamba lazima watumie mitandao ya pahala fulani au nchi fulani, kesi hii Hakimu wa nchi fulani alihukumu hivi, anavuta pale anaona. Kesi hii katika Mahakama ya *Common wealth* iliopo India imehukumiwa hivi, isiwe kama zile za Jaji Ramadhan na Jaji Macarious sio sasa.

Lazima mahakama za leo ziwe za kisasa. Kwa kweli muhimili wa mahakama tunaudhalilisha kweli kweli na mimi ninadhani katika hili Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa mgumu sana kupitisha kifungu hiki cha Mahakama mpaka pale Mhe. Waziri atakaponiambia ni lini itajengwa jengo la Mahakama Kuu la kisasa kabisa, na pale Pemba litajengwa jengo la Mahakama la kileo ambalo kesi za Mahakama Kuu zitakwenda pale na sio pale Jane Building. Hilo ni moja Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, mapungufu mengine yaliopo katika Mahakama zetu hasa pale Pemba kunakuwa na mrundikano mkubwa wa kesi. Kesi zinakuwa ni nyingi sana. Ninashukuru hapa Mhe. Waziri katika kitabu chake kasema kwamba kila mwezi wanakwenda Majaji wawili kuhukumu.

Sasa iwe kila siku tuhangaishe Majaji wetu kwenda na kurudi, ndege na meli zenyewe ni mbovu. Kwa nini tuwahangaishe Majaji. Kule Pemba Majaji hewa iliopo Majaji inawadhuru. Hawana nyumba za kukaa Majaji kule Pemba zenye *status* wao hamna.

Mimi ninadhani katika hili Mhe. Mwenyekiti, lazima hivi visiwa muvi-*treat equal*, musiwe *bias*. Wapemba ni wapiga kura ni sawa sawa na hawa wanaokwenda huku. Majaji pia mumewakusanya huku, kule kwa nini hamuwapeleki wakahukumu.

Lazima muwaendeshe muwarudishe. Mimi ninadhani kwa sasa kuna haja ya kuwa na *permanent residencial Judge* pale Pemba. Nyumba zipo, barabara za kupitia gari zao zipo, kila jambo lipo kwa nini musiwapeleke wakakaa kule.

Hapa Unguja Mhe. Mwenyekiti, kuna Majaji ni Wapemba, wanalipwa *house allowance*. Kwa taarifa nilizonazo Mhe. Mwenyekiti, kila Jaji na sidhani lakini nimepata taarifa kuna *house allowance* ya shilingi laki saba kwa kila Jaji, na kule nyumba za kukaa zipo za kisasa. Kwa nini wasilipe hizo fedha wakaa kule na watastarehe zaidi kwa sababu kuna marashi ya karafuu na kuna mambo mengine mazuri, atapata kustarehe tu Jaji wetu, wapelekeni.

Ninadhani kama mutaweka *permanent residencial Judges*, huu mrundikano wa kesi utapungua. Mhe. Mwenyekiti, wanasheria wanasemaje, maana hivi sasa kuna kesi zimekaa zinasubiri Majaji wawili waende huko Pemba, kuna

kesi chungu nzima zina mwezi mzima au miwili nyuma zinasubiri Majaji waende wakahukumu.

Tunafanya makosa kwa sheria zenu nyinyi, mimi si mwanasheria lakini nyinyi munasema kwamba haki ikichelewa kutolewa ni sawa sawa na kwamba haikutolewa kabisa. *Justice delay is justice denied*. Munatwambia nini kuwa kila baada ya mwezi ndio mutupelekee jaji, huku watu wanasubiri jaji ndio zihukumiwe, haki zao zinachelewa, una Katiba ya nchi.

Ninadhani jambo jengine kuna rufaa kubwa wale, kwa sababu kesi zinakwenda kienyeji kwa mujibu wa *interest* ya hakimu mwenyewe, kuna na kesi nyingi zimerundikana na hii ni kwa sababu hakuna ile *case flow management*.

Mimi ninadhani mahakama wapange hili Mhe. Waziri, muwe na utaratibu wa kimahakama kuona ile *case flow management* ya kila wiki, jaji kahukumu kesi ngapi kwa wiki. Jaji kahukumu kesi ngapi kwa mwezi, unamu-*assess* jaji, sio kama leo katoka jaji anakwenda anaakhirisha kesi tu ndio huo mrundikano unabakia kuwa mkubwa mheshimiwa.

Mhe. mimi nadhani wakipanga hivyo na halafu ukiwa na kitu wataalamu, nyinyi wanasheria mnakiita *monetary system*, mufanye *monetary system* ya wale mahakimu wanaohukumu hizi kesi zao, nadhani huu mrundikano wa kesi hasa kisiwani Pemba utapungua.

Mhe. Mwenyekiti, bado naendelea hapo hapo kwenye mahakama, nakwenda kwenye mahakama ya Kadhi. Mahakama ya Kadhi ni mahakama muhimu sana kuwepo katika nchi inayojali na kuthamini demokrasia na utawala bora. Hii mahakama kwa bahati nakumbuka Zanzibar ipo, aliwahi kupewa Jaji mmoja nguli sana katika mambo ya sheria, marehemu Jaji Wolfgang Dourado, aliikataa mahakama hii kuifanyia kazi. Lakini akaja akaichukua Mhe. Mshibe kwa kweli kafanya kazi nzuri, lakini haiko katika viwango hii mahakama ya Kadhi vya mahakama za Kadhi zilioko katika *Common Wealth.* Mahakama za Kadhi zilioko katika *Common Wealth* zina viwango, yaani zinakuwa na kanuni zao. Kama ingekuwa sio umahiri na umakini wa Jaji Mshibe pale kwenye mahakama hii basi ingekuwa ni tatizo. Kaichukua Jaji Mshibe, lakini kwa sababu ni mahiri katika mambo ya kuendesha kesi na kutoa hukumu akaimudu.

Kwa hivyo, mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, watayarishiwe *rolling* hawa, hii mahakama iboreshwe na iendelezwe, isidharauliwe hata kidogo. Nampongeza sana Jaji Mshibe kwa kuiendesha vizuri mahakama hii.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende katika mahakama ya biashara. Mahakama hii nashukuru imetajwa hapa katika ukurasa wa 35 mpaka 36 kwamba kuna lengo la kuanzisha mahakama ya biashara, nyumba ile inataka kufanyiwa ukarabati. Lakini yule mfadhili aliyekuwa akitufanyia ukarabati ile nyumba, yaani huyu Best kaondoka. Sasa Mhe. Mwenyekiti, pale ina maana walitumia fedha pale na kwa sababu fedha walizozitumia walizileta serikalini moja kwa moja sisi ndio masuuli kwa sababu itakuwa zimeshaingia mikononi mwa nchi.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nataka Mhe. Waziri katika hili anieleze Best katika kusaidia walisaidia kiasi gani, na hiyo kazi ya kui-*assess* imefikia wapi. Ni sababu gani hasa zilizowafanya hawa Best waondoke, nataka Mhe. Waziri aje kunifafanulia kitu hicho.

Halafu tuje katika mahakama nyengine ya watoto. Mhe. Mwenyekiti, mahakama ya watoto tumeambiwa karibu itaanzishwa katika jengo lile liliopo Vuga pale la Mahakama Kuu. Naipongeza sana serikali kwa hili, naipongeza serikali kwa kuanzisha mahakama ya watoto, kwa sababu kumekuwa na wimbi kubwa la ukiukwaji wa haki za watoto, kumekuwa na wimbi kubwa la unyanyasaji wa haki za watoto. Naamini kuwepo kwa mahakama ya watoto, basi watoto watakuwa wamepata mkombozi, kwa hili naipongeza sana serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kaeleza wazi hapa Mhe. Waziri katika kitabu chake kwamba tumeanzisha mahakama ya watoto, ikiwa ni utekelezaji wa sheria namba 6 ya mwaka 2011 ya Kumlinda mtoto, nampongeza sana. Lakini Mhe. Mwenyekiti, hiyo sheria namba 6 ya kumlinda mtoto ina tatizo kidogo, pamoja na kwamba sisi ndio tulioipitisha. Kuna baadhi ya matatizo kwenye sheria ile. Kwa hivyo, kabla mahakama hii haijaanza kazi zake, hebu tuangalie kifungu namba 18 cha sheria hii ambacho kinazuia baadhi ya mashtaka ya jinai kusikilizwa pale kwenye mahakama ya watoto. Yaani mambo ya kuua, kuua bila kukusudia, uhaini pamoja na kubaka.

Mhe. Mwenyekiti, masuala hayo wanasema yasisikilizwe katika mahakama za watoto. Ok kama serikali inaona kwamba jinai hizi sio vyema kuzisikiliza kwenye mahakama ya watoto, kwa upande wangu mimi nina tatizo kidogo, lakini tatizo langu kubwa ni kwenye hii kesi ya kubaka. Kesi ya kubaka mara nyingi mtoto mwanamme ndiye atatuhumiwa kumbaka mtoto mwanamke. Sasa ukisema kwamba isikilizwe katika mahakama za kawaida isipelekwe kwenye mahakama za watoto, ina maana anapelekwa pale mtoto mwanamme tu, lakini mtoto mwanamke hapelekwi. Kwa hivyo, kuna tatizo la kisheria hapa, itakuwa tumewabagua watoto katika mahakama. Huyu mtoto mwanamme anakwenda kwenye mahakama ile, lakini mtoto mwanamke haendi.

Kwa hivyo, hii ni *bias ness* tunasema, kwa hivyo tunaomba sana hizi jinai zote zisikilizwe katika hii mahakama ya watoto, kwa sababu kwa kupitia hii kesi ya kubaka atakuwa anayeshitakiwa katika mahakama ile ni mtoto mwanamme na mtoto mwanamke atakuwa hahusiki basi tutakuwa tanawabagua na tunakwenda kinyume na katiba yetu ya Zanzibar, kwa sababu watu wote ni sawa mbele ya sheria. Kwa hivyo, hii sheria inajikwaruza kidogo na katiba ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende moja kwa moja katika suala zima la marekebisho ya katiba. Mhe. Mwenyekiti nchi yetu sasa hivi iko katika kipindi

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe una dakika tano za nyongeza.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu sasa hivi iko katika kipindi tete, sasa hivi nchi yetu inahitaji umoja zaidi kuliko mifarakano. Nchi yetu inahitaji umoja na mshikamano miongoni mwa Wazanzibari, tofauti zetu za kisiasa tuziache vifuani mwetu.

Mhe. Mwenyekiti, hii Tume ya kuratibu maoni inaanza kunipa wasi wasi. Sitaki niseme nimekosa imani nao moja kwa moja, lakini napata wasi wasi mkubwa kiasi ambacho inapelekea kukosa imani nao. Tume hii hivi sasa iko kisiwani Pemba. Kwa mfano majimbo mengine imeweka kituo kimoja tu, lakini katika kambi za kijeshi, kama kambi ya Alhamis *Camp* wameweka kituo kwa ajili ya majeshi tu, kambi ya polisi kwenye nyumba za polisi pale wameweka kwa ajili ya polisi na vikosi tu, kuna siri gani hapa Mhe. Mwenyekiti.

Nakuomba sana Mhe. Mwenyekiti, atakapokuja Mhe. Waziri anijibu suali hili kwamba wanaokaa Mfikiwa kwenye kambi ile ya polisi, wengi ni watu wa Tanganyika, maoni yatakayochukuliwa ni ya Tanganyika, wahesabiwe kama ni Watanganyika maoni yao wale na watakaochukua katika kambi ya jeshi wengi ni Watanganyika, yachukuliwe maoni yale kwamba ni Watanganyika sio Wazanzibari. Mimi ndio nikasema jambo lolote. Mimi siutaki Muungano. Mimi msimamo wangu ni kwamba siutaki Muungano, jambo lolote likitoka Bara kule lina matatizo na sisi, ndio nikawa naukataa katakata Muungano huu uliopo. Ilikuaje waende kwenye kambi za kijeshi wasiwaweke tu majeshi wakaenda kwenye kambi za uraia kuchukua mawazo. Tume ina tatizo na Mhe. Waziri mimi naanza kukosa imani na Tume hii, iweje iende kwenye vituo vya majeshi na iweje wale majeshi wasichanganyike uraiani kutoa mawazo yao kama raia wa kawaida, kuna jambo hapo linataka kupikwa.

Mhe. Mwenyekiti, ikiwa wamekwenda jeshini kule, kama kesho Tume inakwenda katika kijiji changu niko hapa kazini, nataka waziri aje aniambie Tume itakuja lini hapa kwenye Baraza la Wawakilishi kuchukua mawazo yangu. Waziri uje kuniambia Tume itakuja lini hapa kwenye Baraza kuchukua mawazo yangu ikiwa inawafuata watu jeshini, ikose kunifuata mimi hapa kazini, tena kazi ya wananchi na uniambie hasa Waziri lini Tume itakuja.

Mhe. Mwenyekiti, naona unaniambia muda umekwenda. Sasa niende kwenye Tume ya Kurekebisha Sheria. Tume ya Kurekebisha Sheria ni muhimu sana, sio kufikiria tu na kuziangalia zile sheria zilizopitwa na wakati. Lakini hata kufikiria kutunga sheria mpya zinazokwenda sambamba na mambo haya ya haki za binadamu na utawala bora. Mhe. Mwenyekiti, katika nchi hii kuna tatizo sana. Hivi ninavyokuambia kuna kitu kinaitwa *presidential impeachment* kumu-*impeach* Rais, kumuondosha madarakani Rais haiwezekani. Rais kajengewa mazingira, Rais wa Tanzania kajengewa mazingira ya kumpeleka kwenye *monarchy*, kwa sababu kama sisi tutasema Baraza linataka kumu-*impeach* Rais, wakati Rais yeye ndiye anayeteua Mkuu wa Majeshi, Mkuu wa Jeshi la Polisi, Rais huyo huyo ndiye anayemteua Mkuu wa Usalama wa Taifa. Sasa sisi tuna wasi wasi siku moja tunaweza kuja kufanya *presidential impeachment* hapa, akatoa amri tu Rais tukazungukwa na majeshi hapa tukakamatwa. Ukifika mkamate Spika, Naibu Spika, wakamate na Wawakilishi wapeleke ndani. Huo ni Usultani haiwezekani hivyo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe zingatia muda.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi naiomba Tume hii mambo ya sheria kama hizi, na kwa sababu tunaingia kwenye utawala bora na demokrasia. Ni lazima Rais akiwachagua hawa wakuu wa vikosi na wakuu wa majeshi, basi waletwe katika Baraza hili ili tuwathibitishe kwanza na tuwe na uwezo wa kuwaondosha, kwa sababu kama tutaweza kumu-*impeach* Rais, aah! Kwanza Baraza linakaa kukosa imani na Mkuu wa Majeshi, linakosa imani na Mkuu wa Polisi, Usalama wa Taifa, wote tunawaondosha na baadae ndio tunamuondosha Rais. Hii ndio demokrasia na utawala bora Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo, ili tusiende kwenye *monarchy*. Hii Tume ya kurekebisha sheria iwe makini katika hili na ione msingi mkubwa wa utawala ni watu na sheria zetu ziende kwenye kulenga watu na sio kwenye kulenga serikali. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nadhani nitaunga hoja baada ya kupata ufafanuzi wa kina na upembuzi yakinifu katika hoja zangu nilizozijenga. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kwa sababu wachangiaji tunao zaidi ya 10, kwa hivyo ningeomba sana tuzingatie muda na kila mtu ajipange vizuri kwa *point* zake. Anayefuata ni Mhe. Salmin Awadh Salmin, baadae atafuata Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii asubuhi ya leo nikaweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria. Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze mchango wangu moja kwa moja katika Idara ya Mahakama. Mhe. Mwenyekiti, idara hii ni moja kati ya idara ambazo zimeshikilia moja kati ya mihimili mitatu ya nchi, ambapo hapa Mhe. Waziri ameeleza kwamba jukumu kubwa la mahakama ni utoaji wa haki; na akaendelea kusema ili kuhakikisha kila mtu anaishi kwa amani na utulivu chini ya misingi ya utawala bora.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema kwamba mahakama ina jukumu la kutoa haki ili kuhakikisha kwamba kila mtu anapata haki zake kwa mujibu wa sheria. Mhe. Mwenyekiti, kumekuwa kuna malalamiko kutoka kwa wananchi juu ya ucheleweshaji wa haki zao, au kesi zao. Kesi nyingi zimerundikana na ushahidi Mhe. Waziri hapa ametueleza kwamba naomba Mhe. Mwenyekiti, ninukuu anasema;

“Mhe. Spika, kati ya kesi 5,477 zilizofunguliwa 1,308 ni za madai na 4,070 ni za jinai, ambao kesi 2,604 sawa na asilimia 48 zimetolewa uamuzi, ambapo ameeleza kwamba picha hii inaonakana kuwa bado kuna kesi nyingi ambazo hazijatolewa uamuzi na bado kuna mrundikano wa kesi”.

Mhe. Mwenyekiti, bado suala la kuharakisha utoaji wa maamuzi linaonekana ni tatizo na hili ni tatizo kweli na linaweza kusababisha mambo mengi. Mimi Mhe. Mwenyekiti, najiuliza ni sababu zipi zinazopelekea kesi kucheleweshwa. Kulikuwa kuna kilio cha maslahi mazuri kwa Waheshimiwa Mahakimu na Majaji, lakini sasa hivi *Alhamdulillah* kilio hiki kimeondoshwa, Mahakimu wamekuwa wakipata maslahi mazuri pamoja na Majaji, kwa lengo la kwamba kazi hizi za wananchi ziweze kufanyika kwa ufanisi. Lakini bado inaonekana kumekuwa kuna matatizo na kesi nyingi zimekuwa zinarundikana katika mahakama. Kwa kweli Mhe. Waziri hili sio jambo zuri na hii sio taarifa nzuri katika chombo hiki. Tunakuomba sana Mhe. Waziri, ulisimamie jambo hili na sisi tunaamini kwamba hakuna sababu za msingi za kucheleweshwa kesi kwa kiasi hiki.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri Mahakimu anao wa kutosha na kama huna wa kutosha utuambie kwenye chombo hiki kwamba huna mahakimu wa kutosha. Tuna wanasheria nje wa kutosha ambao hawana kazi, wanasomeshwa katika vyombo mbali mbali, iweje leo kesi ziwe

zinarundikana kiasi hiki. Kwa hivyo, hili Mhe. Waziri tunaomba uje utueleze utakapofanya majumuisho, ni sababu zipi hasa za msingi zinazopelekea kwamba kesi ziwe zinarundikana kwa kiasi hiki.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, kuna Mahakama za Kadhi za Wilaya. Mhe. Waziri umetueleza kwamba Mahakama hizi za Kadhi umeziimarisha. Umeweza kuwaajiri Makadhi saba wa Wilaya, ambao wamejaza nafasi zilizokuwa wazi. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kumekuwa na kilio kikubwa kwa wananchi juu ya Mahakama hizi za Kadhi. Miongoni mwa kesi ambazo zinawasilishwa katika Mahakama hizi za Kadhi, ni zile kesi za watoto wa kike kukataa kuozeshwa waume na mawalii wao, kesi hizi zimekuwa nyingi. Lakini la kusikitisha Mhe. Mwenyekiti, kesi hizi zinapofika kwenye Mahakama za Kadhi, zimekuwa hazitolewi uamuzi unaofaa, au uamuzi unaojenga, au uamuzi unaolenga mafahamiano mazuri kati ya mtoto na wazazi wake.

Mhe. Mwenyekiti, kesi nyingi zinazopelekwa kwenye Mahakama za Kadhi za watoto wanaokwenda kulalamika kwamba hawaozeshwi waume na mawalii wao, basi mahakama za Kadhi zimekuwa zinabeba jukumu la kuwaozesha watoto wale, jambo ambalo linaleta mfarakano mkubwa kati ya mtoto na wazazi wake, hii ni hatari. Badala mahakama zile za Kadhi kutumia nafasi zao kuwaunganisha watu, zimekuwa sasa zikifarakanisha zile koo, jambo hili ni hatari na linahitaji kufanyiwa marekebisho makubwa. Sasa hivi kumekuwa na mitindo ya watoto wari, wanapokataliwa kuozeshwa waume na mawalii wao basi hukimbilia mahakamani, ambapo wana uhakika kwamba akifika kule basi ataozeshwa moja kwa moja.

Hayo sio madhumuni ya mahakama hizi Mhe. Mwenyekiti, lazima mahakama zibebe dhamana ya kuhakikisha kwamba zinasuluhisha mambo kama haya na kuhakikisha kwamba kila mtoto anaozeshwa na walii wake, sio mahakama zibebe dhamana ya kuozesha kila mtu anayekwenda pale. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri hapa ameeleza kesi za zilizofunguliwa katika mahakama mbali mbali za Kadhi, ambazo kwa mwaka huu ni kesi 970. Lakini kesi zilizotolewa uamuzi ni kesi 217.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri utakapokuja kufanya majumuisho, uje unieleze kati ya kesi 970 kesi za madai, je ni kesi ngapi zilizofunguliwa za madai ya watoto ambao wamelalamika kwamba hawaozeshwi waume na mawalii wao, kwa kupitia katika kila wilaya na hizi zilizotolewa uamuzi uje utueleze hapa. Ni kesi ngapi ambazo watoto hao uamuzi wao umekuwa wa kuozeshwa na mahakimu wa makadhi wamewaozesha na kesi ngapi ambazo Mahakimu wa Kadhi wamekataa au wameweza kuzisuluhisha ili tupate picha halisi, lakini isitoshe katika Mahakama ya Kadhi ya Makunduchi, kesi zilizofunguliwa 20, lakini hakuna kesi hata moja iliyotolewa uamuzi, utueleze ni kwa sababu gani.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo Mhe. Waziri ningependa aje kututolea ufafanuzi, katika kitabu hiki kwenye hesabu hii, pamoja na kwamba kumetolewa ufafanuzi na Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo juu ya baadhi ya mafungu, hasa katika idara hii ya mahakama kuu ya Zanzibar. Pamoja na ufafanuzi ambao Mhe. Waziri ameutoa, lakini bado mimi nimekuwa na mashaka sana katika baadhi ya mafungu na kuangalia baadhi ya mafungu mengine.

Mhe. Mwenyekiti, katika eneo la posho maalum ambalo mwaka jana ilikuwa milioni 59, lakini mwaka huu kuna milioni 445,180,000 pesa za walipa kodi. Hiki ni kiwango kikubwa mno na ni tofauti kubwa mno, mbali ya ufafanuzi ambao Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ameutoa.

Kwa hivyo, mimi ninachotaka kusema Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho sasa katika eneo hili. Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo alituambia kwamba fedha hizi ni kwa ajili ya posho za mafuta na wale makarani na madereva ambao zamani zilikuwa mbali mbali, sasa hivi zimewekwa katika eneo hili. Kwa hivyo, uje utueleze Mhe. Waziri katika Mahakama Kuu, ni Majaji wangapi na Mahakimu wangapi ambao wanastahili kupewa posho ya mafuta, utupe uchambuzi. Lakini pia uje utueleze, kuna madereva wangapi ambao wanalipwa posho ya kila mwezi ya shilingi 100,000. Pia uje utueleze ni makarani wangapi wanaostahili kulipwa posho hili, ili tujiridhishe na hili fungu. Mahesabu yako uje nayo vizuri yalingane, vyenginevyo fungu hili tutalipunguza. Fungu hili limekwenda kiasi kikubwa mno.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije kwenye suala la mwisho juu ya marekebisho ya Katiba. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ametueleza juu ya marekebisho ya Katiba. Katika maelezo yake amesema kwamba katika suala hili, naomba nimnukuu;

“Kazi hii ni ya wananchi wenyewe na wala sio kazi ya Wizara ya Katiba na Sheria au Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kazi ya serikali kupitia wizara hii ni kusimamia yale yote ambayo wananchi watayapendekeza katika katiba hiyo. Wizara yangu inawahakikishia Wazanzibari kuwa itaendelea kutoa ufafanuzi kuhusu matakwa ya Katiba zetu mbili, ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, pale ambapo itahitajika. Wizara yangu imegawa katiba ya Jamhuri ya Muungano katika kila Wilaya kwa kupitia Wakuu wa Mikoa, katiba hizo ni kidogo hazitoshi, lakini pale tutakapozipata nyengine, basi pia tutaendelea kuzigawa”.

Hayo ndio maelezo ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria. Mhe. Mwenyekiti, suala la marekebisho ya Katiba ni suala zito, na Wizara ya Sheria na Katiba haiwezi kukwepa juu ya jukumu hili la kuwaelimisha wananchi. Na kwa sababu sisi hapa Zanzibar tunayo mambo mengi ambayo yanahitaji kurekebishwa katika katiba hiyo na wananchi hawaelewi. Kitendo cha kukaa kimya tukasema sisi jukumu la wizara, ni kutoa maelekezo pale yanapohitajika, wakati wa kuhitajika maelekezo ni huu. Hivi tujiulize ni wananchi wangapi wa Zanzibar wanaelewa katiba zao, wanaelewa matatizo yaliyomo ndani ya Muungano.

Mhe. Mwenyekiti, leo wananchi wa vijijini huko wanakwenda wakizungumza, lakini yale wanayoyazungumza hayaoani wala hayana misingi mizuri na marekebisho ya Katiba ya nchi yetu. Tunayo matatizo mengi sana ya kikatiba, ambayo yanahitaji wananchi wetu waelekezwe, ili matatizo yetu katika Jamhuri ya Muungano yaondoke. Leo wananchi wanapokwenda kuulizwa huko na Tume ya Katiba, watazungumzia suala la kuutaka Muungano na kutoutaka Muungano. Hayo yanahusu kitu gani katika mjadala huu, sio suala la kuutaka Muungano na kutoutaka Muungano. Tunazungumzia juu ya marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, ili tuone matatizo yetu yaliyokwamisha katika Katiba hii yanatekelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuna sheria ya mabadiliko ya Katiba ambayo imetoa hadidu rejea. Naomba ninukuu;

“Kifungu cha 9(1) cha sheria hii ya Mabadiliko ya Katiba inasema Mhe. Mwenyekiti, naomba kunukuu kidogo.

Sheria ya Mabadiliko ya Katiba kifungu cha 9(1) kinaeleza hivi:-

9(1) “Majukumu ya Tume yatakuwa ni:-

9(2) (1) Tume itaongozwa na misingi mikuu ya kitaifa na maadili ya kijamii ya kuhifadhi na kudumisha mambo yafuatayo:-

(a) Kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano;

Hii ndio *term of reference* ya tume pamoja na maadili makuu ya kitaifa ndio haya kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa wananchi wanapokwenda kuhojiwa, kuulizwa na kusema kwamba mimi nataka muungano, na yule mwengine akasema mimi sitaki muungano kweli tunaisaidia Zanzibar. Hivi kweli suala hili litatatua matatizo yetu ya Wazanzibari katika Muungano, hili litachukuliwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sehemu ya nne ya sheria, ambapo ibara ya 17 imezungumzia utaratibu wa utendaji kazi wa tume, naomba kunukuu kidogo.

Sehemu ya Nne ya sheria, ibara ya 17(1) na (2) inaeleza hivi:-

(1) "Tume itatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria hii na hadidu rejea.
(2) Kwa madhumuni ya utekelezaji wa kifungu kidogo hichi cha (1) Tume itafanya kazi zifuatazo:-

(a) Kuandaa na kuendesha programu za kuelimisha juu ya madhumuni ya Tume;
(b) Kuitisha, kusimamia mikutano na mabaraza katika sehemu na nyakati mbali mbali kama itakavyoamua.
(c) Kutathmini na kuchambua kwa kutofautisha maoni ya watu, wananchi yanayokubaliana na yale yasiyokubaliana.
(d) Kutayarisha na kuwasilisha ripoti kwa kuzingatia hadidu rejea.

Mhe. Mwenyekiti, hiyo ndiyo kazi ya tume kwa mujibu wa sheria. Sasa Mhe. Mwenyekiti, Chombo hichi cha Baraza la Wawakilishi kina dhima kubwa katika nchi hii. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina dhima kubwa juu ya jambo hili, Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria una dhima kubwa juu ya nchi hii, unapowaachia wananchi tume imekuja na inakwenda kule wanazungumza tu kwamba mimi sitaki muungano, haitusaidii nchi hii na wala mambo hayo hayachukuliwi kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Kwa kweli mimi namshangaa sana Jaji Warioba Mhe. Mwenyekiti, wakati alipokuja hapa na kusema kwamba tutayachukua yale yote ambayo watu wanayosema, kwamba tunataka Muungano au hatuutaki Muungano, yule anawapotosha Wazanzibari na wala hawasaidii Wazanzibari, kwa sababu anajua na yule ni mwanasheria kwamba hili halichukuliwi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nadhani atakuja kutoa takwimu kwamba wangapi wamesema wanataka, na wangapi hawataki basi si yamekwisha, lakini hadidu rejea zitakazochukuliwa na tume ni zile zinazozungumzia marekebisho ya Katiba, na hadidu rejea moja iliyozungumzwa humu ni kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo tume inatakiwa izingatie. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, lazima tuwasaidie wananchi wetu, turekebishe Katiba yetu tunayo mambo ya muhimu ambayo yanahitaji kurekebishwa, ambapo wananchi wanahitaji kuelimishwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tunayo mambo ambayo tunahitaji kuyazungumza, kuna malalamiko ya kuongezwa masuala ya Muungano katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano kutoka 11 hadi 22, na sisi ndio tunaolalamika na huu ndio wakati wetu sasa wa kuyapunguza yale ambayo hayafai. *(Makofi)*

Lakini tunakapokwenda kuzungumza tunataka au hatutaki Muungano hatima yake nini, huu Muungano utavunjika, Mhe. Mwenyekiti hauvunjiki Muungano, isipokuwa itakuwa tumepoteza nguvu zetu bure, jambo la msingi ni kurekebisha Katiba yetu. *(Makofi)*

Vile vile tutapata nafasi ya kusema aina gani ya Muungano tunaoutaka, kwa sababu wengi wanasema kwamba Muungano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hauna mfano popote duniani na watu wanasema hapa. Lakini kuna nchi ambazo zimeungana kama vile Marekani wameungana *United States of America*, kuna Uingereza nchi zimeungana *United Kingdom*, pia Falme za Kiarabu *United Arab Emirates* wameungana ni nchi mbali mbali. *(Makofi)*

Sasa tuseme tunataka Muungano wa aina gani, tunataka wa Marekani au Uingereza ama Falme za Kiarabu tuseme. Lakini tutakaposema sisi hatutaki Muungano hatuwasaidii wananchi, kwa sababu kwenye *terms of references* hii hakuna na tunawapoteza watu na wala hatuwasaidii. *(Makofi)*

Jaji Warioba hakuja hapa kutusaidia Wazanzibari, isipokuwa ameliangalia jambo gani liko ndani ya vichwa vyetu ametujaza, na sasa matokeo yake wananchi wanazungumzia kutaka na kutotaka Muungano hii haisaidii na wala hatuwasaidii wananchi Mhe. Abubakar Khamis Bakary. *(Makofi)*

Kwa kweli tunayo matatizo kama vile kero za mgawanyo wa madaraka katika nafasi za juu, na tunapiga kelele hapa, hakuna *formula* inayojulikana katika Jamhuri ya Muungano, kwamba Rais wa Jamhuri akitoka upande mmoja na kipindi chengine kinachokuja atoke upande mwengine. Kwa hiyo, lazima kuwe na *formula*, na tutakaporekebisha Katiba yetu ndipo tutapopata *formula* juu ya Muungano. *(Makofi)*

Vile vile tunayo malalamiko juu ya nafasi za kazi katika Jamhuri ya Muungano, tuseme kwamba nafasi za kazi katika Jamhuri ya Muungano zigaiwe kwa uwiano kwenye Katiba hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuna masuala ya mafuta yanayotutatiza, tuseme suala la mafuta litolewe kwenye Muungano. Pia kuna matatizo ya mgawanyo wa fedha na sisi tunapewa 4.5, tuseme kwamba jambo hili liwekwe kwenye Katiba sasa badala ya 4.5 tupate kiwango fulani katika mambo ya Muungano kama vile *GBS* pamoja na mambo mengine. Hayo ndiyo mambo yatakayotufaa ndugu zanguni. Lakini kuzungumzia vyenginevyo vyovyote tutakuwa hatuisaidii nchi hii. *(Makofi)*

Tuzungumzie masuala ya uchumi, tuzungumzie namna gani tutaendesha nchi yetu, pia tuzungumzie namna gani nchi yetu itakuwa na maamuzi katika masuala mbali mbali na sio suala la kuvunja Muungano. Kwa kweli tunaweza kuwa na maamuzi ndani ya Muungano, jambo la msingi ni kurekebisha Katiba na tuwaelimishe watu.

Lakini leo tunapowapotosha watu tukawaambia hatutaki Muungano hii hatuwasaidii, Mhe. Abubakar Khamis Bakary ni jukumu lako kuwaelimisha watu. Mhe. Mwenyekiti, leo tunaambiwa kwamba jukumu la kuelimisha watu ni *NGO's* pamoja na Jumuia mbali mbali. Hapa Zanzibar kuna jumuia gani ambayo inaelimisha watu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, zungumza na Kiti na angalia muda.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, namalizia muda.

Mhe. Mwenyekiti, tunaposema Jumuia za Kiraia na taasisi nyengine ndizo zenye mamlaka ya kuelimisha watu. Hebu tuangalie hapa Zanzibar kuna jumuia ngapi zinazoelimisha watu juu ya jambo hili, mbali ya jumuia ya Uamsho, ambayo badala ya kusaidia watu inawapoteza watu. Kwa kweli lazima tukubaliane kwamba Jumuia ya Uamsho haisaidii Wazanzibari na inawapoteza.

Kwa hivyo, ni jukumu la serikali na wizara yako Mhe. Waziri kuwaelimisha watu na kuwarejesha katika mstari badala ya kuacha watu wanapotea, na wala tusiipoteze nafasi hii bure, kwa sababu hii ni nafasi adhimu sana, ambayo tunatakiwa Wazanzibari tuwe wamoja, tushikamane, tuone tunatatua matatizo yetu ambayo ni matatizo katika Jamhuri ya Muungano. Vyenginevyo nafasi hii tutaipoteza na halafu baadae tutakuja kujuta, kwa sababu ya kusema tunataka au hatutaki Muungano. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Muungano huu utaendelea kuwepo, na hii hadidu rejea tunayoizungumza hapa imeshazuia kabisa katika suala la kuwepo au kutokuwepo Jamhuri ya Muungano. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nasaha zangu kwa Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, pamoja na kukwepa majukumu ya kuwaelimisha wazanzibari na kuwaachia waseme na badala yake wanasema visivyo, wanazungumza mambo ambayo hayaisaidii Zanzibar kwa mujibu wa Sheria hii ya Marekebisho ya Katiba. *(Makofi)*

Kwa hivyo, naomba awaelimishe watu wafahamu nini madhumuni ya sheria hii iliyotungwa, nini kilichopo wazanzibari mbele yao wakati huu, na Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi sisi tuna dhima juu ya wananchi, tunapokaa hapa tukawaambia hatutaki Muungano hatuwasaidii, Muungano huu hata tukisema utakuwepo, upo na utaendelea kuwepo. *(Makofi)*

Jambo la msingi tutumie nafasi yetu tuwaelimishe wananchi nini kinahitajika sasa kirekebishwe katika Katiba, ili tunyanyue uchumi wetu kwa manufaa ya wananchi. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ahsante sana. Sasa anafuata Mhe. Hamza Hassan Juma na baadae atafuata Mhe. Hija Hassan Hija.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nataka nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nikatoa machache kabisa katika Hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuanzia nataka niseme siungi mkono hoja na ninayo sababu yangu. Mhe. Mwenyekiti, nitatumia kifungu kile cha 98(6) (b), (c), (e) na kama hakuna uwezekano nitatumia (g) na nimesema hivi kwa makusudi.

Mhe. Mwenyekiti, hii ni Wizara ya Katiba na Sheria, najua rafiki yangu ananitizama Mhe. Abubakar Khamis Bakary rafiki yangu sana, ndio maana nikajaribu niwe muwazi mapema. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sababu yangu ya kuzuia fungu au kuondoa shilingi 100 kuhusu suala la Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo, haiwezekani na hii ndio Wizara ya Katiba na Sheria. Wizara hii Mhe. Waziri anatakiwa asimamie haki za wananchi wote wa Zanzibar. Sasa leo Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo wamenyimwa haki yao, Rais wetu ametangaza kwamba ataongeza maslahi kwa watumishi wake wote na sio kwa ubaguzi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, juzi nilipokuwa nikichangia Wizara ya Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora nilitoa angalizo hili. Lakini Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora alikuwa hana majibu kwangu mimi, isipokuwa majibu yangu atakuwa nayo Mhe. Waziri

wa Katiba na Sheria. Kwa mfano, Mahakimu wa Mikoa na Wilaya wamezidishiwa mshahara pamoja na posho, lakini hawa Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo wamekosa nini? *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora anakuja kutuambia maana yake Tume ya Utumishi iliwasahau, suala la kusahau sio kosa lao Mahakimu. Kwa hiyo, mimi nitakuja kuzuia fungu la ile Tume ya Utumishi wa Mahakama ndio hapa nitakuja kung'ang'ana nalo, kama wenzao wamewasahau kuwaongeza mishahara yao, sasa nazuia na wao wasipate mishahara, waone raha. *(Makofi)*
Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa ninayo mambo mengi ya kusema, na pengine nikipata majibu mazuri basi nitaachia bajeti ipite. Sasa naomba nije kwenye Ofisi ya Mufti hapa kidogo naparapara tu na wenzangu wengi wameshasema.

Lakini mimi naomba kutoa angalizo, kwa hiyo naomba sana waliangalie Baraza la Wawakilishi la hivi sasa ni tofauti na Baraza la Wawakilishi lililopita, kwa sababu serikali yetu imejitahidi kutoa uhuru kwa wananchi na taasisi zote wafanye kazi zao kwa uwazi kabisa, tunamshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa tunahoji kila kitu katika matumizi ya fedha za umma, tunaomba sana Ofisi ya Mufti na hizi taasisi zote za Kiislamu ambazo tunazozipitishia bajeti zake hapa, tunaomba wawe waadilifu sana na mpaka katika kutoa hizo talaka, tusije tukahoji hapa. Kwa kweli taasisi muhimu kama hizi za kijamii zinazoheshimika kuja kuzihoji hapa kwa mambo ambayo wamekiuka taratibu zao wenyewe, itakuwa si vizuri. Sasa hili naliomba kwa upande wao. *(Makofi)*

Suala jengine tumeshasema miaka mingi kuhusu suala la mishahara ya walimu wa vyuoni. Mhe. Mwenyekiti, hivi juzi nilimsikia Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anazindua au alipokuja pale Bwawani kuja kuzungumzia Suala la Uanzishwaji wa *Baitil-mali* (Zaka).

Mhe. Mwenyekiti, hapa naona ndipo pa kuanzia kwamba hizi Zaka ziangaliwe kwamba nyengine zigaiwe watu masikini, lakini itafutwe *percent* angalau kuwasaidia posho na wala si lazima mshahara, kwa sababu mshahara utaleta mambo mengi viinua mgongo na serikali itakuja kuwa haina uwezo, lakini angalau posho ya kila mwezi kwa walimu wa Madrasa waweze kusaidiwa.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye Mahakama. Mhe. Mwenyekiti, nataka niulize kwamba nchi yetu inaongozwa na Katiba na

Utawala Bora, suala la *separation of power* na serikali inaleta mapendekezo ya miswada ya sheria na sisi tunaipitisha na baadae kuwa sheria.

Sasa sisi kazi yetu kuisimamia serikali, je zile sheria tulizozipitisha kweli inazifuata? Ndio maana inapokiukwa tu sheria tunakuja hapa na kumuhoji Mhe. Waziri.

Lakini tunacho chombo chetu chengine ambacho ni Mahakama, sisi vyombo viwili tunayo nafasi ya kusema. Kwa mfano, serikali mnasema huko mbele na sisi *back benchers* huku nyuma Wawakilishi wa wananchi tunasema, lakini kuna chombo kimoja hakina nafasi ya kuingia humu Barazani kikajisemea.
Sasa Mhe. Mwenyekiti, tunatunga sheria na Mahakama zinatoa maamuzi, baada ya Mahakama kutoa maamuzi halafu serikali inakuja kuunda tume kuchunguza yale maamuzi yaliyotolewa na Mahakama, sasa hii inakujaje? Kwa mfano, kuna kesi ambazo zinahukumiwa katika Mahakama ya Zanzibar na kukatiwa Rufaa zikaenda Mahakama ya Rufaa wameshinda, lakini baadae kesi ile inakuja kuanza kujadiliwa tena, hivi serikali haiamini Mahakama. Mhe. Waziri nakuomba kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati atakapokuja kufanya majumuisho anisaidie jawabu.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nipongeze sana kwamba kuna jumuia au taasisi ambayo imeundwa hivi sasa na imeunganisha madhehebu yote ya dini, Waislamu, Wakristo na wengine wanaoabudu kila kitu. Kwa kweli naipongeza sana na ile itatusaidia katika kuondoa hii mitafaruku midogo midogo inayokuja katika masuala ya dini.

Kwa hivyo, naomba wapewe *support*, kwa sababu pale kuna mchanganyiko wa mawazo ya watu tofauti na hiyo ndio demokrasia, maana demokrasia using'ang'anie lile unalolitaka wewe tu na ule unaitwa udikteta, demokrasia achia uhuru wa mawazo, na Katiba zetu zote mbili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kifungu cha 18 na Katiba ya Zanzibar pia imetoa uhuru wa wananchi waseme wanachokitaka almuradi wasikiuke sheria. Mhe. Mwenyekiti, hili ilikuwa *point* yangu nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nakuja katika suala la Katiba. Lakini kabla sijaingia hapo kwa bahati Mhe. Mwenyekiti tunakushukuru sana ofisi yako hivi sasa pamoja na Mhe. Spika, unajitahidi kutupa mafunzo kila siku. Kwa mfano, juzi katika mafunzo tuliyopata *weekend* iliyopita tumeambiwa kwamba hapa tayari tunacho Kitengo chetu cha Utafiti. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kitengo hichi tukipe uwezo na Mhe. Mwenyekiti nakuomba, na hili ni agizo nakuomba umwambie Mhe. Spika, kwamba kitengo hichi tukipe nguvu na uwezo, ili kiweze kutusaidia katika majukumu yetu. Kwa mfano,

leo katika wizara tulizopitisha katika bajeti hii kuna mafungu mbali mbali ambayo tuliyoyahoji na sisi hatuna muda, sasa kitengo chetu cha Utafiti kichukue mafungu yote yale na utafiti wenyewe utakuwa mdogo tu, kwamba bajeti iliyopita mafungu yalikuwa madogo, na bajeti ya mwaka huu kwa nini yakapanda tunahitaji *breakdown*. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, Kitengo cha Utafiti ukiagize kuanzia leo Mhe. Mwenyekiti kikatufanyie kazi, na ije ituletee pamoja na angalizo alilolitoa Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kitengo hichi kitamsaidia sana ingawa hayupo. *(Makofi)*
Mhe. Mwenyekiti, sasa nizungumzie kuhusu Katiba. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuna watu tayari wameshakubali kunikopesha dakika kama muda wangu utakuwa umekwenda sana.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nizungumzie historia ya Katiba. Kwa kweli nataka nimpongeze sana Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa nini? Katika mtu ambaye anayeheshimu demokrasia mmoja ni yeye, kwa sababu hili suala la Katiba nchi yetu hapa tokea kupata uhuru wenzetu mwaka 1961 na sisi Mapinduzi mwaka 1964 imepita katika mikondo mingi ya utawala. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mtu wa mwanzo kumpa ujasiri au pongezi Rais Msataafu Mhe. Ali Hassan Mwinyi, kwa wakati wake ndani ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikuwa inasema kwamba Tanzania itaongozwa katika mfumo wa chama kimoja. Lakini tena kwa wakati wake huo alikubali maoni ya wananchi baada ya vuguvugu kuanzisha Mfumo wa Vyama Vingi mwaka 1992. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ule ulikuwa ni ujasiri Katiba imempa nguvu Rais wa Jamhuri ya Muungano, kwamba Tanzania itakuwa ni nchi inayofuata mfumo wa chama kimoja na ndio Katiba hii ilitengenezwa katika misingi hiyo.
Kutokana na demokrasia kupea kwa upevu wa kisiasa Mhe. Ali Hassan Mwinyi alianzisha Mfumo wa Vyama Vingi na tukaukubali watanzania tukaingia, tena walihojiwa watanzania wakaulizwa je, mnataka Mfumo wa Chama Kimoja au Vyama Vingi na watanzania wakatoa maoni yao na serikali ikaanzisha Mfumo wa Vyama Vingi, na Katiba hii ikafanyiwa marekebisho.

Lakini jambo gani ambalo nakusudia kumpongeza Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati alipokuwa akizindua Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitoa tamko na kusema ataondoa mgogoro au mpasuko wa kisiasa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tunamshukuru sana na mpasuko ameuondoa au hakuuondoa? Mpasuko ameuondoa. Kwa hiyo, kauli yake anayoisema anaitekeleza. *(Makofi)*

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, watu walikuwa wakijiuliza mpasuko huo atauondoa vipi, kwa sababu CUF walikuwa ngangari na CCM walikuwa ngunguri, tukasema Kikwete yuko kule atauondoa vipi huku. Mhe. Mwenyekiti, yule mwenzetu ana akili sana, na kwa sababu ameshawahi kuwa Waziri wa Mambo ya Nje ameshakaa katika nchi na ametembea nchi tofauti na kuona migogoro mbali mbali jinsi inavyotatuliwa. *(Makofi)*

Mhe. Rais wetu na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi akaamua kuwaagiza Makatibu Wakuu wa Vyama, Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi wakati ule Makamba na Katibu Mkuu wa CUF wakati ule Maalim Seif Sharif Hamad; ambaye hivi sasa ndiye Makamo wa Kwanza wa Rais. Kwa hivyo, kaeni Makatibu Wakuu angalieni kwani mna matatizo gani walikaa huko na walitumia fedha nyingi hazipungui karibu shilingi milioni 27 fedha za walipakodi na kuangalia nini tatizo, nipe nikupe na watu wakakubaliana na ngoma ikaletwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, makubaliano yale yakapelekwa mpaka Dodoma katika Halmashauri Kuu ya Taifa, Mhe. Mwenyekiti, samahani kwa sababu hichi si kikao cha chama, lakini tunazungumza historia. Kikao cha chama kikafanya maamuzi kwamba Zanzibar kuwe na Serikali ya Umoja wa Kitaifa, na wengine wakapinga ndani ya kikao tena ni halali yao, kwa sababu ni uhuru wao.

Lakini suala likaja na tukaja zetu mpaka hapa Zanzibar na lilisita kidogo kutokana na kutokuaminiana pamoja na kuelewana. Mhe. Mwenyekiti, kunguru anaishi miaka mingi kwa sababu ya hofu, na ukiwa na hofu utafanya jambo lako kwa utulivu na kuliko kila unachoambiwa *hewallah*. Kwa kweli ukiwa na hofu kila unachoambiwa unajiuliza hichi ninachoambiwa vipi, ngoja nikichambue na halafu niangalie na *impact* yake. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya wenzetu kuondoa hofu wakarudi wakakutana Katibu Mkuu wa Chama cha CUF akamuona Makamo Mwenyekiti wetu wa Chama cha Mapinduzi Zanzibar wakanywa maji Ikulu, ndivyo walivyotwambia. *(Makofi)*

Matokeo yake wakaja wakawashawishi wananchi wao pamoja na wanachama, na tulishuhudia Maalim Seif Sharif Hamad alivyopigwa viatu pale Uwanja wa Demokrasia na wala hakupita njia ile aliyozoea na alitokea kwa mlango wa

nyuma, kwa sababu wananchi hawaamini kinachoendelea na wala hawaamini maneno ya viongozi. Lakini baadae hivi sasa wameanza kuamini kumbe kweli yanawezekana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Dkt. Karume naye mwanzo sio kama aliukubali huu mfumo, lakini baada ya maamuzi kupitishwa walisema wakaulizwe wananchi, tuliulizwa hatukuulizwa? Tuliulizwa na wananchi wakapiga kura, na katika kura inaitwa nipe nikupe. *(Makofi)*
Sasa ndio maana pale ninaposema kwamba jambo lolote tutakaloliamua tusiangalie nguvu, uwezo na mabavu yetu, isipokuwa tuangalie maamuzi ya wananchi Katiba yetu ya Zanzibar hivi sasa imewapa uhuru mkubwa sana wananchi kuliko sisi viongozi, na wala tusije tukaanika karafuu wakati wa masika. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuanika karafuu wakati wa masika kwa nini? hutaki kusikiliza wananchi na unataka kufanya maamuzi unayoyataka wewe, maamuzi unayoyataka wewe kama wananchi hawakuyatekeleza basi mzee umepigwa ngwara, ndio ile kuanika karafuu wakati wa masika.

Mhe. Mwenyekiti, tumeunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa, na leo kuna viongozi hawaitaki Serikali ya Umoja wa Kitaifa tena wana dhamana ndani ya Serikali. Mhe. Mwenyekiti, ndipo pale tuliposema kwamba hawa viongozi wengine waliobakia nao wateuliwe wale kiapo kwa ajili ya kuitii hii Katiba. *(Makofi)*

Kwa mfano, mtu unamwambia anakaimu tu miaka miwili, hii bado kwa sababu huku nyuma ilikuwa hii haipo, na ilikuwepo ile nyengine ya *cream* na hivi sasa tunayo ya kijani *pure* hii Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Sasa leo kuna mtu anasema wale wanasema vile musiwasikilize wanashirikiana na upinzani ah! Hatushirikiani, isipokuwa Katiba ndiyo iliyosema tushirikiane na upinzani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, leo kuna Mkuu wa Mkoa mmoja na Makamo wa Rais hayupo, lakini tunamuomba Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, kuna Mkuu wa Mkoa mmoja anasema sisi tunashirikiana na wapinzani, kwanza wao lazima waseme hivyo kwani hawajala kiapo kwa ajili ya kuitii hii. Kwa hivyo, ndipo pale tunaposema kwamba hebu hii Katiba tuitekeleze yote, halafu tufanye kazi na baadae mwenye kuikiuka hii bakora. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, unaposema Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Mbarouk Wadi Mussa, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk wanashirikiana na wapinzani. Sasa kama Dkt. Shein anashirikiana na Maalim Seif kwenye *Cabinet*, na wale si ndio wakubwa wetu, basi mtoweni Maalim Seif katika Vikao vya *Cabinet*

na mimi sitozungumza tena na Mhe. Hija Hassan Hija wala Mhe. Ismail Jussa Ladhu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, siku moja nilisema hapa kwamba itolewe elimu ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa, bado elimu haijatolewa. Mhe. Ali Mzee Ali nitakuja kuhoji fedha mlizotumia Ulaya kwenye ile tume yenu, Mhe. Ali Mzee Ali, Mhe. Haji Omar Kheir, na wengine mlipokwenda kuwaeleza wenzetu Mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, kumbe vile bado wazanzibari hawajaelimika. Kwa kweli matumizi yale na wala sitaki kusema matumizi mabaya, kwa sababu yametuletea faida nzuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Wizara ya Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora hivi sasa ikatolewe elimu kwa viongozi wote kila aliyekabidhiwa dhamana, kwa sababu tatizo sisi tunaambiwa wakati mwengine tunaambiwa wanawasakama mawaziri wa CCM, na humu hamna Waziri wa CCM wala CUF, isipokuwa hawa wote ni Mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Sasa leo Mhe. Nassor Ahmed Mazrui akifanya madudu nimuachie au nimsakame Mhe. Mazrui, Mhe. Omar Yussuf Mzee akifanya madudu nimuachie kwa kuwa CCM tutakuwa tunajenga au tunabomoa nchi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi siku zote nasema Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar ni mfumo wa peke yake duniani. Serikali zote za Umoja wa Kitaifa kuna vyama havikushinda na Zanzibar Chama cha Mapinduzi kimeshinda.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, umebakiwa na dakika tano za ziada pamoja na muda uliokuwa umeazimwa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nilikwambia unikopeshe. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Katiba hii na kawaida ya bajeti dakika 30, kwa hiyo pia unayo haki ya kuweza kunikopesha pia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Katiba hii ya Zanzibar hivi sasa Zanzibar hakuna upinzani kwa mujibu wa Katiba hii ya Zanzibar, kwa sababu unaunda chama kwa ajili ya kushika dola na kushika dola ni kuunda serikali, na Katiba yetu imeshasema ikishinda CUF au CCM, mawaziri wa CCM watakuwemo, ikishika CCM mawaziri wa CUF watakuwemo, sasa kuna upinzani uko wapi hapo na hiyo ndio Serikali ya Umoja wa Kitaifa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nadhani na serikali nyengine za Kiafrika waige mfano huu na Zanzibar sisi ndio walimu wa demokrasia, kwa sababu siasa Zanzibar imeanza zamani sana kuliko hata hizo nchi nyengine za Kiafrika. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba nizungumzie hiyo Katiba yenyewe. Mhe. Mwenyekiti, tunayo marekebisho ya Katiba, mimi mwaka jana nilipokuwa nikichangia bajeti kama sikosei Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, niliiomba serikali kwamba kuna kitu kinakuja suala la Katiba mpya, je serikali yetu imeandaa mpango gani wa kutoa elimu? Kwa sababu wananchi wetu wengi hawaijui Katiba, na tuliiomba Wizara ya Katiba na Sheria, Mhe. Abubakar Khamis Bakary, itoe Katiba nyingi hizi ili itoe elimu. Kitu hicho hakikufanyika. Matokezeo yake ndiyo yale tuliyosema, sasa hivi tunaanika karafuu wakati wa masika, yale mategemeo ya kuvuna sasa hivi kuna hatari mwenzangu Mhe. Salmini Awadh, kasema. Leo kuna wananchi huko tayari wameshapotoshwa, wanaambiwa kabla ya hayo maoni waulizwe kwanza wanautaka, hawautaki.

Siku hizi kwa bahati mbaya tunaona haya hata kwenda kwenye maskani zetu. Maana ukifika tu unaulizwa unautakaa. Mimi nautaka maana ndio nnao, sasa nitasema vipi, nnao ndio nisiutake, hiyo ndiyo hali iliokuwepo. Tena ni vijana wangu wenyewe je, kama vijana wa upinzani wataniuliza vipi? Mhe. Mwenyekiti, naomba tusianike karafuu wakati wa Masika. Tukawaelimishe wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sasa nataka nije kwenye hayo marekebisho yenyewe ya Katiba. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania hapa tunabishana bure tu. Angalia kifungu cha kwanza cha Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kinasemaje?

Tanzania ni nchi moja tena ni Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini sisi hapa tunatumia Katiba mbili aidha hii moja itabidi tuichane. Katiba ya Zanzibar inasema vipi kifungu cha mwanzo, naomba nikisome:-

> "Zanzibar ni nchi ambayo eneo la mipaka yake ni eneo lote la Visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na Visiwa vidogo vidogo vilivyozunguka bahari yake ambayo kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ilikuwa ikiitwa Jamuhuri ya Watu za Zanzibar."

Mhe. Mwenyekiti, Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania inasema kifungu cha 2, kwamba:

> "Eneo lote la Jamuhuri ya Muungano ni eneo lote la Tanzania Bara na eneo lote la Tanzania Zanzibar pamoja na bahari yake ambayo Tanzania inapakana nayo."

Kwa hiyo hii Katiba ya Jamuhuri ya Muungano inaikubali Zanzibar, lakini ni eneo, haikufafanuliwa kama Mkoa au Wilaya au kijiji au Kanda. Katiba ya Zanzibar ilipoona Katiba ya Jamuhuri ya Muungano ina masuala yasiyokuwa na majibu ikatoa ufafanuzi. Haya maeneo ndio ambayo wananchi wetu wayajue. Kama wanakubali kwamba Zanzibar si nchi basi kifungu hichi kiendelee hivi hivi. Mimi sisemi watu waseme nini.

Nakuja katika ibara ya 64 ya Katiba ya Jamuhuri wa Muungano wa Tanzania. Ibara ya 64 inasema kwamba:

> "Mambo yote ya Muungano pamoja na sheria zote za Jamuhuri ya Muungano zitatungwa na Bunge la Jamuhuri ya Muungano na itasimamiwa na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano na mamlaka yote ambayo sio ya Muungano yatashughulikiwa na Zanzibar"

Kwa hiyo hapa sisi tunapiga kelele tunataka tuanzishe sheria inayohusu mafuta. Ukija katika orodha ya kwanza ya mambo ya Muungano hili ni suala la 15, limewekwa katika orodha ya mambo ya Muungano. Inamaana sisi tukiunda Sheria ya Mafuta sawa itakuwepo sheria lakini itaweza kufanya kazi kama vile tulivyokusudia. Tumeshaambiwa katika Katiba ya Jamuhuri ya Muungano kwamba Sheria yoyote itakayotungwa Zanzibar kwa mambo ya Muungano, sheria hiyo itakuwa *batil*. Haya ndiyo mambo ambayo wananchi wetu wanatakiwa wayajue, vifungu kama hivi wananchi wetu wanatakiwa wavijue. Lakini vifungu hivi wananchi wetu hawavijui.

Jengine vijana wetu hasa wa michezo kila siku wanapiga kelele kwamba Zanzibar tunataka tutambulikane kimataifa, tujiunge na FIFA. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamuhuri ya Muungano mambo ya Kimataifa, mambo ya nje ni mambo ya Muungano. Zanzibar mambo yetu ni ya ndani tu ya Zanzibar na hatuna maamuzi mengine yoyote kwa mambo ya nje, isipokuwa kwa mambo ya Zanzibar. Je, kifungu hiki kiendelee kubaki au kiondoke?

Wananchi na vijana wetu wambao wana mambo ya michezo wanataka Zanzibar isijiunge na FIFA basi tukiache kama hivi kilivyo. Lakini kama Zanzibar inataka ijiunge na FIFA basi tuseme haya mambo ya nje sasa hivi kila mmoja ashughulike na yake. Na mambo mengine kama kujiunga na Jumuiya za OIC na Jumuiya nyengine, hata ushirikiano wa kitamataifa. Tumesema Muungano wetu mambo ya kiuchumi kila mmoja ashughulikie yake. Mambo ya nje ni uchumi kama hujashika mambo ya nje huna uchumi. Mhe. Mwenyekiti, haya ni mambo ambayo wanatakiwa wananchi wetu vile vile waweze kuyajua.

Zanzibar tumeunda sheria ambayo imo ndani ya Muungano, suala la Bandari. Sisi tumeunda Shirika la Bandari Zanzibar na linafanya kazi na wala hatujaambiwa tumekiuka Katiba. Shirika Bandari linafanya kazi lakini sheria ya kuunda Shirika la Bandari kwa mujibu wa Sheria ya Katiba ya Muungano, sheria zile tumekiuka Katiba ya Muungano. Sasa mambo kama haya tunatakiwa tuyaweke sawa.

Hata hili suala la mafuta na gesi ni jambo la Muungano lakini tujiulize liko katika Wizara ya Muungano. Katiba yetu ya Jamuhuri ya Muungano, mimi nakubaliana na yule msomi aliyeandika kitabu akasema humu kuna maswali yasiyokuwa na jawabu. Sasa kama wasomi, wanasheria wakubwa Zanzibar, wanazuoni wameshasema Katiba hii haina majibu. Leo wananchi ukawambie wananchi wa kawaida mtu ambaye hajui hata hii Katiba inasema nini, atakwenda kuzungumza kitu gani.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niendelee tena kumpongeza Mhe. Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Suala hili leo tunalolijadili kama ingelikuwa hajaunda hii Tume tungekuwa tunakiuka Katiba ya Muungano. Kwa sababu marekebisho ya Katiba ni suala la Muungano na ndio maana hata wale wanaosema kwamba zile kura zitakazokuja kupigwa kwa wananchi katika maoni zihesabiwe hapa. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamuhuri ya Muungano suala hili lililopigiwa kura la Katiba ni suala la Muungano.

Inamaana Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar haina mamlaka ya kuhesabu kura ikatoa matokeo. Kwa hiyo sisi kwa mambo ya Muungano hatuna la kusema. Mimi nataka niseme Rais ya Jamhuri ya Muungano ilipokuja hii Tume ilipokuwa ije Kamati ya Bunge aliituma akenda katika Mikoa, ikenda Dodoma na Dar-es-Salaam, ikaja Zanzibar. Ilipokuja Zanzibar mimi ndiyo niliyesimama pale Bwawani nikamwambia Mhe. Samuwel Sita, nikamwambia hebu angalia hii Rasimu hata haikumtaja hata kumtambua Rais wa Zanzibar. Tukakataa tukasema sio kumtambua tu Rais wa Jamuhuri ya Muungano kwa kushauriana na kukubaliana na Rais wa Zanzibar.

Tunashukuru yale maoni yetu yalichukuliwa. Pamoja na kwamba tunaitwa wapinzani kwa sababu tunaambiwa kwamba sisi tunapinga kila kinacholetwa. Sio tunapinga kila kinacholetwa, tunaangalia ambacho kina athari. Tume ile mwanzo ilikuwa katika mashauri katika maamuzi. Rais wa Jamuhuri ya Muungano anaamua peke yake, lakini sasa hivi Rais wa Jamuhuri ya Muungano maamuzi yote atakayoyafanya atashauriana na Rais wa Zanzibar, tena kwa kubaliana. Mimi namshukuru sana Mhe. Kikwete kwa ustahamilivu wake.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ile sheria ilipokwenda Bungeni ilikuwa imeshapita, ni Rais wa mwanzo ambaye sheria imeshapita akakubali kuwaita wapinzani waliyoikataa akakaa nao Ikulu, akakubaliana nao. Akawambia basi mimi kwa mujibu wa katiba hii lazima niitie saini. Kwa hivyo nitaitia saini halafu nitairejesha halafu ukaifanyie marekebisho. Ni Rais muungwana kweli kweli, kakubali kakaa na wapinzani Ikulu, ikapelekwa tena Bungeni ikafanyiwa tena majadilio.

Mhe. Mwenyekiti, hata hili la sasa hivi wananchi kuweni huru mnavyotaka lakini suala la kusema mnautaka au hamuutaki hilo halipo. Tunakwambieni kabisa kama kweli mnajipenda na mnaipenda Zanzibar. Lakini toeni mapendekezo yetu ni aina gani ya Muungano mnaoutaka. Kwa sababu fursa hii tuliyoipata Katiba hii haijaruhusu, kwa kuwa hii sheria marekebisho ya Katiba yamekuja ndio nafasi pekee tulioipata.

Mhe. Mwenyekiti, ikiwa kama mwenzako anatoa maoni ya Serikali moja muheshimu, anayetoa maoni ya Serikali mbili, muheshimu, anayetoa maoni ya Serikali tatu, muheshimu na anayetaka Muungano wa mkataba muheshimu ndio Katiba hii inavyosema. Sasa leo ukijifanya wewe ndio mkereketwa mkubwa, wewe ndio unapenda zaidi Wazanzibari, ndio unaipenda zaidi Tanzania, unachotaka wewe ndio kiwe hicho hicho. Baadaye wananchi ndio watakaokwenda kuamua. Mimi naomba kwa kumalizia tusianike karafuu wakati wingi la Masika limeshatanda.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipura. Kama nilivyosema katika angalizo langu kama sijapata kauli ya Waziri ambaye anasimamia haki akashindwa kusimamia haki za Mahakimu wake wa Mahakama ya Mwanzo peke yangu nitapita kura sitounga mkono hoja hii. Ahsante Mwenyekiti.

Mhe. Hijja Hassan Hijja: Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, baada ya jana kumuachia Mhe. Mansoor, nilimuachia si kwa sababu ya utashi au woga. Nilijua kwamba ana maneno muhimu sana kwa ajili ya maisha ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi naomba nitangaze kabisa kwamba nitazuia mafungu mawili kwenye hotuba hii. Fungu la mwanzo ambalo nitazuia ni fungu la mipango na sera na fungu la utumishi na uendeshaji. Naomba nitangulize mwanzo nisije nikasahau nikaambiwa kwamba sikusema nasema kabisa mpaka pale Waziri atakaponitosheleza. Tena kama kuna mfano wa kuzuia nataka nioneshe leo mfano za kuzuia. Ili ionekana wale Wakuu wa Mikoa wanaomhisi Hamza basi hata CUF pia wanazuia CUF wenziwao.

Sisi hatumzuwii Waziri kwa maana ya kwamba CUF au CCM. Tunazuia wale ambao hawatutoshelezi maslahi yetu. Kwa hiyo leo nitamzuia Mhe. Abubakar Khamis Bakary ili Mhe. Tindwa kule Pemba aone kama kumbe Mhe. Hija anamvuia Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kwamba Wizara hii imepewa jukumu la kusimamia haki. Jana niliwambia wenzangu kwamba Wizara hii ukizungumza uwe na udhu kweli kwa sababu ina mashekhe, ina majaji, ina maulamaa, kwa hivyo uwe na udhu kweli kweli. Naomba kuwakumbusha Mashekhe kwamba hii Wizara inasimami haki kwa maana ya Mahakama za Kidunia, inasimamia haki kwa maana ya wamba zinachunga mpaka haki ya siku ya Kiyama, kwa maana ya ndoa, talaka, mirathi na mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza wanahitaji wao wenyewe kujitathmini je, kweli wanasimamia haki. Hilo naomba nisijibiwe wao wenyewe wajitathmini je, kweli wanasimamia haki? Jawabu lao watalipata naomba wajibu kwa yale maelekezo ambayo Mwenyezi Mungu ataridhika je, wanasimamia haki? Kama hawasimamii haki watajirekebisha na ndio binaadamu walivyo.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya mwanzo naomba nipate majibu ni upatikanaji wa fedha. Mwaka jana walituomba bilioni 4.6 fedha za uendeshaji, bilioni 2.2 ilikuwa ni mishahara na bilioni 2.4 ilikuwa ni kazi za kawaida. Lakini Mhe. Waziri anatwambia hadi kufikia Machi 2012, mishahara wamepatiwa bilioni 2.7 asilimia 123. Naomba Mhe. Waziri anambie kwa nini fedha za mishahara ziliongezeka kwa asilimia 123 badala ya asilimia 100 ya kipindi hichi cha robo tatu.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya pili Mhe. Waziri ametwambia kwamba wanaendelea ujenzi wa jengo la Ofisi lenye ghorofa kama sikosei 7 au 8. Naomba pia anisaidie fedha hizi zinatokana na chanzo gani. Je, fedha hii iliidhinishwa na Baraza la Wawakilishi? Naomba Mhe. Waziri akifika anielimishe.

Hoja ya tatu ambayo naomba nipatie ufafanuzi ni Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwamba Baraza la Wawakilishi baada ya kuja kutunga sheria, sheria ile hulazimika kupata baraka ya Raisi kwa maana ya kutiwa saini. Kumekuwa na wasi wasi kwamba zile Sheria ambayo tumezipitisha Baraza la Wawakilishi hapo kati kati hubadilika kwa mfano.

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni tulipitisha Sheria ya Baraza la Mitihani lakini, juzi Wizara ya Elimu walitwambia wao Sheria walioiyona ni Sheria ya Baraza ya Tathmini na Vipimo. Nikamwambia hiyo si sheria yetu labda sheria

nyengine, Baraza la Wawakilishi walipitisha Baraza la Mitihani sio Baraza la Vipimo na Tathmini. Kwa hivyo Mhe. Mwanasheria Mkuu naomba unisaidie kwamba hilo ilikuwa sahihi au kuna makoseo ambayo hapo kati kati yalifanyika.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya tano ni maslahi ya wafanyakazi, nimesema nitazuia fungu la utumishi kwa sababu hapa ndio hoja yangu. Naunga mkono ile hoja ya Mhe. Hamza kwamba sitomuelewa Mhe. Waziri kama hakunijibu maslahi ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo. Hadi asubuhi ya leo nafanya utafiti Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wanapata mshahara wao ni kiasi laki mbili na nusu mpaka laki tatu. Wakati Mahakimu wa Wilaya ni karibu milioni moja na zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri anijibu na hapa ndio nitazuia fungu kama sikupata majibu ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo kwa nini maslahi yao hayajaongezwa. Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wanahukumu kesi, msingi wa kesi hiyo ndiyo baadaye unaweza ukakata rufaa ukenda Mahakama ya Wilaya au Mkoa. Kitendo cha kutoa maslahi duni sana kwa Mahakimu hawa kwa kweli hakipendezi ni lazima Mhe. Hamza tuungane mkono kwamba fungu hili tulizuie ili kama kuzuiwa fedha ni haki na hawa Mahakimu wengine wakose haki. Huu ni utawala bora ni lazima kila mtu apewe haki yake kwa mujibu wa nguvu yake.

Mhe. Mwenyekiti, hoja nyengine ni suala la Maslahi ya DPP. Ofisi hii ni Ofisi moja ambayo ina fitna kubwa. Ili jaji apate kesi ya kuhukumu ni lazima afisi hii iandae mashtaka. Kwa hivyo unavyowapa maslahi madogo afisi hii unaifanya hiyo kesi yenyewe isifanyike. Nadhani ndio sababu kesi hizi ikawa hazisikilizwi kiasi hicho kwa sababu matayarisho yote ya kesi za Mahakamani ni lazima ofisi hii ndio waandae. Maslahi ya ofisi hii Mhe. Waziri nakuomba sana uyaongeze na kuzingatia na elimu zao. Inasemekana kwamba wapo mbali sana baina yao na Mahakimu, wako mbali sana baina yao na majaji. Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Waziri atumie busara zake, maslahi ya wafanyakazi wa DPP lazima yaongezwe.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya sita ambayo nataka niifafanue ni tatizo la vyeti vya kuzaliwa. Hii tuliisema zamani sana bado wananchi wetu Vijijini hawapati vyeti vya kuzaliwa. Hata pale Mahakama inapoamua kwamba hiki cheti apatiwe fulani. Hili pia Mhe. Waziri naomba utupe ufafanuzi pamoja na bidii yako unayoifanya ya kusimamia vyeti hivi lakini bado kuna tatizo la vyeti vya kuzaliwa. Wananchi wetu bado wanasumbuka na hasa vijijini bado wanapata matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, suala la mwisho ambalo nataka niseme ni suala la marekebisho ya Katiba. Hapa ndio ninazuia hoja yangu ya pili ya Fungu la Mipango na Sera. Mimi nataka niwambie Wazanzibari wenzangu wala wasipate tabu hakuna mtu wa kunizuia kutozungumza na Mhe. Hamza na Mtando, hakuna. Mimi naitwa Hija Hassan na yeye Hamza Hassan jina pekee linaonesha kwamba hawa watu ni damu. Kwa hiyo usihangangaike ukatia U-CUF wako U- CCM wako ukafikiri mimi nitazuilika kwa kuungana na Hamza Hassan. Naungana naye kwa sababu nimemuona ni mtu wa maana, ameamua kuwasaidia Wazanzibari. Kwa hiyo hata kwa uganga nitaungana na Hamza Hassan, nitaungana na Mhe. Makame Mshimba, nitaungana na Mhe. Mborouk Wadi Mussa (Mtando) na Mhe. Asha Bakari na Mhe. Salmin Awadh kwa sababu ni waungwana na ni wakweli na sio wasaliti.

Mhe. Mwenyekiti, humu wamo Wawakilishi hawasemi wanasubiri useme wakaseme, wala miye hatusalimiani. Kwangu mimi msaliti hana nafasi kwa hiyo nampenda Hamza Hassan na wengine kwa sababu ni wakweli na ni waungwana. Hata siku moja hatujakaa na Mhe. Hamza Hassan tukazungumzia CCM wala CUF kila mtu ana magwanda yake. Mimi kadi yangu safi na naipalilia na Hamza yake safi anaifagilia. Lakini kwenye suala la Uzanzibari kwa kuwa kuna maslahi yetu ni lazima tuungane. Wale viongozi wa Pemba kule wanaomshutumu Hamza Hassan wasihangaike bwana. Hamza kachaguliwa na watu zaidi ya 10,000. Wewe umeteuliwa wala hujaapishwa upo, ipo tu.

Mhe. Mwenyekiti, marekebisho ya Katiba lazima tuungane na hapa ndio nazuia fungu kwa nini Mhe. Mwenyekiti, baadhi ya majimbo vituo vya kutoa maoni ni vitatu mpaka vitano. Jimbo langu la Kiwani ni kituo kimoja kwa nini. Jimbo la Kiwani jiografia yake ni Visiwa, mtu wa Shamiani hafiki Muwambe mpaka avuke bahari, mtu wa Mtangani hafiki Kiwani mpaka avuke bahari. Wametuwekea kituo kimo Kiwani kwa madhumuni gani.

Mhe. Mwenyekiti, nitazuia fungu hili Mhe. Mwenyekiti la Mipango na Sera mpaka Waziri anambie vituo vingapi jimbo la Kiwani ameongeza. Haya ndio niliyotumwa, nimeambiwa nisipitishe na sipitishi. Mimi ajira yangu ni watu wa Kiwani na nawaheshimu sana, baada ya Mungu, Mtume, baba na Mama na watu wa Kiwani nawaheshimu. Sipitishi kifungu hichi hata Katibu Mkuu wa Chama anambie pitisha, sipitishi. Mpaka anambie ni lini ataongeza Vituo angalau kimoja ndani ya jimbo langu. Haiwezekani ikiwa hii ni Wizara ya Kutoa haki lakini watu mnawabana wasipate haki hatuwaelewi Mhe. Mwenyekiti.

Nasema kwamba Wazanzibari ni lazima tuungane kwenye kutoa maoni ya kweli kwa ajili ya kuitatua Zanzibar yetu. Tuwaache wale ambao

wanatupotosha. Mimi naungana na Mhe. Salmin kwamba lazima Wazanzibari tumtahadhari sana Jaji Warioba. Kwa sababu sheria imesema kwamba mambo ambayo hayapaswi kujadiliwa ni Muungano. Anakwambia wewe kama huutaki sema tu. Ni lazima tumtahadhari.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, kwa uoni wangu na hivyo ndivyo watu wa Kiwani nimewafundisha kwamba kila mtu wa Kiwani akenda aseme Zanzibar kwanza baadaye mkataba. Watu wa Kiwani msimamo wetu kwamba Serikali ya Mkataba, kila mtu akae kwake tuungane kwa Mkataba, ikiwa kuna haja. Na kama hamuamini nendeni mkaangalie maoni.

Kuna haja Wazazibari wenzangu wote kuwanasihi kwamba ni lazima tuungane katika jambo hili. Zanzibar tuko mbali sana, Zanzibar tumeliwa sana, ikiwa wasomi wamehangaika miaka 48 hakuna majibu. Lazima wananchi tuwe na majibu na majibu ni kutetea Zanzibar kwanza baadae twende kwenye Muungano wenye maslahi. Muungano wenye maslahi pekee kwa uoni wangu ni ule Muungano ambao tutakubaliana kwa mkataba ambao utasema muda gani na mambo gani. Leo unaweza Alkhamis ukaambiwa mambo 10, Ijumaa 16, hatwendi hivyo, lazima Wazanzibari wajue nini walichoungana na kwa muda gani.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme tu kwamba wale ambao wamemsikia Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba anasema kwamba majimbo ambayo kuna kituo kimoja watu wasijali watafanyiwa tena, lini watafanyiwa tena? Kwa hivyo hatuwezi kubahatisha khatma yake bila ya kupata usahihi wa Serikali. Mhe. Waziri ni lazima utwambie kwa nini majimbo yetu hayakupangiwa vituo vingi vya kutoa maoni. Na kwa nini ukawapa majeshi zaidi na askari kuliko kuwapa wananchi, ambao hata uoni wao wa kutoa maoni ni mdogo.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili namuomba sana afanye mawasiliano na Tume yake ili anambie Jimbo la Kiwani ameongeza vituo vingapi ili nimpitishie. Vyenginevyo leo hapa nitawaomba wenzangu wote waniunge mkono akose fungu la mshahara, kwa sababu hajawatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Kiwani. Mimi kati hilo sina masihara, namuheshimu sana Mhe. Abubakary kwamba ikiwa si yeye siwi mgombea nitahiyari nikose ugombea lakini hili nitalisimamia.

Mhe. Mwenyekiti, wala musijidanganye humu ndani ya Baraza kuna viongozi wawili wa chama kuna Mhe. Ismail Jussa Naibu Katibu Mkuu, Mhe. Gavu Katibu Mwenezi. Kama hawaamini kwamba Wazanzibari hawana haja ya Chama zaidi nchi ndio muhimu. Tunafanya kazi moja nataka nikwambie. Jumamosi CUF wanaweka Mkutano pale Kibanda Maiti, angalia idadi ya watu wakaokwenda. Jumapili CCM wanafanya Mkutano Kibandamaiti

uangalie idadi ya watu watakaokwenda. Jumatatu UAMSHO wanafanya Mkutano, mikutano yote miwili ya CUF na CCM itashindwa na Uwamsho mmoja. Kwa sababu sasa hivi wananchi haja yao ni Zanzibar, vyama wameviweka pembeni. Zanzibar mwanzo baadae ndio chama.

Msijidanganye viongozi wa siasa mkafikiria kwamba Wazanzibari yale mawazo ya 1964 mpaka 1975 muhimu Chama kushika hatamu muda huo umepita. Lazima Zanzibar mwanzo ndio baadaye Chama. Mimi nasema wazi kwamba Naibu Katibu Mkuu wangu yupo hapa mkono wa kushoto, lugha ya kunambia kwamba kawasahihishe watu wa Kiwani kuwe na Serikali tatu, siendi. Kwa sababu msimamo wa wananchi wangu baada ya kufanya mazungumzo ni Serikali Zanzibar yake Tanganyika yake baadae kuwe na mkataba wa kuandikiana. Kila mtu, mwanafunzi, mdogo wa darasa la kwanza anajua nini tumeungana.

Leo hii ukimuuliza Mwanasheria Mkuu tuambie Muungano wetu uko vipi atakwambia, aah miye, nasikia tu maana sijauwona mkataba. Sasa ikiwa Waziri wa Sheria humu ndani aliwahi kutwambia kwamba mkataba hayauwona. Kama hajauwona yeye Waziri wa Sheria aje auone mtu wa Mwambe. Lazima tuungane kwa mkataba, kila mtu ajue tumeungana nini, mwanafunzi wa Darasa la kwanza mpaka mwanafunzi wa Chuo Kikuu ajue tumeungana nini na huo ndio muungano.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuheshimu muda wako nasema mafungu mawili hayo Mhe. Waziri unijibu. Mipango na Sera kuhusu ratiba ya maoni na utumishi kuhusu Mahakimu wa Mwanzo ndio bajeti nipitishe, kwa sasa siungi mkono mpaka nipate majibu tena majibu yasiyokuwa ya ubabaishaji majibu hasa.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabla ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Allah (SW) aliyeniwezesha hapa kusimama na kunipa pumzi zake nikaweza kupumua. Huu si ujanja wangu wala si akili zangu wala si uwezo wangu hii ni neema yake Alla (SW) nasema Alhamdulillah.
Kwanza nampongeza Mhe. Abubakary Said Bakary, kwa *speech* yake nzuri ya hotuba ya Waziri wa Katiba na Sheria. Mimi mchango wangu utakuwa mdogo tu, katika Idara ya Mahakama ukurasa wa 11.

Kwanza nataka nilipongeze kwa dhati kabisa jeshi la Polisi kwa kuwa makini katika kufungua kesi, kesi ambazo zina muelekeo tofauti na zamani polisi walivyokuwa wakifungua kesi. Hapa nataka nimpongeze kabisa na hii ndio dunia inavyokwenda kwa wenzetu, wanafanya vitu kama hivi, hufanya utafiti

kwanza ndipo kesi ikafunguliwa baadaye. Kwa hilo nataka kukupongeza zaidi.

Baada ya hapo nije katika Idara ya Mahakama. Hivi sasa Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mahakama kuna kesi nyingi sana na zinachukua hata miaka mine mpaka mitano ni usumbufu uliyokuwa wa hali ya juu. Tuchukulie mfano mtu anakaa Chwaka ana kesi ya jinai anataka kuripoti Vuga, atakwenda nayo miaka 4 kesi ile haijesha, ile peke yake ni adhabu ya kwenda kutoka kule Chwaka akaja zake Vuga. Hatuwezi kuwalaumu mahakimu tu vile vile kuna vitendea kazi navyo mtihani. Tuiangalie mahkama ya Mwanakwerekwe, Ofisi moja inatumiwa na mahakimu watatu, kweli itapatikana haki pale. Tuchukulie kesi ya kubaka mtoto ana umri wa miaka 4, kesi yake itakuwa na miaka 6, nne jumlisha na sita ngapi jawabu utapata kumi, atakuwa na kumbukumbu kweli ya kuja kutoa ushahidi mahakamani pale. Kwa kweli hapa ni pahali pazito Mhe. Mwenyekiti, na hapa nitahitaji maelezo ya kina Mhe. Waziri utajipanga vipi hapa kuhusu mrundikano wa kesi zilizokuwa katika mahkama zetu.

Mhe. Jusa jana alichangia kuhusu mahkama ya kadhi na Mhe. Jussa akisema kitu anakuwa na uthibitisho habahatishi wala akakohoa, hii ndio sifa ya Mhe. Mwakilishi wa Mjimkongwe. Hivi juzi kulikuwa na kilio, kulikuwa kuna kesi imesikilizwa pale upande mmoja tu sijui kama mama au baba bila ya kuitwa muhusika na ukapata hukumu. Kitengo kile Mhe. Abubakar ninafikiri ukiangalie ile ni hukumu ya Mwenyezi Mungu, kuna watu wengine wanapoteza haki zao pale. Mimi ningelishauri angetafutwa mwanasheria aliyesoma au mwenye digrii ya kiislam akawekwa pale, huu ni ushauri wangu tu.

Nije katika mwezi mtukufu wa Ramadhani, Mheshimiwa tunakaribia katika wiki hii Mungu akitujaalia penye uhai tunaupokea mwezi wa Ramadhan.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe zungumza na kiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti mwezi huu wa Ramadhan hivi sasa umekuwa hauna hadhi, umekuwa hauna heshima, watu hawajali wanavyojiamulia ndio hivyo hivyo, mtu kula njiani imekuwa ni kawaida, suala la mikahawa kukuta iko wazi sasa hivi limekuwa jambo la kawaida. Hapa Mhe. Mwenyekiti nitahitaji maelezo mwezi huu unataka kuheshimiwa, tumeshuhudia Mhe. Mohammed Aboud mwaka jana alikuta watu wamevaa nguo ambazo mtu huwezi kuzitizama alipiga kelele na hatua zikafuata, sasa hapa sijui Mhe. Waziri atanieleza kitu gani. Nguo zinazovaliwa hivi sasa hazikidhi matakwa ya wananchi, na kuna sheria nyingi ninafikiri hazijaondoshwa mpaka hivi sasa wakati huo Mwenyekiti alikuwa Mhe. Marehemu Dourado hivi sasa ninafikiri ni Mhe. Mshibe Ali Bakari.

Kulikuwa na sheria za nywele zaidi ya nchi mbili unapata hukumu, sijui sheria ingalipo au tunaendelea vile vile. Nguo kubana sasa hivi sijui tuseme vipi, tukipita humo njiani na mwezi unakaribia Mheshimiwa. Hapo nitahitaji takwimu Mhe. Waziri watu waliokamatwa kwa mambo kama hayo najua sheria ipo haijafutwa, sisi tumekuwa hodari wa kupitisha sheria lakini utekelezaji wake umekuwa mdogo.

Tuje mahakama ya ardhi sasa hiki kitengo sijui kiko mahakama ya ardhi kwako, wewe Mhe. Waziri au Ardhi wenyewe wanashughulikia, pale bado pana matatizo na si madogo pamoja na kuongeza mahakimu, *judgement* zinachukua muda mrefu kupatikana pale na kubwa ninafikiri *rules* hawana ninafikiri wanafuata kama mahakama za mwanzo, *rules* hazifuatwi, hapa nitahitaji maelezo vile vile Mhe. Waziri napo ili tujipange. Vitendea kazi sasa hivi ninafikiri nchi kama Nairobi; Kenya, hata hapo ndugu zetu Dar es Salaam wana kitu kama hapa Baraza la Wawakilishi *hansard* mtu anazungumza maneno yanajirikodi, sijui hicho kitu kina gharama gani. Mtu atatoa ushahidi anajirikodi ni vitu vya kuangalia watu wanakwenda mbele sisi tunarudi nyuma.

Mhe. Hija, Mhe. Hamza walizungumza hapa kuhusu mahakimu wa mwanzo hiki kimekuwa ni kilio kikubwa kwa Waheshimiwa sana sana sana, kama haki itendeke kwa wote tusianze kubagua kwa mujibu wa katiba zetu kwa hawa wamekwenda kinyume kwa muda mrefu Mheshimiwa. Haya ndio yanayopelekea hata maamuzi wakati mwengine yasipatikane ya uhakika.

Kwa hayo Mhe. Mwenyekiti mpaka nitakapopata maelezo nitaunga mkono.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti ninawashukuru kwa kunipa nafasi hii baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha leo hii kuweza kukutana katika ukumbi huu, kwa nia ile ile ya kuwakilisha wananchi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti naomba nianze kwa kumpongeza Mhe. Rais, naomba nimpongeze Mhe. Rais kwa namna alivyoipanga Wizara hii ya Katiba na Sheria. Ukweli ukiangalia kuanzia Waziri mwenyewe na hadi wale wakuu, mahakama pamoja na vitengo vyengine vilivyomo katika Wizara hii inathibitisha kwamba Mhe. Rais kakusudia kikweli kweli kuimarisha Wizara hii. Tukianzia na Waziri mwenyewe Mhe. Abubakar, Katibu Mkuu pamoja na Naibu Katibu Mkuu walioteuliwa ni watu makini sana, Mhe. Jaji Mkuu wa Mahkama Kuu, Mkurugenzi wa Mashtaka, Mrajis Mkuu, Mufti na Kadhi Mkuu. Watendaji wote ni watu ambao ni wachapa kazi, lakini zaidi kuliko yote ni kwamba watendaji wote wana sifa ya uadilifu.

Kwa hivyo pongezi kwa Mhe. Rais na kwa uteuzi wake huo mimi ninaamini kwamba ndani ya kipindi hiki cha miaka 5, kwa kweli Wizara hii itapiga hatua kubwa sana kutokana na usimamizi wa watendaji hawa ambao wameteuliwa.

Sasa baada ya pongezi hizo naomba nianze kwanza kwenye suala zima la upatikanaji wa fedha ambayo inaonekana katika ukurasa wa tatu, na katika hii naomba nihoji namna ambavyo mishahara ya jumla ilivyoingizwa kwamba ilikusudiwa mishahara elfu mbili mia moja na thamanini na nne milioni, lakini hadi kufikia Machi tumeambiwa imeingia elfu mbili mia sita thamanini na nane milioni ndani ya kipindi cha robo tatu ya mwaka hawa wamepata asilimia 123, na hapo pana robo nzima kuanzia Aprili mpaka Juni. Sasa ninaomba Mhe. Waziri anieleze sababu ambazo zilipelekea malengo ya mishahara pamoja na mambo mengine ndani ya kipindi cha miezi 6. Kwa nini ikawa hivyo na hiki kipindi cha Aprili/Juni walilipa mishahara na stahiki nyengine kutoka fungu gani kwa sababu tayari fungu lao linaonekana limemaliza.

Lakini vile vile kazi za maendeleo washirika waliazimia kutuchangia elfu tano mia tatu ishirini na nane milioni, lakini hadi kufikia kipindi hicho zimeingia mia mbili hamsini na tano milioni sawa na asilimia 5 ya lengo. Kuna mapungufu asilimia 95, naomba Mhe. Waziri atakapokuja atueleze ni sababu zipi zilizopelekea wahisani kutuacha mkono katika kiwango hicho cha ajabu. Lakini la mwisho katika hili naomba tu Mhe. Waziri atakapokuja anieleze kwa nini hakufikia lengo la ukusanyaji, kwa sababu ametueleza kwamba hadi Machi kafikia asilimia 67, sidhani kama kati ya kipindi cha robo tatu ataweza kufikia asilimia hii. Kwa hivyo naomba atueleze kwa nini katika kipindi hicho hakufikia katika lile lengo ambalo tulilikusudia.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti sasa naomba niende katika kile alichokigusia Mhe. Hija kuelezea namna ya utungaji wa sheria na wasiwasi wetu tuliouanza kuupata Waheshimiwa Wawakilishi katika Baraza. Tunafahamu kwamba mfumo wa utungaji wa sheria unakuwa na mchakato mkubwa. Lakini mchakato wa mwisho kabisa ni rasimu ya sheria kuletwa katika Baraza hili, rasimu ya sheria inapoletwa katika Baraza hili na Baraza kupitisha sasa kama sheria, sheria hurudi kwa Rais kwa ajili ya kupata saini.

Sasa tulichokibaini na ambacho kinaanza kutupa wasiwasi tumeanza kupata wasiwasi kwamba baadhi ya sheria zikishatoka katika Baraza hili hufanyiwa uchakachuaji. Na hapa tumekusanya kama sheria mbili tatu hivi, tunazifanyia utafiti ili tupate rasimu tuziangalie na vile Rais alivyozitia saini tunaendelea na utafiti huo. Lakini yote kwa yote tunapendekeza sasa kwa serikali, mara

tutakapopitisha sheria, na kufika kwa Mhe. Rais kuweka saini tunapendekeza kwamba sheria hiyo sasa irudi kwa Wawakilishi, ili angalau kila Mwakilishi apate *copy* yake moja na nakumbuka kwamba tumekubaliana, kwa sababu katiba yetu imeruhusu kiingereza na Kiswahili, kwa hivyo tumekubaliana sheria atakayopelekewa Mhe. Rais ziwe zote mbili kiingereza na Kiswahili zote aweke saini. Kwa hivyo tunazidi kusisitiza kwamba Rais apelekewe sheria zote mbili aweke saini, lakini vile vile kwa sababu sisi ni wadau wakubwa watungaji wa sheria Rais atakapoweka saini sio tu Mhe. Spika, kututangazia kwamba Rais ameweka saini. Bali iwe sasa kila Mwakilishi agaiwe *copy* yake moja kwa ajili ya kumbukumbu.

Niondoke hapo nami niungane na wenzangu wote wanaotetea maslahi kwa mahakimu wetu wa mahkama za mwanzo, niunge mkono kwa nguvu kubwa sana, kuboreshwa kwa maslahi katika Ofisi ya DPP na Idara nyengine. Mahkama hatusemi kwa sababu Mahkama tayari tushaliweka katika fungu lake kwamba wao wastahiki kwa namna yoyote maslahi yao yaboreshwe zaidi, kwa sababu ni muhimili kama vile ilivyo muhimili wa Baraza la Wawakilishi pamoja na Serikali.

Mhe. Mwenyekiti sisi Wawakilishi kwa kweli haturidhiki na suala zima la upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa. Katika karne ya sasa katika haki ya asili, haki ya mwanzo kabisa ambayo mtu hulazimika kuipata mara tu baada ya kuzaliwa ni chetu cha kuzaliwa. Lakini tunakumbuka na tunafahamu kwamba kwa muda mrefu sana kunakuwa na usumbufu mkubwa sana wa vyeti kupatikana kwa watoto wetu tunaowazaa. Sasa utaratibu huu unaoendelea bado Mhe. Waziri hatujaridhika nao, tunaomba ufanye kazi zaidi na zaidi, ili urahisishe upatikanaji wake pamoja na gharama. Suala la mtu kutoka kijijini akavuka akenda Mambo msige, suala la mtu kutoka kijijini akavuka akenda kwenye Makao Makuu ya Wilaya asijue inakuwaje. Lakini ninachosisitiza hapa Mhe. Waziri urahisishe upatikanaji wa vyeti kwa njia rahisi na njia ambazo hazina usumbufu. Kwa hivyo ni matumaini yangu Mhe. Waziri hilo utalipa mkazo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba niingie suala la marekebisho ya katiba, na katika suala la marekebisho ya katiba naomba nifanye nukuu, ukurasa wa 55 ambapo umesema kwamba kwa maana hiyo mtu anaweza akipenda kusema anataka nini kirekebishwe katika muungano huu. Jambo muhimu ni kuhakikisha kuwa maoni yake ni kwa maslahi ya Zanzibar. Hii ni hotuba ya Mhe. Waziri na hii ni hotuba ya Serikali. Kwa hivyo mimi ninachukulia kwamba huu ndio msimamo wa Serikali sasa, kwamba jambo muhimu ni kuhakikisha kuwa maoni yake ni kwa maslahi ya Zanzibar na wazanzibari, na hakuishia hapo alisema kwamba kimsingi lengo letu ni

kuifanya Zanzibar kuwa na haki na uhuru wake kamili ndani ya muungano wetu.

Mhe. Mwenyekiti kwa kweli maneno haya ni makubwa mno. Na mimi naomba niitumie fursa hii kuipongeza serikali kwa kuweka msimamo huu bayana, sasa wale wanaopita pita wakisema vyenginevyo dhidi ya hii kwa kweli ni bahati mbaya sana. Sasa huo ndio msimamo wa serikali. Kwa kuwa huo ndio msimamo wa Serikali sasa hivi katika visiwa vyetu au katika nchi yetu, kwa kweli kuna kitu kinachoitwa ukusanyaji wa maoni ya wananchi. Maoni maana yake Mhe. Mwenyekiti ni uelewa, huwezi kutoa maoni kama huna uelewa. Na huwezi kuwa na uelewa kama hukuwa na elimu. Mhe. Mwenyekiti mimi ninasikitishwa sana, sana, sana na serikali kutoandaa utaratibu mzuri wa kuwapa elimu wananchi. Jambo hili ni jambo zito sana hakuna jambo jengine zito, isipokuwa ni suala hili la kuangalia hatma za nchi zetu. Hatuwezi kuzungumzia uchumi, hatuwezi kuzungumzia mambo ya kijamii, hatuwezi kuzungumzia siasa, kitu cha kwanza ni kuwepo kwa nchi yenyewe.

Suala la kuwepo kwa nchi ni suala la msingi, kama hatuna nchi hayo yote hayana maana. Leo tumepata zoezi hili muhimu sana la kukusanya, ili wananchi wende wakatoe maoni yao, serikali haikuchukua juhudi ya kuelimisha wananchi. Sasa ikiwa serikali haikuchukua juhudi ya kuwaelimisha wananchi tunategemea leo wananchi wakazungumze nini mbele ya Tume. Jana kuna kijana wangu mmoja makini sana kasoma sana hii elimu ya kidunia alinipigia simu hapa hapa Barazani kwamba Mhe. Omar hebu jaribu kesho tarehe 17/07 Tume inakuja katika Jimbo letu la Chake Chake, hebu angalia katiba uangalie mapungufu yake. Sasa nilikuwa nikijiuliza ikiwa kijana huyu kamaliza takriban elimu kubwa, *Dar tech* sijui wapi hajui nini anakwenda kuzungumza leo hii mfikirie yule mwananchi aliyekuwa hajui '*a'* na '*b'* atakwenda kufanya nini.

Na mimi nawambieni, kama laitani si jumuia hii ya Uamsho kufanya harakati walizozifanya, nina hakika kwamba leo hii mpaka leo wazanzibari wangekuwa hawajui hata kama kuna hii Tume. Walaumiwe kiasi cha kulaumiwa lakini mimi kwa hili ninawapongeza sana watu wa Uamsho wametuamsha, na ingelikuwa si wao ninakwambieni tena, ingekuwa si muamsho mpaka leo Tume ingekanyaga katika nchi hii wazanzibari hatujui chochote kinachoendelea. Serikali kwa kweli hamkutimiza wajibu, leo tunawachukua wananchi kama mbuzi wa sadaka mliowapeleka machinjioni hawajui wanakwenda kufanya nini. Sasa matokeo yake sijui mara kuna wengine wanagawa bahasha na elfu kumi, na kuwaandikia hiyo sio *fair* kwa kweli sio *fair* kabisa kabisa. Wananchi kwa kweli kwa hili Wawakilishi tunawalaumu sana serikali kwamba haikutimiza jambo la msingi katika suala

hili ambalo linahusika. Sasa Mheshimiwa katika hilo mimi nasema kwamba tuna kila wajibu wa kuhakikisha kwamba elimu ndio ya msingi kulikoni kitu chengine chochote. Na katika hili tuna kila sababu sasa kutanabahi na kujua tunafanya nini.

Mhe. Mwenyekiti viongozi tuliopo Zanzibar tumegawika katika makundi mawili, kundi la kwanza ni kundi la viongozi ambao wana uchungu na nchi yao, na wana uchungu kwa sababu pamoja na kwamba, Mwenyezi Mungu katuumba kwa lengo la kumuabudu yeye tu, lakini katika hilo basi katuleta wanaadamu katika mataifa pamoja na makabila ili tupate kujuana kwa lengo hilo, Mwenyezi Mungu hakutuleta katika vyama katwambia nyie nawaombeni nendeni kwenye CUF, nyie nendeni kwenye CCM hakufanya hivyo, katuleta katika mataifa na Mwenyezi Mungu kawaumba watu wa Zanzibar na kaitengeneza ardhi yao ya Zanzibar. Na kwa sifa na hulka zetu katutenganisha pamoja na watu, sijui kwa sababu gani mwenyewe anajua hatima yake kwamba hatupendi ugomvi, hatupendi shari, hatupendi tabu ni watu wapole na wakarimu.

Kwa hivyo hiyo ndio sifa ya kwanza tuliyonayo, viongozi kuna watu ambao wanatetea maslahi wapo, lakini vile vile katika hili hili kundi la kwanza kuna watu ambao kwa kweli wana uchungu sana na wanaangalia misingi ya Afro Shirazi Party, ambayo misingi ya Afro Shirazi Party imetueleza kutakuwa na utu, kutakuwa na heshima na kutakuwa na usawa kwa watu wote. Hii ndio misingi ya Afro, hawa wana Afro walioanzisha chama hii ndio misingi yao kutetea utu, kutetea heshima, kutetea usawa na kutetea na haki kwa wananchi hiyo ndio misingi. Sasa leo wanaozungumza hivyo ni kwa sababu ya misingi hiyo ya Chama Afro Shirazi Party, ambaye huyo ndie mlezi wetu, huyo ndio baba yetu tuliyemuaga pale mwaka 1977 ndio misingi yake hiyo.

Kwa hivyo kinachofanyika leo ni kwa watu kuu-*revise* hiyo misingi ya Afro Shirazi Party. Lakini kundi hilo hilo linaongozwa na ile dhamira ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964. Ambapo lengo kubwa ilikuwa ni kuondosha dhiki na dhulma. Kwa hivyo ukichanganya mambo yote matatu hayo ndio utaona kundi hilo sasa la kina Mansour, la kina Raza, la kina Omar Shehe, Hamza, Jussa wao wanoitwa Muamsho tunasimamia misingi hiyo leo, kwamba hii ndiyo nchi yetu na hatuna pengine pa kwenda, tulizaliwa na tutakufa hapa.

Lakini misingi ya pili ni ile ya vyama vyetu, hichi chama chetu kilichotulea kikatuzaa, Afro Shirazi Party. Lakini msingi wa tatu ni dhima na dhamira ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964, lakini kuna kundi la pili Mhe. Mwenyekiti, kwamba wao bado wanaendelea katika kuishi katika misingi ile ile ya kuwagawa watu miongoni mwetu katika vyama vyetu bado tuna watu

wanaota ndoto zile za kutugawa, ili wao wapate njia rahisi watutawale. Lakini katika kundi hilo vile vile kuna watu wana njaa za nafsi, na hakuna njaa mbaya kama njaa ya nafsi. Hawa ni mithili ya bendera wao hufuata upepo unavyokwenda, hufuata jua linavyokwenda, likitoka jua hutoka na jua, likizama jua huzama nalo, wakeshapewa cheo hawa ndio basi.

Sasa katika hilo kitu cha msingi kabisa Mhe. Mwenyekiti, tunapaswa wazanzibari sote wa makabila tofauti, wa rangi tofauti, wa dini tofauti tutanabahi katika hili, hakuna jambo jengine isipokuwa hili. Hakuna zaidi kulikoni nchi yetu, wala suala hili halipaswi kabisa kabisa kulitia katika masuala ya vyama. Vyama hivi ni vitu hivi vya mpito ukiangalia historia ya vyama katika nchi yetu, vyama historia yake havizidi miaka 57. Vyama vyetu Mhe. Mwenyekiti havizidi miaka 55, historia ya vyama hapa ni kuanzia miaka ya mwisho wa 1950 mpaka leo 2012. Lakini Zanzibar yetu ilikuwepo karne na karne, na karne tangu kuumbwa kwake.

Ilikuwa Afro Shirazi hatunayo, vikaja vyama vyengine vya Hizbu, nani nani hatunavyo, kesho na keshokutwa hutosikia tena haki sawa kwa wote, wala hutosikia kidumu chama cha mapinduzi, vitakwenda tu hivi ni vitu vya mpito. Na watu hawa wala wasiwasumbueni, utawajua kwa matendo yao na utawajua kwa mienendo yao tunao. Wakati sasa umefika tusimameni wazanzibari kuitetea nchi yetu. Tunahitaji tuwe na Muungano, hakuna mpumbavu aliyekuwa hahitaji kuwa na muungano, sote tunahitaji kuwa na muungano. Tuwe na Muungano ambao utatufanya tupumue katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Ahsante.

Mhe. Ali Mzee Ali: Mhe. Mwenyekiti na mimi naona bora nichangie ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii, nimesikiliza mjadala huu tangu jana, wiki iliyopita mambo ya ardhi, mambo mengine, nimeridhika na Wajumbe wa Baraza hili la Wawakilishi la awamu hii ya saba kwa namna wanavyochangia, namna wanavyokosoa hivi ndivyo inavyotakiwa. Hii serikali ya sasa hivi ni serikali ya Mapinduzi, ni ile ile tangu 1964 mpaka leo, lakini mfumo wake ni mfumo wa Umoja wa Kitaifa. Lakini Serikali ya Mapinduzi, juhudi nyingi zimechukuliwa mpaka tumefika hapa.

Mhe. Hamza amezungumza juu ya kamati yetu. Sisi kweli kamati yetu imetumia pesa nyingi sana, lakini Mhe. Hamza usiwe na wasiwasi lete hoja. Mhe. Abubakar alikuwemo ndani ya safari, Mhe. Ali Abdalla alikuwemo ndani ya safari, Mhe. Mazrui alikuwemo ndani ya safari, Mhe. Haji Omar alikuwepo, Mhe. Ali Mzee alikuwepo, Mhe. Zakia hayupo waliobakia wote watano tumo ndani ya Baraza. Kama tumetumia vibaya fedha tukatwe, mimi nitatoa zangu *about* 15,000 *dollars* na hawa wakatwe, Zakia maskini hana

kazi tutamsamehe. Tulikwenda kujifunza, na pesa za wananchi zilitumika tena kwa taarifa yako ninamshukuru sana Balozi Seif Ali Iddi kila akiniona ananambia Mhe. Ali Mzee niandikie barua ili nikusaidie, lete *form* ya barua usaidiwe jambo hili, mimi nikamwambia hapana kwa sababu ushauri niliopata fedha zitatoka ndani ya SMZ.

Balozi nisamehe sana leo nitakupa ile siri sijakuandikia kwa sababu tuliamua fedha itoke kwenye SMZ, na kweli tulikwenda Uingereza fedha tulizotumia zetu, Ujerumani zetu, ukikutana na Mhe. Hamza atakwambia tulishuka Ujerumani Katibu Mkuu aliagiza akamwambia Omar King atume pesa Ujerumani, tulipofika Ujerumani pesa zimeisha. Mimi nimemkopesha 10,000 *dollars* nimelipwa lakini ilikuwa pesa hakuna.

Sasa Mheshimiwa mimi nitazungumza mambo matatu. Kwanza nitazungumza Ofisi ya Mufti, Ofisi ya Mufti ni Ofisi mpya sio kongwe. Ndugu Salmin Amour alianzisha hii mimi nilipoingia Barazani mwaka 2001 nikakuta kuna mgogoro mkubwa sana baina ya Mhe. Hafidh Ali na Mhe. Abdalla Mwinyi kuhusu msikiti wa Rahaleo, ugomvi ndani ya Baraza, mimi nikasema Mufti hana meno. Hafidh anataka ende akafunge Rahaleo ende Kikwajuni akamate Hafidh Ali, mimi nikasema hana meno Waziri alikuwa Dr. Shein, akaahidi hotuba ya Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais Katiba Dr. Ali Mohammed Shein 2001.

Dr. Shein akaahidi akasema tutaandaa mswada wa sheria itakayoipa mamlaka Idara ya Mufti kuwepo kwa mujibu wa sheria, kwa sababu ilikuwa mabavu mabavu tu. Dr. Shein akasema hapana, ninampongeza sana Dr. Shein alipokuwa Waziri wa Katiba na Utawala Bora, Dr. Shein ni mkweli ni muungwana ametimiza mwaka 2002 mswada ule ukaja ukapitishwa, lakini Mheshimiwa ukazuka mzozo mkubwa sana tuko Pemba. Hawa hawa wanaoitwa Muamsho wakaanza kuleta makaratasi wakati huo Dr. Shein sio Waziri, Waziri Mwakanjuki. Vipi mkristo, vipi kafiri, balaa likawa tuko Pemba pale *Rest House* ya Shirika la Bandari, muadhini anaadhini *qad-qaamati salaa* serikali mbovu lakini juhudi zikafanywa. Sasa ninasoma hotuba ya marehemu brigedia Adam Mwakanjuki 2004/2005 anasema hivi:

“Mhe. Spika, Wizara yangu yaani imeshirikiana vizuri na jumuia za kiislamu kama vile Muamsho, na pamekuwa na maendeleo mazuri baada ya pande hizi mbili kukutana’. Muamsho si ya leo, Wizara yake marehemu brigedia Adam Mwakanjuki, nimeona nitoe historia tu watu wengine wanadhani Muamsho imekuja jana au juzi, walianza zamani mambo haya, hiyo kwa taarifa ya historia.

Sasa Ofisi ya Mufti, Ofisi ya Kadhi wenzetu Bara wanahangaika na Kadhi, Kadhi Zanzibar tuna Kadhi tangu *Said bin Sultan* 1832, mpaka leo Zanzibar inaongozwa na Makadhi. Na Makadhi ni mahakama na makadhi wanafanya kazi ya uadilifu, sio zile mahakama za kapika tende aa hii mahakama ya sheria za kiislam na Mwenyezi Mungu, lakini kama alivyosema Mhe. Hamza tunawaheshimu hawa jamaa, ndugu zetu wazee wetu, na hatupendi kuyazungumza humu ndani. Mhe. Abuu Mahakama ya Kadhi itazame tuone hatutaki kukashifu hapa, ina uchafu, ina ubaya haitekelezi uislam, talaka zinatoka kama njugu, maamuzi kasema leo Salmin Awadh, maamuzi yanatoka ovyo ovyo itazame Mhe. Abuu una jukumu. Na wananisikia wenyewe juu nini wanataka mimi nina taarifa, Mhe. Hamza ana taarifa, Mhe. Jussa ana taarifa wote Mhe. Salmin Awadh. Mhe. Abuu usiitetee wala wewe si shekhe.

Na Mhe. Abuu ninakumbuka kuhusu kupeleka Jaji Pemba ukasema utajitolea kutoa nyumba yako wewe akae Jaji. Marehemu Mwakanjuki ulimbana, ulimbana mwisho marehemu Mwakanjuki akaapa akasema Mhe. Abuu *astaghfiru llahi laadhim* naapa nitatekeleza, sasa nikamwambia Mhe. Marehemu Mwakanjuki unaapa unasema uongo, unastaghfiru ndiko tulikotoka. Hilo Mhe. Abuu limemalizika.

Sasa tuje kwenye historia, unajua jana mimi nilikuwa usiku naumwa umwa nikasikia jana mambo mengi umezungumza. Historia ya nchi yetu Zanzibar ni kubwa sana, Zanzibar ni nchi ambayo ina historia ndefu sana, lakini kwa siasa Zanzibar ni nchi ya kwanza katika Kenya, Uganda, Tanganyika, Rhodesia, Nyasaland, Swaziland, kote huko ni nchi ya kwanza Zanzibar kuwa na uchaguzi wa vyama vingi *multi party*. Sisi tulianza uchaguzi 1957, Tanganyika 1958. Sisi tulikuwa na uchaguzi *one man one vote*, Tanganyika walipewa kura 3 kura ya mzungu, kura ya Muafrika na kura ya mu-Asia, hapa kura mtu kura. Kwa hivyo sisi ni wanasiasa wazuri sana, lakini tulianza siasa na vuguvugu.

Nchi yetu ya Zanzibar hii imetawaliwa sana Wareno, Warabu, walitugawa na ndio maana leo unakuta kuna Chama cha *Afro Shirazi Party* na chama cha *National Party*, hivi vyama viwili Hizbu na Hizbu maana yake ni chama lakini kinaitwa *Zanzibar National Party* na *Afro Shirazi Party*. *TANU* ilizaliwa na TAA *Tanganyika African Union* wakaweka 'N' ikawa *TANU*, Kenya ilikuwa *KAU, Kenya African Union* wakaweka 'N' ikawa *KANU* Zanzibar haijawezekana Africa Association kuweka alama au Shirazi kila mtu ana nasaba yake ndio ikaundwa *Afro Shirazi Party*, yaani Jumuiya ya Waafrika na Jumuiya ya Washirazi. Hii historia *documented* sio porojo na humu ndani sasa hivi imekuwa porojo hasa kwa mtu mzima kama mimi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi hapa ninayo *Manifest* ya *ASP* lakini nitaisoma baadae. *Manifest* ile inazungumza mambo mengi, lakini la msingi Mhe. Mwenyekiti, tukaanza siasa uchaguzi wa kwanza, wa pili, wa tatu na wa nne, lakini uchaguzi wa kwanza mwaka 1957 vyama viwili ASP, ZNP na *independent* akaingia tukenda hivyo hivyo; uchaguzi wa pili Juni tukapigana; uchaguzi wa tatu mwaka 1963 tukenda Lancaster Uingereza kudai uhuru. Kule Uingereza kuna katiba yake tukapewa Mzee Karume tarehe 5/04/1958 Rahaleo alisema hivi, "Tukipata nchi yetu, nchi itakuwa Jamhuri". Siku ya pili yake akataka kushtakiwa akaambiwa kwa sababu nchi ilikuwa na Mfalme, nchi akiwanayo Mfalme huwezi kuwa na Jamhuri, Mzee Karume akasema neno 'Jamhuri' ni neno la Kiarabu mimi silijui akaomba radhi sasa, maulana, mfalme, niliwahi kuisoma barua awamu ile, akaomba radhi akasamehewa lakini wakataka ile barua itoke ndani ya Gazeti la Uongozi na *African Page* naweza nikakuleteeni kesho mkitaka barua hiyo.

Tarehe 12 January, Mapinduzi tarehe 13 anatangaza Jamhuri *People Republic of Zanzibar* Sultan, Muingereza na Vibaraka wake Mhe. Ali Juma Shamuhuna alikuwa anapenda vibaraka wake Serikali ikiongozwa na Sheikh Mohammed Shamte kama Waziri Mkuu, Sheikh Abadhari Juma, Salum Kombo Bawaziri, Ali Muhsin, Ibun Saleh ninayo picha yao hapa, wakatulia wakaondoka ikazaliwa *Peoples Republic of Zanzibar*, Jamhuri ya Watu wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Jamhuri ya Watu wa Zanzibar ndio Zanzibar ikazaliwa. Sasa Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria katika hotuba yake anasema humu tuipate Zanzibar na haki zetu. Mhe. Mwenyekiti, naomba unipe muda na wale wengine, hatuwezi kuzungumza mambo ya marekebisho ya Katiba, mambo ya Muungano kabla hatujajua historia ya Zanzibar. Serikali imepinduliwa ya *ZNP, ZPP*, lakini nchi ilibaki lazima tujue tofauti baina ya nchi na Serikali kinachopinduliwa ni Serikali nchi imebaki kwa hivyo, Zanzibar ilibaki kama *state*. Sasa baada ya Mapinduzi wale ambao wameunda Baraza la Mapinduzi nitawataja kwa madhumuni ya kwenda katika historia na kwenda mbele ili tujue leo baada ya miaka 48 mambo yakoje. Hawa wamesaini Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi, hii inaitwa *legislative power law* 1964 Mwanasheria yuko pale siisomi nilichukua majina yao.

President Abeid Amani Karume kafa, Abdalla Kassim Hanga kafa, Abrahman Babu kafa, Hasnuu Makame kafa, Aboud Jumbe yuhai, Saleh Sadala kafa, Idrissa Abdulwakil kafa, Othuman Sharif kafa, Twala kafa, Hassan Nassor Moyo yuhai, Okelo kafa, Kisasi kafa, Yussuf Himid kafa, Seif Bakari kafa, Ramadhan Haji yuhai, Said Natepe kafa, Pili Khamis kafa, Khamis Hemed kafa, Hamid Ameir yuhai, Said Idd Bavuai kafa, Said Washoto kafa, Abdalla Mfaranyaki kafa, Hafidh Suleiman kafa, Khamis Daruweshi kafa, Khamis Abdalla Ameir yuhai, Mfaume kafa, Muhsin bin Ali kafa, Daud Mahmoud

kafa wamebakia watano tu, 31 wamebakia watano miaka 48; kabaki Hassan Nassor Moyo, Aboud Jumbe, Hamid Ameir, Ramadhan Haji na Khamis Abdalla Ameir.

Sasa hawa waliokufa tunasema wameshatangulia mbele ya haki na ile nyimbo yetu tunaimba kwamba tunawakumbuka, sasa hawa nafasi zao zimechukuliwa na nyinyi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, nyinyi ndio warithi, ndio watetezi wa nchi hii mkiongozwa na Balozi Seif Idd, hao washakufa hawasemi tena hawa, hawatoi maoni yao, maoni yanatolewa na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi viongozi wa nchi hii sisi ndio wenye dhamana sisi ndio wenyewe, tukiwangojea hawa ah, haya. Moyo unajitahidi zaidi lakini sisi Zanzibar ndio zaidi.

Niliona nitoe historia hii ili watu wafahamu tulikotoka, lakini si hayo tu sisi tulikuwa na nchi kamili Mhe, Mwenyekiti, tena nitakwambia sheria inasemaje,

Sheria Nam. 4 inasema,

> "There shall be a President of Zanzibar who shall be the head of state and commander in chief of the armed forces".

Tumesamehe tukakaa baada ya miezi mitatu tukaungana. Kwa nini tukaungana, siku moja Dr. Mwinyihaji nilimsikia anauliza kwa nini tuliungana? Sijaiona ile *manifesto*, *manifesto* ya *ASP* iko hapa inasema, Umoja wa Afrika tukaungana na lengo hilo Umoja wa Afrika si mengine tukaungana tukazaa Jamhuri ya Muungano, lakini tulipoungana kila nchi ilikuwa ina kiti chake na uhuru wake. Ninayo barua hapa Tanganyika 1961 inasema, "Having received recomondition …….of UN Tanganyika is admitted United Nation", yaani Tanganyika sasa inaruhusiwa kuingia UN.

Ninayo barua hapa nilisema mwanzo nchi inabaki serikali inapinduliwa, ninayo barua hapa inasema, In connection with application of Zanzibar for membership of United Nation, I have the honor on behaf of the Government of Zanzibar in my capacity as a Prime Minister to declare the Zanzibar accept the obligation contained in the chatter of United Nation and solely under taking at …..I have the honor your exlency humble of regent servant Mohammed Shamte Hamad".

Tulipompindua hatujaomba tena kwa sababu kiti cha nchi sasa ….. Muungano wetu ni wa muda mrefu, kelele nyingi, tume ninayo hapa ripoti muhtasari mkuu wa taarifa ya Kamati ya Baraza la Mapinduzi kujenga hoja juu ya masuala ya Muungano wa Tanzania. Hii ripoti ya Mhe. Amina Salum Ali,

lakini hizi ripoti ziko nyingi, iko ripoti ya Mhe. Amina Salum Ali, ripoti ya Ali Juma Shamuhuna, ripoti ya Balozi Moh'd Ramia, sasa Mhe. Waziri kama Serikali ya Mapinduzi imetoa ripoti nyingi kero za Muungano sasa hizi ripoti zichukuweni mzilete hapa tuzifanyie kazi wala wewe usiingie. Kwa sababu bado Baraza la Mapinduzi, Serikali hii ya Mapinduzi na Baraza la Mapinduzi limefanya ripoti zaidi ya nane kuhusu kero za Muungano, sasa leo mnatwambia.

Mimi nafikiri Wizara ya Katiba na Sheria haiingii lakini sidhani serikali, serikali haiwezekani iseme haiingii, haiingii vipi sasa, sisi tumeungana na Serikali ya Mapinduzi imekuwa na hoja nyingi juu ya Muungano huu, Muungano tunautaka kwa sababu asubuhi tunaapa hapa, lakini kuna kero na wala sio siri. Sasa zile kero zote ambazo zipo tunaweza kwendazetu tukasem asisi tuna kero, moja tunataka Rais wa Zanzibar awe Makamu wa Kwanza wa Rais hatutaki mpango huu wa *running mate*, hii ni kero yetu. Tunataka Zanzibar tuwe na nafasi ya kupata mgombea *independent*, kuna mambo mengi yamesemwa kwenye hii ripoti ya Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, inasema mambo ambayo yanapendekezwa kuondolewa katika orodha ya mambo ya Muungano Kodi ya Mapato, Mikopo, Misaada, Uhusiano wa Kitaifa, haya yote ni ripoti ya Baraza la Mapinduzi tupeni haya ndio tukawaambie hao Tume ya Jaji Warioba, wananchi wetu tuwaambie nendeni mkasema haya suala la mnautaka au hamuutaki halimo, bado muda wake haujafika hakuna suala hilo. Mhe. Hamza Hassan Juma amesema Mhe. Warioba ametuchezea, ametuchezea kweli, kuna makala imeandikwa kampa nani madaraka hayo, yeye katuachia *reference*.

Mimi Mhe. Mwenyekiti nilikuwa mjumbe Tume ya Rais ya kukusanya maoni kuhusu Afrika Mashariki peke yangu humu ndani Mjumbe wa Baraza, tumepewa tumepewa tu *reference*, huwezi kufanya kazi kinyume na ile. Jaji Kisanga kafanya tume akachukua maoni ya kuuliza serikali mbili au tatu, chombo chake kilitupiliwa mbali akaambiwa nani amekutuma wewe? Wewe ulitumwa kwa haya tu. Kwa hivyo hii kasema tu Warioba mbona hajasema Dar es Salaam tena kwenye hotuba yake hamna kasema kwenye masuala. Suala la muhimu mimi nataka nimpongeze sana, sana, Rais Jakaya Mrisho Kikwete.

Kwa sababu hii Serikali ya Umoja wa Kitaifa yeye ndiye wazo lake ndani ya Bunge na mimi watu ambao ninawaheshimu ni waasisi wa jambo hili sio sisi kina Ali Mzee ni kwa upande wa *CUF* Seif Sharif Hamad, Abubakar Khamis Bakary, Juma Duni Haji, Ismail Jussa Ladhu. Kwa upande wa CCM ni Kingunge Ngombale, Ali Ameir, Bi Zainab Omar Mohamed, Vuai Ali Vuai huyu Naibu Katibu. Hawa ndio waasisi wamekaa miezi 18 Bagamoyo

wakatuletea hoja tuunde Serikali Shirikishi sio Umoja wa Kitaifa, tukasema hapana tukazozana zozana tukasema hili jambo jamani lende kwa wananchi. Mhe. Abubakar akaleta hoja Barazani hapa kwamba Baraza la Wawakilishi liamue tukakataa, kila aliyesimama anasema twende kwenye mpango wa Butiama ndio ikaundwa kamati ile. Kwa hivyo, jambo hili watu wameshirikishwa.

Rais Kikwete kaja hapa kasema pale Maisara lisilo budi hutendwa, anawaomba wanawachama wake wa CCM wapige kura ya ndio wala sio siri, lakini matokeo yake kutoa agizo kutekeleza tofauti, kwa sababu nchi yetu imejengeka kwenye demokrasi mtu ana uhuru wake, kura za maoni Jimbo la Dole asilimia 51 walisema hapana, Jimbo la Chaani asilimia 63 walisema hapana, Jimbo la Donge asilimia 71 walisema hapana, Jimbo la Kitope asilimia 51, Jimbo la Uzini asilimia 74, Jimbo la Chwaka asilimia 59, Jimbo la Makunduchi asilimia 78, Jimbo la Muyuni asilimia 74 na huko kuna viongozi, lakini walifanya juhudi waliwaambia wananchi wao wakawafahamisha lakini wananchi wakaamua wala hakuna mtu aliyewasaliti. Baadhi ya hawa majimbo yao leo wako mbele, Serikali haijatizama, Dr. Ali Mohammed Shein hajajali kwa sababu wananchi wetu tuliwapa uhuru waseme ndio au hapana wala sio kufa, hii hapa *record* na hii hapa ripoti wako mbele kule.

Sasa Dr. Shein amesema hivi juzi, mapema kabla ya Tume hiyo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika nyakati tofauti amekuwa akiwasihi wananchi wa Zanzibar kutoa maoni yao kwa Tume hiyo bila ya woga bila ya jazba. Na mimi naunga mkono twendeni Rais wetu keshatuagiza tukatoe maoni yetu bila jazba bila ya woga, tena inasema ripoti hii.

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wameeleza fursa hiyo kuwa ni muhimu na adimu, hivyo Wazanzibari hawana budi kutimia ipasavyo kwa kueleza namna ambavyo wao wanataka Katiba ya Jamhuri ya Muungano iwe vipi. Sasa wanaotoa vikaratasi wanataka moja, wanaotaka mbili, wanaotaka tatu, wanaotaka kumi, waachiwe wakatoe maoni yao na sababu. Lakini kwa sisi Wazanzibari mimi nina rafiki zangu wako Bara huko sehemu nyingi tatu tu, wana sababu sababu zao wenyewe lakini sisi Wazanzibari tumeungana, sasa zile kero ambazo zinatukera ndio tuwaambie wananchi wetu tuwafahamishe na tuwaelimishe. Kwa sababu Tume hii ya Nyalali inazungumza kuelimishana sio hii Tume ya Warioba.

Warioba amesema tume yake inafahamu umuhimu wa elimu ya uraia kwa wananchi ili waweze kushiriki vizuri katika zoezi hilo na kwamba tume yake imefanya jitihada mbali mbali kuwaelimisha wananchi. Hata hivyo, amesema

vyombo vya habari bado vitakuwa na jukumu kubwa la kuelimisha wananchi je, Serikali inasema haielimishi, Serikali lazima tukae wala Wizara ya Katiba na Sheria si Serikali, yeye ataisemea wizara yake tu. Serikali humu ndani inasemewa na Makamu wa Pili wa Rais wala asijibu leo, ipo haja Serikali tukate, Baraza tukae tuelimishe watu wetu hatwendi kuulizwa mnataka hamtaji? Aa, tunakwenda kufanya marekebisho ya Katiba au Katiba mpya ya Muungano.

Sasa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais mimi nakuelewa tena nataka nikupongeze, kero za Muungano zimeanza tangu mwaka 1964. Kuanzishwa *Peoples Bank* imetokana na kero za Muungano ikaundwa tume akasema Mzee Karume 'hapana pesa hairuki hapa tutafungua *central bank*', zote ni kero za Muungano zikaendelea, zikaendelea mpaka Dr. Salmin Amour Juma akaleta mambo ya *OIC* na mengine.

Mhe. Hamza Hassan umekosea, hatujavunja Katiba kwa kuunda Shirika la Bandari. Kwa sababu Shirika la Bandari sisi tulitaka kuunda *Zanzibar Shipping Authority* wakatwambia aa, *authority* hapana Dr. Salmin Amour mtu wa hekima na busara akasema alaa basi *corporation* tukaambiwa sasa fulil ruhusa tukaanzisha. Lakini bado ndani ya Katiba Bandari ndio Muungano, Dr. Salmin mtu aliyekuwa na hekima na busara hakutaka ugomvi akasema haya, *authority* futa. Mimi ni mjumbe wa mwanzo nilikuwa Chicago wakati napata simu kuwa nimechaguliwa kwenye Bodi ya Bandari mimi na Mhe. Haji Omar Kheir.

Mhe. Mwenyekiti, mimi hizi safari safari nimeanza zamani sana Chicago, Ulaya, wapi mimi sio kama nimeanza safari kuja hapa Barazani za China sijui za wapi aa, mimi nimezunguka. Mtu mmoja ananambia wewe hupati safari nikamwambia mimi nishachoka safari, mimi nishasafiri. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hajakosea sasa wakati umefika Balozi kaingia Awamu hii ya Saba, Dr. Shein kaingia Awamu ya Saba ndiye aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati yangu ile ya Mawaziri. Lakini miaka yote Mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mawaziri wa Bara wanakutana wanazungumza Rais Kikwete akaema safari hii kutaneni japo hamna maneno mseme tu je, habari hamjambo, habari ya siku nyingi, wazima?

Kwa taarifa nilizonazo kikao kimoja tu kimefanywa cha mawaziri, unajua penye watu wengi habari zinapatikana, Balozi Seif Ali Idd kataka Wazanzibari wamtambue kama ni mkereketwa na juzi kasema ana uchungu wa nchi hii. Kaweza vikao tena kuongoza na wenzake, juzi imetoka kauli hapa kwamba baada ya miezi mine kauli hii ni mpya nimeisikia zamani. Kwa hivyo, juhudi iliyofanywa na hawa jamaa, mawaziri wetu tuwashajihishe.

Mhe. Balozi Seif Idd mchukue Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kasema kwenye vikao kule anaweza kwenda wewe mchukue tu ndani asiingie, kwa sababu ukinichukua mimi tatizo huyu Mwakilishi wako mchukue pale apige suti, anapiga miwani ya jua ile unawaambia Mhe. Mshimba yuko nje labda itasaidia. *(Kicheko)*

Lakini Mhe. Balozi mimi nakupa hongera sana kwa jitihada uliyoifanya na juzi umeahidi na msije mkambana akaja akashindwa, kwa sababu tunaomba yale yote ambayo sisi tumeyafanya bendera, sijui nini yote lakini naamini kwa uwezo wake na juhudi zake na sisi tuko nyuma yako Balozi hatukugandi nyuma yako tuko, Balozi usiwe na wasiwasi Baraza hili liko nyuma yako nenda ukawaambie na wanasikia wachukulie *hansard*. Nakutakia mafanikio kwenye shughuli yako hiyo, Balozi wewe si mtu wa leo wewe ni Naibu Katibu Mkuu wa Chama chetu cha Mapinduzi umekuwa, umekuwa Balozi Canada, China, mzoefu mimi na wewe tunajuana sana una uwezo tumia uwezo wako ukiondoka Baraza hili ufanye historia wakati wa Balozi Seif lilikuwa hili, lilikuwa hili, usiondoke hapa kimyakimya tu na ushafanya historia.

Kwa hivyo tuko nyuma yako, mimi nakwambia ndani ya moyo wangu sio ile kupiga *brush* ni ndani ya moyo wangu nakwambia na hawa wote wako nyuma yako wewe ndiye mkubwa wetu. Sasa hii nchi yetu watu jana wanasaema sijui ghasia, lakini Mhe. Mwenyekiti, sisi ni Wazanzibari. Nimeiona ile picha ya mawaziri wale.

Mhe. Mwenyekiti, kwa taarifa tu watu waone nikuletee halafu kama utakubali watu waione halafu nirejeshewe mwenyewe. Nimemsikia sasa hivi hapa anazungumza Mapinduzi yamefanywa na Chama cha Afro Shirazi, kwa sababu walikosa viti dhulma ikawa, lakini Mapinduzi yana malengo yake na tulipokuwa tunatembeza kura za maoni tuliwasomea wananchi Unguja nzima malengo ya Mapinduzi na ndio wakachagua hii Serikali kwa kujua haya ndio malengo. Mhe. Mwenyekiti, niruhusu nisome.

Sheria Nam. 6 ya Katiba inayotambua kuwepo kwa Usawa, Maridhiano na Umoja wa Watu wa Zanzibar katika kutekeleza uwezo waliopewa uwezo wa kutunga sheria ya 1964, Rais wa Jamhuri kwa kushirikiana na kukubaliana na Baraza la Mapinduzi imetunga sheria ifuatayo:

Sheria itajulikana kama ni Sheria ya Usawa, Maridhiano, Umoja wa Watu wa Zanzibar. Madhumuni makuu ya Mapinduzi ya Watu wa Zanzibar ni kutokomeza upendeleo wa kiuchumi, kijamii na upendeleo wa kisheria na mapungufu yote yaliyopita yaliyokuwa yanawagawa wananchi na makundi mbali mbali ya raia kwa njia ya ukabila, jinsia, dini au asili ya mtu na

madhumuni hasa ya mapinduzi ni kukuza usawa, maridhiano, umoja wa watu wa Zanzibar.

Kwa msingi huo, kila raia wa Zanzibar anatangazwa kuwa ana haki sawa, fursa na hifadhi ya uraia wake kama vile ambavyo anatekeleza majukumu yake na wajibu wake wa uraia. Hakuna haki, fursa au hifadhi inayoweza kufutwa kisheria kwa raia yeyote kwa kutumia vyombo vya dola, au kwa kutumia vyombo vya mtu binafsi, kwa sababu ya msingi wa visingizio vya ukabila, dini, jinsia, uraia huo. Hakuna kifungu chochote ndani ya sheria hii kitazuia serikali kutunga sheria itakayotoa nafuu, sio kupunguza nafuu zaidi maalum na upendeleo wa kiuchumi, kiutamaduni, kijamii, kwa raia waliokosa haki ya msingi kwa madhumuni ya kuelezea hii.

Sheria hii ilisainiwa tarehe 25 Februari, 1984. Ninakuomba Mheshimiwa nikuletee hii. Tuligawa wakati ule labda ukipenda tutoe kopi tuwagaie Wajumbe iwe kama hirizi wanatembea nayo.

Sasa ninataka nimalizie. Naomba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuwe wavumilivu, tustahamiliane. Sisi ni viongozi, tukisemwa, tukitukanwa ndio viongozi. Musitukanwe huku mukaja huku mukajibu eeh! Mimi mwenyewe katarasi nyingi zilitupwa na kutukanwa kila matusi.

Leo walionitukana wananikumbatia, wananitaka msaada, ndio mambo. Sasa muhimu tutekeleze wajibu wetu tujenge nchi yetu. Musilazimishe watu kuwa na msimamo mmoja, haiwezekani. Tuelimishe lakini wananchi wa Zanzibar wanajua kuwa Zanzibar ni yao. Zanzibar ni kwanza.

Hii Katiba inazungumza haki za Zanzibar. Kwa hivyo hakuna kosa lakini sisi tuelimishe watu. Wala tusiseme fulani katoa karatasi na wewe katoe tu kwa sababu sheria inaruhusu. Lakini hairuhusu njiani kuzitupa. Unaweza kupeleka maoni yako kule kwenye Tume. Vyama vya siasa vimeruhusiwa vinapeleka maoni yao. Haya maoni yao ya CUF, CCM wanapeleka kwenye Tume kwa sababu sheria imeruhusu.

Lakini Serikali ya Zanzibar, Baraza la Mapinduzi sisi ndio wasemaji wa wananchi lazima tuwe na muongozo, tujue tunafanya nini wananchi wetu kuwaelimisha. Kama hamjatupa basi tutawaomba wanadhimu wetu wawili tukae tuzungumze tufanye kazi, lakini haifiki hivyo kwa sababu sisi sote ni wamoja, nchi yetu ni moja. Sote sisi tunaapa.

Tuna ile kanuni asubuhi tunaisoma hapa, tunasema huyu bwana! Huyu hapa, Hamza eeh! Njoo hapa, huyu bwana hafai bwana aah. Huyu hajazoea huyu, huyu bwana usimpe *advantage*.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa tuzingatie muda

Mhe. Ali Mzee Ali: Eeh! Vipi?

Mhe. Mwenyekiti: tuzingatie muda.

Mhe. Ali Mzee Ali: Hii ni ya mwisho kwa sababu ni muhimu sana. Ile dua tunayosoma. Sisi asubuhi tukiingia hapa tunasoma dua, na ile dua tunaisoma hapa ni dua muhimu sana, na sisi humu ndani tunaapa. Lakini kuna *fashion* mpya Katiba mbili, Katiba tatu lakini tunaomba dua asubuhi.

Ile dua ambayo tunaomba asubuhi, leo balaa nani ananiroga huyu.
Dua ya kuliombea Baraza. *Tunakuomba Mwenyezi Mungu, mwenye rehema, mwingi wa utukufu, bwana wa viumbe vyote, muumba mbingu na ardhi, tunakuomba uiweke nchi hii ya Zanzibar ikiwa ni miongoni mwa nchi mbili zinazounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya himaya, ulinzi wako na utukufu wa milele, ibariki Zanzibar iwe nchi ya amani na wote wanaoishi humo wawe na upendo na umoja, tuepushe na tamaa mbaya, chuki na ubinafsi na utulinde na maadui ambao wanaitazama Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa jicho la husda, umjaalie Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi afya njema, hekma, busara kwa kusaidiana na viongozi, uwezo wa haki na amani kwa manufaa na ustawi wa Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*

Sasa kwa nini nikasoma hii Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunaiombea dua humu ndani asubuhi. Mpaka sasa hivi Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama Salmin Awadh yupo, hivi sasa sera zimebadilika, tulikuwa na sera ya chama kimoja, baadae mwaka 1991 tukawa na sera ya vyama vingi. Sera zimebadilika, lakini kwa sasa hivi Jamhuri ya Muungano ndio ipo na bado tunahitajia.

Lakini la mwisho kabisa tulipopindua tulitambuliwa. Nchi ambazo zimetutambua Cuba wametutambua tarehe 23 mwezi wa kwanza mwaka 1964, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hiyo, Serikali ya *Ghana* tarehe 28 mwezi wa kwanza 1964, *Republic of Cameroon* tarehe 30 mwezi wa kwanza 1964, *German Republic* tarehe 30, *People of Poland* tarehe 30, *Ireland*, *United Arab Emirates*, *Soviet Union* mwezi wa Februari, *China* tarehe 6 mwezi wa pili, *Nigeria* tarehe 18, *India* tarehe 22, *Britain* tarehe 24 Februari, Marekani tarehe 24 Februari, *Mali* tarehe 26, *Congo* tarehe 26, *Sierra Leone*, *Liberia*. Ni nchi 18 zimetutambua kabla ya Muungano.

Hapa Zanzibar zilikuwepo afisi za ubalozi. Tulikuwa na ubalozi wa Ghana, German, Israel, Soviet Union, China, Uingereza na Vietnam. Hizi balozi zilikuwepo kabla hatujaungana. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mafupi sina tabia ya kusema naunga mkono hoja hii.

Ninamuomba Mhe. Waziri, Katiba umeitunga wewe ya mwaka 1984 ukiwa ni Mwanasheria Mkuu. Mhe. Abubakar umekuwa mpinzani humu ndani muda mrefu. Leo Waziri wa Katiba na Sheria.

Jukumu la nchi hii lipo kwenye kichwa chako. Umeandika makala nyingi za muungano. Umewajibu akina Mvungi, sijui Tundu. Mhe. Abubakar ulimwambia Mhe. Ali Juma Shamuhuna ikiwa pita Kisumu, pita Naivasha, pita Mombasa, ninayo *hansard* yako, pita wapi. Shamuhuna tupo nyuma yako. Hayo uliyasema wewe Abubakar, na sisi leo tunakwambia Abubakar tupo nyuma yako, usitetereke, umri wako tena ni mkubwa, jenga historia. (*Makofi*).

Kwa hayo mafupi ninashukuru sana. (*Makofi*).

Mhe. Mohamed Mbwana Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi namshukuru Mwenyezi Mungu mchana huu wa leo kupata nafasi hii ya kuchangia Hotuba ya Waziri wa Katiba na Sheria.

Hotuba ambayo ni muhimu mno katika nchi yetu hii ya Zanzibar. Lakini pia ninachukua nafasi hii ya makusudi kumpongeza Mhe. Mzee wetu Bwana Ali Mzee Ali kwa maelezo yake na ufafanuzi wake, ambayo maelezo yake ni dira kubwa sana kwa Wazanzibari, mbali ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi lakini hata kwa Wazanzibari hivi sasa ambao wanalisikiliza Baraza hili.

Bwana Ali Mzee kwa kweli niseme kuwa ni tegemeo kubwa kwa Wazanzibari, kwa sababu anayajua mengi ambayo vijana wengi wa hirimu zetu katika nchi hii hatuyajui. Kwa hivyo Mhe. Ali Mzee Ali hongera sana. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo kwa Bwana Ali Mzee, nachukua nafasi hii na mimi kuchangia kidogo kuhusiana na mahakama. Mhe. Mwenyekiti, wengi wamesema kuhusiana na habari ya mahakama kuwa Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo wapewe angalau na wao nyongeza yao ya mshahara, wajisikie kwamba na wao ni wafanyakazi wa Mahakama kama walivyo wafanyakazi wengine wa Mahakama ambao tayari wameshatengenezewa haki zao.

Mhe. Mwenyekiti, la pili kuhusiana na Mahakama niseme kwamba inafaa kabisa majengo ya Mahakama yaangaliwe ili yawe ya kisasa kwa mujibu wa taratibu zetu zilivyo. Lakini pia Mahakimu wapatiwe vitendea kazi, si vespa tu bali wapatiwe vitendea kazi na vipando vya kwendea kazini vinavyostahiki kwa mujibu wa nafasi zao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya kuuchunga muda ninataka niendelee kidogo katika Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali ukurasa wa 34. Mhe. Mwenyekiti, afisi hii imekuwa na changamoto nyingi. Ninataka nizungumze hapa kimuhutasari kwamba afisi hii ina jukumu kama alivyosema mwenyewe mtaalamu hapa kwamba imesajili kampuni 139, majina ya biashara 271 na mpaka mwisho wa maelezo hayo.

Ninachotaka kuzungumza kwamba afisi hii imesajili kampuni kama hizi 139 lakini jambo la kusikitisha, ninataka niingie katika kitabu cha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali jinsi afisi hii inavyovujisha mapato ya Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, ukaguzi umebaini kwamba kuna baadhi ya kampuni zimesajiliwa kwa muda mrefu, lakini kampuni hizo zimeshindwa kuwasalisha hesabu zao za mwaka na kutoweza kulipa marejesho. Hatimaye kuweza kuikosesha mapato serikali. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya Mrajis Mkuu wa Serikali, na vile vile kampuni zinashindwa kuwasalisha hesabu zao za mwaka kwa Mrajis Mkuu wa Serikali, yanastahiki kupewa adhabu.

Lakini ukaguzi umebaini karibu asilimia 70 ya kampuni zilizosajiliwa Zanzibar hayawasilishi hesabu zao kwa Mrajis Mkuu wa Serikali. Hata hivyo tumegundua kampuni hizi hazilipi gharama hizo kwa kiasi fulani ufuatiliaji haupo.

Mhe. Mwenyekiti, ninamuuliza Mhe. Waziri kutokana na ripoti hii ya Mkaguzi ambayo ina mamilioni ya shilingi, jee Mhe. Waziri anatuelezea nini juu ya kufuatilia kampuni hizi kulipa mafao na badala yake tunawatoza wananchi wa Zanzibar kodi ya vitu mbali mbali. Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri hapa atupe ufafanuzi wa kutosha kwa nini mapato haya yanavuja bila ya kufuatiliwa.

Mhe. Mwenyekiti, ninataka nimwambie Mhe. Waziri kutokana na upungufu huu wa kutoyafuatilia mapato haya serikalini, wananchi wengi wanapata taabu kwa sababu haya mazoea katika wizara mbali mbali ikiwa wizara yake tumeyaona haya.

Mhe. Mwenyekiti, nikiacha hapo niendelee kidogo katika Afisi ya Vizazi na Vifo. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri ya Mhe. Waziri kwamba wamejipanga vizuri lakini bado mrundikano wa vyeti vya kuzaliwa kwenye Afisi za Wilaya bado upo, na wananchi wetu wanapata taabu kubwa kuvipata vyeti hivi kwa wakati.

Sasa mimi ningemuomba Mhe. Waziri kwamba aweke sheria kando ili wananchi wetu wale ambao wana umri mkubwa, wanaostahiki kupata vyeti vya kuzaliwa wapatiwe vyeti vya kuzaliwa bila ya masharti magumu. Sisi Baraza la Wawakilishi tunaweka Kanuni kando hapa kwa kuongeza muda. Kwa hivyo na yeye kama ruhusa inamkubali aweke sheria kando ili wazee wale wapewe vyeti vya kuzaliwa, waendelee na kupata haki zao nyengine kama vile vitambulisho vya Uzanzibari Mkaazi.

Mhe. Mwenyekiti, mbali na wazee walio na umri mkubwa, kuna hawa watoto ambao wanazaliwa katika miaka ya karibuni hivi, kunakuwa na mrundikano wa vyeti vinachelewa kufika kwa walengwa. Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri atoe tamko rasmi la muda mahsusi baada ya kuzaliwa mtoto na kuandikishwa mtoto, ni muda gani ambao mzee wake atapata cheti hiki cha kuzaliwa bila ya usumbufu wa kwenda rudi, rudi nenda, kwa sababu watu wetu wengi wanakaa vijijini. Kutoka kwenye eneo analokaa mpaka kwenye Afisi ya Wilaya ni nauli karibu shilingi elfu mbili kwenda na elfu mbili kurudi. Mtindo huu utaendelea mpaka lini. Tunamuomba Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri atengeneze mazingira mazuri ili tuwaepushe watu wetu na usumbufu huu ambao hivi sasa unatokea.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kuna taarifa ambayo vyeti vingi vinapotea kutokana na Masheha. Baadhi ya Masheha wanapoteza vyeti kwa sababu wanachukua fedha za wazaliwa kwa lengo la kuwarejeshea vyeti, lakini mwisho wake vyeti vile havipatikani, Sheha anatoa taarifa tu kwamba cheti chako keshokutwa mpaka mtu anatimia miaka mitano au sita hajapata cheti cha kuzaliwa kwa sababu ya Sheha. Kwa hivyo ningelimuomba Mhe. Waziri hapa atoe taaluma ya kutosha kwa wananchi na Masheha, ili wajue dhamana zao na wananchi wajue haki zao za kufuatilia vyeti.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu niende katika Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. Mhe. Mwenyekiti, Kamisheni hii ina kazi nyingi na muhimu. Ina kazi kama ilivyoeleza kwenye kitabu; kukusanya kodi na kuzigawa kwa wanufaika wa mali hizi za wakfu. Hapa ningemuuliza Mhe. Waziri, jee ni nani hao wanufaika, kwa sababu wanufaika hapa wametajwa hapa wanufaika gani na wana sifa gani ambazo zinawafanya wawe wanufaika ili kugaiwa haki hizo.

Halafu vile vile Kamisheni hii imeweka mfumo wa zakka, kwa kweli hili ni jambo zuri kwa sababu watu wengi hivi sasa wana uwezo wa utoaji wa zakka, lakini hawapati labda ushajihishwaji. Tunaiomba Kamisheni hii iwashajihishe watu katika kutoa mali zao zakka ili ziwafikie wale walengwa wanaostahiki.

Kamisheni imefungua akaunti kwa mujibu wa kitabu. Kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri ataje nambari ya akaunti hii, ili wale wenye uwezo wa kuingiza fedha hizi moja kwa moja waziingize ili wanufaike wale wanaostahiki.

Mhe. Mwenyekiti, nikiacha hapo nitakuwa ni mchache wa fadhila sana ikiwa na mimi sikugusia jambo muhimu ambalo linazungumziwa sana katika nchi yetu hivi sasa kuhusu marekebisho ya Katiba.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mimi niseme kwamba Zanzibar hivi sasa imefika pahala pazuri ambapo inaweza ikajinasua au inaweza ikajididimiza. Kwa maana hiyo, mimi ninaomba kwamba Wazanzibari sote kama maelezo mbali mbali yaliyotolewa na wazee wetu waliopita hivi sasa, na waliochangia tokea jana na leo asubuhi kuhusu na ukusanyaji wa maoni, tuwe tayari kukusanya maoni yetu ya pamoja. Lakini nielezee suala la Mhe. Ali Mzee alilozungumza kwamba Mhe. Abubakar ana haki kubwa ya kuwasimamia Wazanzibari haki yao.

Ninataka nimkumbushe Mhe. Waziri ule usemi wake aliousema jana alipokuwa akiisoma ripoti yake, usemi aliou-*quote* kwa Sayyidina Omar Ibn Khatwab aliposema *ni vyema kuiendelea haki iliyokudhihirikia kuliko kudumu katika batili ulioizoea*. Zanzibar ni haki yetu. Kwa vile Zanzibar ni haki yetu ni juu yetu kabisa kuuelewa usemi huu wa Sayyidina Omar ili kuirudisha Zanzibar katika hadhi yake. Ili Zanzibar iwe na hadhi yake Mhe. Mwenyekiti, ni kuhakikisha kwamba Zanzibar ina kiti chake Umoja wa Mataifa. Zanzibar ina uhusiano na nchi nyengine, Zanzibar inafungua ubalozi katika nchi mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ali Mzee alisema hapa, Zanzibar kabla ya muungano ilikuwa na balozi katika nchi kazitaja nimezihesabu saba, lakini nimuulize Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, jee baada ya muungano Zanzibar ina balozi ngapi hivi sasa katika nchi za nje.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niseme kwamba kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Chambani, nitaunga mkono hoja baada ya maelezo atakayonifafanulia Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kama yale niliyomuuliza.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*).

Mhe. Abdalla Mohamed Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, wakati umeanza kutukimbia lakini sisi wengine tuliopitia ualimu tutafanya *summary* kidogo angalau na sisi tusikilikane.

Kwanza ningempongeza jirani yangu hapa na ile aya inayosema *'Wafauka kullu dhuu ilmin aliym"* Imethibitisha kwamba ukiwa kuna wanaojua, basi ujue kuna wengine wanajua zaidi. Ninampongeza kwa hilo.

Mhe. Mwenyekiti, tumo katika marekebisho na mimi sisemi marekebisho, tunasema kuandika Katiba mpya, na ninafikiri watu wengi itabidi walijue hilo kwamba hapo nyuma tulikuwa tunatia viraka Katiba yetu, lakini mwaka huu ni fursa pekee kwamba sisi hatutii viraka, yale yote yaliyokuwa yanatukera kwa muda wa miaka arobaini na nane, sasa tunatakiwa tuyaondoe.

Kwa maana hiyo sasa tunashona koti jipya, linatakiwa hili liwafae watu wote. Sasa ninachohisi kwamba kulikuwa kuna umuhimu mkubwa wa hili koti tutakavyolishona litufae sote. Sasa ilikuwa kuna jukumu kubwa la watu kuwapa elimu ya kujua nini tunachotaka kukifanya. Wengi hivi sasa hawafahamu tunafanya nini, na ndio ukakutia wanakwenda wanasema mimi sitaki muungano.

Tunafanya Katiba mpya, hatutii kiraka. Kwa hivyo kama tunafanya Katiba mpya kuna mengi tunayoyataka tuyaandike. Mhe. Waziri tunapopeleka watoto wetu chuoni mara nyingi huwa tunawapeleka kwa kuanzia na juzuu, hatuwapeleki tukaanza na misahafu. Kwa kujua kwamba tukiwapa na juzuu ndio mwanzo, tukiwapeleka kwenye misahafu hawatofahamu, kwa sababu hawajaupata ule msingi wa mwanzo. Sasa katika hili ninahisi mimi kwamba tutafeli kwa sababu hakuna uelewa, watu hatufahamu chochote hivi sasa, tunataka kufanya nini.

Sasa hili mimi ninahisi ni jambo la kitaifa. Sasa kama ni jambo la kitaifa bila shaka litakuwa na *national interest*. Sasa kama kuna *national interest* itakuwaje sasa tuwaache wananchi wenyewe moja kwa moja, lazima kulikuwa kuwe na muongozo fulani. Si hivyo tumeingizwa kwenye msahafu sura hatuzifahamu, tutafeli Mhe. Mwenyekiti.

Namuomba Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri muda bado upo wananchi wakaelimishwa tunataka kufanya nini. Tunakwenda kuandika Katiba mpya. Kwa hivyo kwa vile ni Katiba mpya itajaa kila kitu sio suala la muungano tu. Wengi tushaelekea kwenye muungano, kwamba kila mmoja anasema muungano siutaki, sio hilo. Kuna mambo mengine mengi kama ya kodi na

mengineyo yatakuwemo katika Katiba hiyo. Sasa uelewa wa wananchi ni muhimu kwa hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, ninakwenda kidogo kwenye Tume ya Marekebisho. Ninachofahamu mimi tunapofanya marekebisho huwa mara nyingi tuna madhumuni yake na sababu zake. Sisi tuna Tume yetu hii ya marekebisho. Sasa Tume ya marekebisho kazi yake kubwa ni kuangalia jee ni sheria gani hivi sasa ipo na kasoro au ipo sawa sawa.

Sasa mimi ninachotaka kujua hivi tunavyofika kuiona sheria hii ina matatizo, tunaiangalia kwa upande wa serikali tu au tunaiangalia pia kwa upande wa wananchi, kwamba wanayo fursa ya kusema kwamba hii sheria hivi sasa tunayoiona ina marekebisho.

Mhe. Mwenyekiti, kwa nini ninasema hivyo kwa sababu hivi sasa tuna sheria ambazo zinawahusu moja kwa moja wananchi, na sheria hizi zinazowahusu wananchi basi tunaziona sisi hazitufai. Kwa maana hiyo sasa hii tume labda ingekuja na kwetu sisi ikatusikiliza kwamba vipi munaonaje. Katika hili kuna sheria ambayo hivi sasa wengi sana inatupa shida ile sheria ya vitambulisho.

Mengi yameshasemwa hapa katika vikao vilivyopita lakini bado sheria hii ina matatizo, na ni kikwazo kwetu kwa sababu haina maendeleo yoyote ya kijamii wala kisiasa. Sasa jee ningeliwauliza sheria hii itakuwa imo katika orodha ya marekebisho ambayo yatakuja hivi karibuni au ipo tu itaendelea kuwemo.

Lakini katika hilo pia hapa tulifanya marekebisho ya 10, tukasema kwamba Zanzibar ni nchi hivi sasa ndivyo tunavyosema katika Katiba yetu, lakini jee katika sheria hii hivyo kuna maendeleo yoyote yaliyopatikana kisiasa au kiuchumi baada ya kutamka tamko hili kwamba Zanzibar au tumeiweka tu katika orodha ya marekebisho na tukaiweka kwamba Zanzibar ni nchi. Kuna mafanikio yoyote.

Ikiwa sababu ilikuwa ipo, jee ile sababu tumeanza kuifikia kwamba kweli sasa tunaweza tukasema kuwa Zanzibar ni nchi. Mhe. Mwenyekiti, ninajua muda unatukimbia labda kidogo niende kwenye Kamisheni ya Wakfu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwakilishi mwanzo tulizungumza kwamba dakika zilizobakia ni chache mno na muda wetu kwa mujibu wa Kanuni umemalizika. Sasa labda tuchukue fursa hii kuwaomba wale Waheshimiwa ambao bado walikuwa wanataka kuchangia, lakini kwa mujibu wa utaratibu wetu na wakawa hawakupata nafasi ya kuchangia, tuwaombe radhi basi.

Vile vile tuwape fursa ya kuchangia japo kwa maandishi. Waheshimiwa waliosalia mpaka sasa ni Mhe. Rufai Said Rufai, Mhe. Hassan Hamad Omar, Mhe. Farida Amour Mohamed, Mhe. Mbarouk Wadi Mussa, Mhe. Salim Abdalla Hamad na Mhe. Panya Ali Abdalla.

Waheshimiwa hao walikuwa wamebakia kwa ajili ya kuchangia, na kwa bahati mbaya kutokana na ratiba yetu ilivyo jioni tunatakiwa tufanye majumuisho. Kwa hivyo naomba kukufahamisheni kwamba jioni tutakapofika tutamkaribisha Mhe. Mwanasheria Mkuu ili aweze kusaidia kujibu baadhi ya hoja pamoja na mchango wake, na baadae tutamkaribisha Mhe. Waziri ili aweze kutuletea majumuisho ya shughuli yetu hii ya leo.

La ziada Waheshimiwa Wajumbe kabla sijaakhirisha kikao kuna ombi hapa limeletwa hapa kwamba niwatangazie wanawake wote Wawakilishi kuwa baada ya kikao hiki leo, saa 7:30 wataendelea na mafunzo yao katika maeneo ambayo ni kawaida kwa upande wao.

Baada ya maelekezo hayo sasa ninachukua fursa hii kuakhirisha Baraza hili hadi saa 11.00 jioni.

Ahsanteni sana.

(Saa 7.00 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa karibuni tena. Majadiliano yanaendelea. Nimepewa taarifa kwamba tumefikiwa pahala kwamba wachangiaji wapo baadhi ambao hawajapata nafasi kwa sababu ya muda, lakini kuna mchangiaji mmoja halafu baada ya hapo tumkaribishe Mhe. Waziri. Naomba basi nimkaribishe Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, kwanza na mimi naomba nichukue fursa hii kukushukuru kuwa kunipa fursa hii ya kuchangia hoja ya Mhe.Waziri wa Katiba na Sheria.

La pili waliotangulia wametoa pongezi nyingi kwa Mhe. Waziri lakini na mimi naomba niwahakikishie tu kwamba pongezi zilikuwa ni sahihi kabisa, tunashukuru tumepata Waziri mahiri, makini na mweledi vile vile. Kwa hivyo ninaamini kwamba Waheshimiwa Wajumbe watapitisha hoja yake, watapitisha bajeti hii ili imuwezeshe kufanya kazi zaidi katika mwaka unaokuja wa fedha.

La tatu katika michangio mbali mbali iliyotolewa, kwanza nikianza na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Mhe. Jussa, wao walitoa pongezi nyingi kwangu binafsi kutokana na utendaji. Nasema hili niseme tu kwamba mimi ninazichukua pongezi zao kama ni deni. Ninajua kama ni deni kubwa kwa sababu deni kama lingekuwa la pesa unarejesha tu, hadithi imekwisha lakini deni la ufanisi ni kubwa na kwa kweli linahitaji kujituma zaidi. Mimi naomba niwaahidi kwamba nitajitahidi kutumikia, kuwatumikia, na kuitumikia serikali kwa ukamilifu na kwa uadilifu na juhudi zangu zote.(*Makofi*).

Katika michango mengine iliyotolewa labda nilisema nichangie kwa kujaribu kujibu baadhi ya hoja ambazo zimetolewa. Ninaamini kwamba Mhe. Waziri amejiandaa vizuri kujibu hoja nyingi na kwa hivyo nisichukue muda mwingi ili apate fursa ya kutosha ya kuweza kujibu.

La kwanza ni Mhe. Rashid Seif Suleiman alitaka kujua tu kuhusiana na uhusiano baina ya wanasheria waliopo katika taasisi za serikali na wale waliopo katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mimi nimwambie tu kwamba kwa hivi sasa kwa kweli hakuna uhusiano rasmi isipokuwa tu wote ni waajiriwa wa serikali na inapotokea haja tunawaita na kushauriana nao baadhi ya mambo.

Lakini kama nilivyosema katika hotuba ya Mhe. Waziri kwenye ukurasa wa 20, tumeeleza mipango ya kuwaweka pamoja wanasheria wa serikali, kwanza kukuza viwango vyao kwa sababu wote hawa wanaisaidia serikali, wanaishauri serikali na wanafanya kazi za serikali. Kwa hivyo haitokuwa vizuri kwamba wamepishana sana katika viwango vya uelewa wa baadhi ya mambo ya msingi ya kisheria.

Kwa hivyo juhudi ya mwanzo na kama pengine tutaona katika fungu letu la mafunzo ya ndani tumeliongeza kidogo ni pamoja na kuwa-*commodate* kuwapatia angalau mafunzo ya msingi hawa wanasheria wengine wa serikali katika mambo ambayo tunahisi ni vizuri na wao wakayaelewa.
Kwa hivyo na itakapokuja sheria yetu basi tutaona namna gani na wao tumewa-*commodate* ili wawe ni kitu kimoja isionekane kama serikali katika suala hili hatupo *organized*. Itatusaidia kuwaweka pamoja.

Suala jengine ambalo liliulizwa au lilichangiwa na Mhe. Jussa lakini pia na Mhe. Omar Shehe ni kuhusiana na utungaji wa sheria, taratibu zile. Mhe. Spika, ilitolewa hoja hapa kwamba inaonekana labda miswada baada ya kupitishwa hapa kunakuwa na uchakachuaji, kwa maneno ya Mhe. Omar Ali Shehe.

Sikutegemea kama angetumia neno kuchakachua lakini kama kuna hitilafu ninadhani tukubali kama ilitokea na tutafute sababu kwa nini ilitokea. Lakini naomba nimuhakikishie kwamba kwa utaratibu wa utungaji wa sheria mpaka kusainiwa na Mhe. Rais. Kwanza jambo la kwanza kwamba tunaelewa hata Mhe. Rais kwa mfano, baada ya mswada kupitishwa na Baraza la Wawakilishi, anapotaka kufanya marekebisho yoyote katika mswada ule inabidi aurudishe tena Barazani.

Sasa seuze mtu mwengine ambaye ni wa chini kuliko Mhe. Rais. Kwa hivyo tunaelewa wajibu wetu baada ya mswada kwishakupitisha hapa ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba kile kile kilichopitishwa na Baraza hili basi kile kile kinakwenda kwa Mhe. Rais kwa ajili ya kupata *assent*.

Na kwa utaratibu ulivyo haiwezekani kuwa Afisi yangu mfano kufanya mabadiliko kwa sababu baada ya sisi kwa utaratibu tu tunawasaidia tu Baraza la Wawakilishi kufanya kutokana na ule uzoefu na wale waandaaji wa ile sheria, lakini baada ya hapo inarudishwa kwa Katibu wa Baraza na Katibu wa Baraza akishakujiridhisha kwamba ni sawa yale yaliomo katika ule Mswada, yeye mwenyewe anasaini kwanza, anafanya *endorsement*, halafu baada ya hapo ndio unapelekwa kwa Mhe. Rais kwa ajili ya *assent*.

Sasa kama kulitokea tatizo basi ninadhani hilo tatizo lilitokezea namna gani lakini sidhani ilikuwa kwa nia mbaya wala sidhani kama kuna utaratibu huo na wala sijawahi kuona wala kutuhumu wala kuwa na mashaka nao.

Kuhusiana na hii sheria ya elimu au Mswada wa Sheria ya Elimu wa Baraza la Mitihani, hata mimi aliwahi kulipigia Katibu Mkuu Wizara ya Elimu akaniulizia kuhusiana na hilo, nikamwambia na mimi sikuwepo bahati mbaya ulivyopitishwa huu mswada, lakini nilipata taarifa kwamba kulikuwa na mabadiliko hayo munayosema. Lakini tulipowapigia Afisi ya Baraza wakatwambia aah! kilichobadiliko ilikuwa ni jina la Bodi sio jina la Sheria.

Lakini hatimaye wenzetu wamegundua hiyo na wameshatuandikia barua ili kufanya masahihisho. Kwa kawaida marekebisho kama haya hayafanywi, yanafanywa kwa utaratibu tunaita kutoa tu masahihisho kwa uwezo alionao Mwanasheria Mkuu chini ya Sheria Na. 7 ya mwaka 1984 ya kufanya hayo marekebisho kama hayo madogo. Kwa hivyo hilo litafanyika lakini kama litaonekana kuna jengine limetokea tatizo kama hilo, litatusaidia sana katika kusawazisha jambo hilo ili pengine kuwa na utaratibu mzuri au kuwa makini zaidi katika kuweka mambo sawa, lakini naomba nimtoe wasi wasi kwamba halijafanywa kwa hila wala kwa njama, ni ubinadamu tu kukosea katika utendaji wa kawaida.

Na lile suala la kupeleka miswada kwa Mhe. Rais ya Kiswahili. Kusema kweli ni jambo ambalo ninadhani tunahitaji tuliwekee utaratibu mzuri zaidi kwa sababu mbali mbali. Kwanza kwa sababu bahati mbaya tumerekebisha huku lakini tunapokwenda Mahakmani bado Mahakama zetu hazijarekebisha taratibu zake za kutumia sheria ya Kiswahili katika shughuli zake rasmi.

Kwa hivyo ule mswada wa Kiswahili unabaki kama ni tafsiri ambayo mwisho wa siku kwa matumizi hasa ya kisheria unakuwa kama haina matumizi kwa ujumla kwa kweli. Sasa ni jambo kwa kweli ni *trick* lakini ni suala ambalo sheria mwisho wake inatumika kwa mtoaji wa haki na lazima tuandae utaratibu wa hili. Tutakaa na wenzetu wa Mahakama tuone na wao wanaweza wakafanyaje ili kile tutakachokitumia, juhudi tutakayoofanya baadae iwe na maana.
Lakini na pia kuna suala moja la msingi ambalo inabidi tuje turekebishe katika sheria ya interpretation, yaani sheria Na. 7 ya mwaka 1984, kusema inapotekea mgongano baina ya ile ya Kiswahili na ya Kiingereza basi ipi ita-prevail ili wanaotumia hizi sheria waweze kujua, kwa sababu sheria zetu hazitumiwi na Mahakama zetu tu hapa, zinaweza zikatumiwa na Mahakama yoyote inapotokea mtu kachagua sheria zetu kuzitumia.

Kwa hivyo hilo ni lazima tuliweke sawa na tutalifanyia kazi na tunachukua huo ushauri ili tuufanyie kazi na inshaallah kabla ya kumalizika mwaka huu wa fedha tutakuwa tumelikamilisha hilo.

Jengine ni suala la kutungwa kwa Kanuni. Mhe. Spika, tunachofanya afisi yetu hivi sasa mara baada ya kupitishwa sheria hapa, ikiwa inaanza baada ya kutiwa saini na Mhe. Rais, kwa kawaida huwa tunawaandikia wizara husika na pia kuwahimiza kwamba kama kuna tarehe ya kuchagua ili ianze kutumika kuwahimiza kwamba watafute hiyo tarehe ya kuanza kutumika na pia kuna Kanuni, pia kuwakumbusha kwamba kuna Kanuni.

Lakini kwa kawaida huu ufuatiliaji unakuwa baada ya hapo kusema kweli hatufuatilii kama Kanuni zimetungwa kwa sababu anayevaa kiatu ndiye anayejua kinakobana, kwa hivyo na wale watumiaji wa sheria hasa ndio wanaojua Kanuni wanazihitaji wakati gani na wanazihitaji Kanuni za namna gani.

Lakini tunachukua huo ushauri na tutaendelea kushauriana na wenzetu kutunga Kanuni. Kwa mfano Kanuni hizi za *public service*, sheria ya utumishi ya umma, tumejitahidi kukumbashana na wenzetu na hatimaye zimekaribia nadhani kukamilika, kwa sababu ilikuwa ni muhimu kuwa na Kanuni.

Suala jengine ambalo naomba nichangie Mhe. Spika, ni kuhusiana na ilielezwa hapa na Mhe. Jussa kwamba kuna rasimu ya Katiba ya Afrika ya Mashariki au ya Shirikisho la Afrika Mashiriki na kwamba hilo linaandaliwa, na kwamba labda linataka ifanywe juhudi hatimaye tuingizwe katika Shirikisho la Afrika Mashariki.

Mimi kwanza naomba nimuhakikishie kwamba na mimi nimepata hiyo inayoitwa rasimu. Kwa hivyo inaonekana kwamba kuna kitu kinachoendelea lakini tutafuatilia ukweli wake kwamba unafanywa kwa msingi gani.

Mhe. Spika, lakini naomba niseme kwamba baada ya ripoti ya Wangwe na wengi tutakumbuka, inayohusiana kutizama zile concerns za watu wa Afrika Mashiriki, yaani kila nchi iliunda tume kama ile ya Wangwe ili kutizama zile mambo au wasi wasi wa wananchi kuhusiana kuwa na shirikisho.

Na ile baada ya kutoa taarifa yake ikaundwa kamati ya wataalamu wa Afrika ya Mashariki. Likaundwa jopo la wataalamu wa Afrika ya Mashariki kuandaa kitu kinachoitwa *way forwad*. Na mimi nilipata heshima na bahati ya kuwa mmoja katika wataalamu hao 15 walioteuliwa katika nchi hizi tano za Afrika Mashariki, kila nchi ilitakiwa itoe wataalamu 3, kwa Tanzania nilikuwa mimi na Pro. Kabudi na mmoja ambaye hivi sasa ni Katibu Mkuu Wizara ya Ulinzi.

Moja ambalo lilijitokeza wazi ni kuna baadhi ya nchi zilikuwa zinaonesha hamu yao ya kuwa na Shirikisho la Afrika ya Mashariki, na walipendekeza kwamba iandaliwe hiyo rasimu ya Katiba. Lakini sisi Tanzania pamoja na Burundi tulipinga kata kata kwamba hicho kitu hakiwezekani.

Kwa upande wa Tanzania sisi tulisema tuna tatizo la msingi la Kikatiba. Mhe. Spika, ukiisoma ibara ya 98 ya Katiba ya Muungano na halafu ukasoma orodha ya pili, utaona kwamba haiwezekani kuwa Shirikisho la Afrika Mashariki kwa Tanzania haiwezi kuingia. Katiba inakataza na inakataza kwa sababu gani?
Kwa sababu inasema Katiba, kuwepo au kutokuwepo Rais wa Jamhuri ya Muungano suala hili ni lazima lipitishwe na Wabunge, *two third* ya Zanzibar na *two third* ya Bara. Na pia kuendelea kuwepo au kutokuwepo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni lazima ipitishwe na *two third majority* ya pande zote mbili.

Sisi hoja yetu ilikuwa tunawaambia kwamba kwa kadri tunavyofahamu Zanzibar iliingia muungano wa kisiasa na nchi moja tu, nayo ni Tanganyika. Sasa Tanganyika haiwezi ikatuingiza tena katika muungano wa kisiasa mwengine kwa kupitia mlango wa Tanzania. (*Makofi*).

Kwa hivyo kwa kadri tunavyofahamu sisi Wabunge wa Zanzibar hawawezi wakakubali tuingie katika Shirikisho la Afrika Mashariki tukiwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Labda uvunjwe muungano kila mtu awe na nchi yake, kama ataamua sasa kuingia kwenye muungano mwengine wa kisiasa, hilo linawezekana. Na hili tuliwahi kulizungumza na ikaja pia mission ya ya Kituo cha Katiba ya Afrika ya Mashariki, ikafanya hiyo study na ikaeleza hilo tatizo. Ninadhani wana kitabu kueleza kwamba kufanya Jumuiya ya Shirikisho la Afrika Mashariki haitowezekana hata nchi zote zikikubaliana kama Zanzibar haijakubali. (*Makofi*).

Kwa hivyo hiyo ndio position. Hivyo hata kama kuna rasimu wacha waendelee na rasimu lakini tunavyofahamu sisi kwa msimamo wa Kikatiba wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unless sisi wenyewe Zanzibar turidhie kuingia katika Shirikisho la Afrika Mashariki tukiwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hiyo ni shauri letu na hiyo ni hiyari yetu lakini si vyenginevyo. Kwa hivyo hilo tutaendelea kulifuatilia.

Mhe. Spika, jengine alilieleza Mhe. Hamza na baadhi ya waheshimiwa kuhusiana na elimu ya uraia kuhusiana na *GNU*. Mimi nawaomba niwaunge mkono kwa dhati kabisa kwamba kwa kweli kunahitajika elimu ya uraia kuhusiana na *GNU*.

Ninasema hivi Mhe. Spika, kwa sababu binafsi yangu nilinipa wasi wasi wakati ule nilipokuwa Mkurugenzi wa Mashtaka, nilikuwa ninajua kwamba taasisi ninazofanya kazi nazo, sisi kazi yetu ukiwa kwenye mashtaka sehemu kubwa pia ni kulinda amani ya nchi kwa kupitia usimamizi wa sheria. Lakini taasisi ninazofanya kazi nazo nilihisi kwamba zilihitaji kujua huu mfumo ili tuweze kufanya kazi zetu kwa urahisi usilete mzozo. Na nikachukua juhudi nikaomba pesa na ninashukuru *UNDP* wakatupa pesa za kutosha kuandaa semina kuhusiana ili kuwafahamisha hivi vikosi vyote kuanzia Polisi na vikosi vyote Unguja na Pemba tukafanya semina kuwafahamisha mfumo huu wa GNU.

Ninaamini na tulifanya semina hiyo mapema tu, mwezi wa Novemba ninadhani, mwezi wa Novemba, Disemba na Januari 2010/2011. Wenyewe hawa vikosi wali-*appreciate*, walisifu kwamba hili lilisaidia sana au liliwasaidia sana kuwapa upeo kwamba sasa wanafanya kazi katika mfumo gani.

Kwa hivyo ninadhani ni vyema na juhudi zikachukulia pia na taasisi nyingi zinazohusika ili huu mfumo kuufahamu na utatusaidia sana katika kufanya kazi zetu na kuondoa vikwazo ambavyo si vya msingi.

Kwa hivyo Mhe. Spika, mwisho nimalizie kwa jambo ambalo limezungumzwa sana. Kwa kweli leo walizungumza magwiji hapa, vingunge. Sasa inakuwa shida. Naona waliyozungumza kwa kweli kama yanatosheleza. (*Makofi*).

Mhe. Spika, na mimi nipate muda niyazungumze. Ninazungumza kwa sababu si kwamba yale waliyoyazungumza hayajatosha au hayajatosheleza, lakini kwa sababu ninahisi tu na mimi ni wajibu, na ninadhani wajibu sote kwa kila tunalolijua kuhusiana na jambo hili kulieleza, ku-*share* na wenzetu ili hatimaye katika mchakato huu uende salama na ulete tija kama ulivyokusudiwa, nao ni kuhusiana na hili zoezi linaloendelea la maandazi ya Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, mimi nimefarijika sana leo au tokea jana Waheshimiwa Wajumbe hapa walipokuwa wanazungumza, kwa sababu mimi nilikuwa na wasi wasi sana, na niliwahi kusema hapa kwamba jamani katika hili ni vizuri tukatafuta lile tunalokubaliana, kuliko kuhangaika kutafuta lile tusilokubaliana.

Kila mtu kama atazungumza katika lile tunalokubaliana basi hatimaye tutakuta kumbe hatuna tofauti. Maana hata dini Mhe. Spika, zina madhehebu lakini hatimaye kumbe katika mambo ya msingi dini ile, yale madhehebu si tofauti isipokuwa ni ufahamu wa mambo yale yale ambayo wenyewe hatimaye wanakubaliana.

Kwa hivyo na haya mawazo tofauti ninadhani ni namna tu wakati mwengine mtu alivyolieleza au anavyolielewa au wakati mwengine hata hapo pa kuanzia. Lakini sioni mimi baada ya kusikiliza mazungumzo ya humu ndani kama kuna tofauti ya msingi baina ya watu wa Zanzibar katika suala hili la muungano, maana kila mtu kasema kwamba muungano unaotakiwa uwe na tija na uwe na heshima vile vile. Sasa sijaona kama kuna mtu kasema tofauti na hayo. (Makofi).

Sasa mimi nilitaka kuzungumza kuhusiana na suala hili katika maeneo matatu. Eneo la kwanza ni kuhusiana ambalo limezungumzwa sana hapa misimamo ya vyama na zoezi hili linaloendelea au na utunzi wa Katiba. Katika hili Mhe. Spika, kwanza naomba nitanabahishe mambo mawili tu.

Jambo la kwanza ni kwamba Katiba ni ya watu. Hata ukisoma Katiba zote zilizotungwa kwa utaratibu huu wa kidemokrasia basi zinaanza kusema, "*we are the people so and so*". Hata tulipotunga ile Katiba ya kudumu ya mwaka 1977 ilisahauliwa ikaandika tu kwamba sisi *consitutency assembly* lakini ikabidi waje wabadilishe waseme, "*one behelfu of our people*".

Lakini Katiba hasa kwa kawaida inatungwa na watu, ni watu wenyewe. Yaani Katiba kama inachaguliwa timu basi vyama vinakuwa havimo kwa sababu hilo linakuwa ni jambo la watu wenyewe. Na kwa nini vyama havimo katika mchakato wa kutunga Katiba. Kwa sababu vyama vyenyewe navyo ni sehemu ya kujadiliwa.

Maana mtu sijui atasema watu waweze kujadili kuwepo au kutokuwepo vyama katika Katiba ni haki yao katika kujadili. Ni haki yao kwa sababu gani. Kwa sababu vyama ni vyombo vya tu vya kufika safari ambayo watu wanakwenda.

Mhe. Spika, Katiba yetu huko mbele watu wanahiyari wakasema aah! tunataka *private candidate*, maana hawana hiyari hiyo. Kusema kwamba kuanzi sasa tuwe *private candidate.* Nchi nyingi zinafanya. Na mimi naona mwelekeo huko tunakokwenda ni huo vile vile, hata kwa hapa kwetu.

Sasa *private candidate* hana chama. Kwa hivyo inaweza ikajikuta katika …

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Mwanasheria Mkuu ajitahidi sana kuzungumza Kiswahili kwa sababu anazungumza vitu muhimu sana. Kwetu kule Chaani unaposema *private candidate*, wananchi hawajui, mimi nitajua maana yake nishakuja mjini.

Sasa nilikuwa namuomba sana azungumze sana Kiswahili chote.

Mhe. Spika: Lugha ya Baraza ni Kiswahili basi nenda kwenye Kiswahili pale ambapo unabidi unukuu ninadhani utajitahidi kufanya tafsiri. Mwanasheria Mkuu endelea.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, ninashukuru, naona hata hicho Kiswahili Mhe. Hamza huwa analalamika anasema kuwa ninazungumza mafumbo. Sasa nitajitahidi (*Kicheko*).

Mhe. Spika, ninasema kwamba hilo tuzingatie, mimi sitaki kuzungumza habari hii kwa misingi ya kisiasa, ninazungumza kwa misingi ya Kikatiba na misingi ya kisheria, kwamba zipo nchi na katika mchakato huu wananchi hawauzuiliwi pia kusema tunataka mgombea mbinafsi, kwamba badala ya kupitia kwenye chama, unaweza ukaja ukajikuta katika Baraza hili lote, kuanzia Spika mpaka Wajumbe wote hawakutokana na vyama.

Hilo linawezekana na kama linawezekana. Sasa unajiuliza hivyo vyama vilivyotuwekea misimamo, chama kutoa maoni mimi ninadhani ni sawa ni haki yaki kama chombo nacho cha kutoa maoni. Lakini kusema kwamba msimamo, mimi ninadhani hilo si jambo si sawa katika utunzi wa Katiba, sidhani kama ni jambo sawa kwa sababu kama nilivyotangulia kusema kwamba chama nacho kinakuwa kama ni mbuzi wa karamu au kitoweo cha karamu. Sasa kitoweo cha karamu, mbuzi hawezi kumwambia mwenye karamu aah! kamchinje ng'ombe, ana hiyari yake.

Hivi vyote vyama, taasisi, NGOs sijui nini, hizi zote ni sehemu ya taasisi ambazo watu watazitumia katika Katiba. Sasa zenyewe nikasema zinawawekea watu misimamo, ninadhani si sahihi katika utaratibu wa utungaji wa Katiba.

Sasa mimi nilidhani kwamba vyama vingewaachia watu zoezi hili kama vina maelekezo, kama vina maoni vikatoa lakini misimamo mimi ninadhani tutakuwa hatufiki. Mimi hili linanipa wasi wasi kwa sababu moja tu.

Mimi sidhani kwamba kwa bahati mbaya. Linanipa wasi wasi kwa sababu hapa tulipofika katika Katiba tuliyonayo hatukufika Mhe. Spika, kwa bahati mbaya. Na ukitaka kujua kama hatukufika kwa bahati mbaya inabidi usome tokea historia. Ukianza ile Katiba ya mpito ya mwaka 1965, kifungu cha 3 ilikuwa inaeleza kwamba, "Mpaka TANU na Afro-Shirazi vitakapoungana, hiyo ilikuwa ni mwaka 1965, kuwa chama kimoja basi chama kitakachoruhusiwa kwa Tanganyika ni TANU, chama kitakachoruhusiwa kwa Zanzibar ni Afro-Shirazi.

Lakini baadae tumekuja kuwalaumu watu mwaka 1977 kwamba wamekubali kuja kuunganisha vyama. Lakini imeshasemwa kwenye Katiba kwamba huko ndiko tunakoelekea.

La pili Mhe. Spika, ukitizama mambo ambayo yameingizwa kwenye Muungano tuliingia kwenye muungano kwa mkataba. Ndio nasema wanaosema muungano wa mkataba pia nao inabidi ujiulize mkataba wa namna vile vile. Maana na huu tuliingia kwa mkataba lakini baada ya kuingia kwenye mkataba ndio tukaambiwa ile Katiba ya Tanganyika ifanyiwe marekebisho iwe ndio Katiba ya Muungano.

Kilichofanyika yale mambo ya muungano ambayo ndiyo ya msingi tumeungana yamewekwa huko kwenye kifungu cha 85 ambayo ni *interpretation* tu. Yanaingizwa kama kitu kidogo cha mwisho. Maana ile *interpretation* ndiyo yamewekwa huko, maana mambo ya muungano ndio yakatajwa pale kwamba ni hili na hili na hili. Sasa yalipokuwa yanaongezwa

wenzetu hawakupata shida walikuwa wanabadilisha tu kifungu cha *interpretation*, wakaanza 65 likaongezwa moja, ikaja 67 likaongezwa jengine, 68 humo ndio likaja lori zima.

Nasema lori zima kwa sababu ilisema kwamba yanayoongezwa ni pamoja na mambo yote yaliyokuwepo katika jaduweli la 10 la Mkataba wa Afrika Mashariki ambamo kulikuwa na mambo 27. Sasa kama reja reja ilionekana kwamba watachelewa, ikaingizwa sasa kwa lori zima na mengine yalikuwa yameshakuwemo. Mnamo mwaka 73 yakamaliziwa.

Sasa ndio nasema na haya marekebisho ndiyo haya watu wengine wanayosema labda yalikuwa kinyemela kwa sababu kama yameingia kwa mkataba, kifungu muhimu cha mkataba ya Muungano kilikuwa ni kifungu cha 5 ndicho kilichogawana kwamba yepi ya muungano na yepi si ya muungano. Sasa katika hili anapokuja mmoja akalirekebisha bila ya kushauriana, bila ya kuwa na utaratibu tena kwenye kifungu cha *interpretation*. Wakati ule Bunge lilikuaje?

Chini ya kifungu cha 51 yote yalikuwa yanapitishwa kwa *two third majority* ya Wabunge. Bunge lilikuwa lina wabunge 203, katika hao 203 kutoka Zanzibar ni 57. Kwa hivyo haitimii hata hiyo *one third* ya kusema tunapinga hivi, hata kama wengetaka. Na hayo ndiyo mambo ambayo Mhe. Spika, si kwa bahati mbaya ndiyo yakarithiwa katika Katiba hata hiyo ya kudumu. Maana Katiba ya kudumu kitu cha kushangaza ni kwamba sisi tumeungana tuseme kwa hayo mambo 22. Lakini kwa mujibu wa ibara ya 98 yale mambo 22 yatapopitishwa sheria zake yanapitishwa kwa idadi ya wingi wa kura za Wabunge wote.

Watu wengi tunasema aah mambo ya Muungano haya ni kwa theluthi mbili ya huku na huku. Si kweli, yanayopitishwa kwa utaratibu huo ni mambo ambayo yapo katika orodha ya pili jaduweli la pili ambayo ni mambo manane. Katika hayo mambo manane mambo matatu siyo ya Muungano. Lakini haya yote yaliyokuwepo kwenye orodha ya mambo ya Muungano wakitaka kuyatungia sheria, Sheria ya Uraia haipitishwi kwa theluthi mbili ya kura ya Wabunge, yanapitishwa kwa Wingi wa kura za Wabunge. Tujiulize Wabunge waliokuwepo Zanzibar ni wangapi na Wabunge kutoka Bara ni wangapi. Ina maana kwamba umempa mtu mamlaka anageuza anavyotaka, anatengeneza anapotaka, anakata anapotaka, anaongeza anavyotaka. Tujiulize hivyo kweli Muungano umebakia wapi?

Mimi nadhani hizi inabidi zote tuzielewe kwamba hakuna muungano. Muungano *essence* yake ni kwamba kwa yale mliyoungana basi mnakuwa na sauti sawa katika kuyaamua, kisera, kisheria na katika usimamizi.

Mnapokuwa hayo hayapo masharti hayo matatu huo si muungano, muutafutie jina labda muuite.

Jengine ambalo ni jambo la kushangaza kweli kweli tunaambiwa kwamba ule uhalali hata Muungano wenyewe kwa maana ya serikali. Maana wenzetu Mhe. Spika, Wamarekani mimi nilikuwa nawaona ni watu wa ajabu sana. Wamarekani katika mfumo wao wa uchaguzi ndio watu kidogo ndio wanaomchagua Rais. Kila jimbo limepewa kura zake za Uraisi. Mimi nashukuru nilipata fursa ya kwenda kusomea Marekani kuhusiana na mambo ya uendeshaji wa shughuli pamoja na mambo mengine ya muungano wao mwaka 2007. Nikatembea takriban Majimbo yote takriban ya Marekani. Ndio nilipowauliza kuhusu hili. Wakasema utaratibu huu wa uchaguzi unajenga uhalali wa serikali. Uhalali wa Serikali kwa maana gani?

Uhalali wa serikali kwa maana ya kwamba Rais yule wa Marekani kama angelikuwa anachaguliwa kwa wingi wa kura tu, angekwenda katika majimbo yake matano yameshamtosha kupata Uraisi. Asingekwenda Majimbo ambayo yana watu kidogo, asingekwenda mahala kama *Wyoming* ambao ni watu sijui laki 6 au laki 7 na ndio jimbo masikini kabisa. Angelikwenda California kwa sababu ya watu wake wengi na kama ingelikuwa ni nchi peke yake ingelikuwa ni ya saba kwa uchumi imara duniani. Lakini utawakuta wao wana kura zao pengine zinakaribiana pengine na *Wyoming* ambao ni masikini na ni watu wachache.

Sisi leo tunasema tuna Rais wa Muungano katika uchaguzi wetu. Lakini Rais wa Muungano ana haja gani ya kuja Zanzibar kuja kupiga kampeni. Kwa hivyo tunaweza tukafika pahala tukawa na Rais wa Muungano ambaye hakupata hata nusu ya kura Zanzibar, na hata Raisi wa Muungano huo uhalali ataupata wapi?

Unaweza kuwa na chama kikatawala kikawa ndio kinachoendesha muungano, lakini hakikupata hata mguu wa kiti seuze kiti. Lakini ndio kikawa Chama Tawala kinachoendesha Muungano kutokana na mfumo wetu wa uchaguzi. Hiyo ndio unasema una mfumo gani wa muungano, huo muungano uko pahala gani. Ambapo una Raisi hakupata kura hata moja, una chama hakikupata hata kiti kimoja, lakini bado ndio kinachoendesha Serikali ya Muungano. Ndio maana ya serikali mbili.

Naomba watu tuifahamu vizuri. Tukizungumza Serikali mbili maana yake tunalizungumza hilo, hayo yatatufika. Kwa hivyo suala la kuzungumza hapa idadi ya serikali mimi bado nasema sio la msingi. La msingi ni kusema tunataka mfumo, utaratibu gani wa kuendesha muungano.

Jengine naomba nimalizie Mhe. Spika, katika hili mimi nimebahatika kuingia skuli ya Muungano mwaka 19 sasa hivi. Niliteuliwa kuwa Katibu Mkuu na Naibu Mwanasheria Mkuu mwaka 1993 nikiwa bado Othmani kweli kweli. Maana nilikuwa na miaka 30 tu wakati huo. Tokea wakati huo nimekuwa katika takriban mikutano yote Kamati zote. Mwaka 1992 tulikuwa tuna Kamati ya Bomani kabla ya kupitishwa marekebisho ya 11 ya Katiba yaliyomuondoa Rais wa Zanzibar asiwe Makamo.

Ripoti ya Bomani ikaja na pendekezo la kwamba tuurekebishe basi huu mfumo wa serikali mbili ili tuwe na pahala ambapo na hawa Zanzibar nao watapata kuwa na sauti katika kuamua mambo ya Muungano. Lakini mashahidi pengine wamo, ikaambiwa ukifanya hivyo maana yake kwamba unaleta Serikali Tatu.

Nasema huu ni wajibu wetu kusema ukweli kwa yale tunayoyajua katika kipindi hichi. Ni muhimu kwa sababu ndio kujenga misingi imara na sio kuipendelea Zanzibar, kuwa na muungano imara ni kuipendelea Jamhuri ya Muungano yeyote itakayokuwepo. Mimi napata wasi wasi wakati mwengine ninaposikia wenzetu, mpaka juzi karibuni kuna Waziri wa Serikali ya Muungano anasema tukiwa na serikali tatu Tanganyika ndio itabeba mzigo. Mimi angekuwa na sababu nyengine ya msingi ningeweza kuelewa. Napata mashaka mtu anapokuja na hoja hiyo ambaye ni Waziri tena ni Waziri wa Sheria. Sasa hivi nani anayebeba mzigo? Jibu mnalo.

Baadaye mwaka 2001 nadhani wengine ni mashahidi humu ndani, mimi binafsi yangu nilikuwa ni Mwenyekiti wa Kamati ya Wataalamu ambao tulipitia kero za Muungano na kupendekeza muundo mzuri katika mfumo huu wa Serikali Mbili. Tukapendekeza kuwa na Bunge la Muungano ambalo lina Bunge la Juu, Kuwa na Mabunge mawili ndani ya Moja kama mfumo wa wenzetu ulivyo. Jibu likawa ndio lile lile, ukisema hivyo maana yake ndio unakuwa na Serikali Tatu.

Hii ni kusema je, mfumo wa Serikali mbili wenyewe umeshafika pahala hauwezi kubadilika. Sasa kama hauwezi kubadilika, unasema kitu tunakitetea wazungu wanasema kama kimejaribiwa na kuthibitishwa kwamba hichi kinafaa. Mimi nasema wasi wasi wangu ni kwamba matatizo mengi yametokea katika Muungano kwa sababu tumefungiwa kwenye boksi ukitaka kuvuta pumzi shida, ukitaka kuchungulia nje shida. Kwa sababu tumejifunga kwenye muungano wa mfumo na kwamba muungano maana yake ni mfumo huu.

Mimi nasema katika mchakato huu hebu tutoke kwenye boksi kama baadaye tutaona kama hizo serikali mbili au tatu au nne au tano ndio muwafaka basi

tutasema, kwamba jamani hizi ndio muafaka lakini kwa sababu, kwa hoja, kwa misingi. Kama ni kusema kwamba nitoe wasia wangu basi ungekuwa ni huo, kwamba jamani tutoke kwenye boksi maana humu ndio tunamopata shida. Tumefika hapa kwa sababu tumekuwa kwenye hili boksi kwa muda mrefu.

Mhe. Spika, mimi nasema kwa kumalizia nchi yoyote, muungano wowote ambao haukujenga misingi basi tusijidanganye kwamba aah Muungano umedumu muda mrefu, hauwezi kuvunjika. Si kweli, kama hauna misingi madhubuti Mhe. Spika, utavunjika, usingevunjika Muungano wa Ireland na Uingereza maana ulifanywa mwaka 1800, wakajitoa majimbo 26 mwaka 1922 baada ya miaka mingapi hiyo, miye sijui hesabu. Sasa hao ndio usingevunjia basi eti. Lakini ambalo nikumbushe kwamba bila ya misingi unaweza kuwa na jambo likavunjika. Watu wenyewe wakasema hili bwana halitufai. Na hili naomba mimi nikumbushe, maana historia tunaambiwa ndiyo hiyo ya kutukumbusha.

Kuna bwana mmoja maarufu anaitwa *Simon Bolivar*. Alikuwa ndio wanamwita mkombozi wa Amerika ya Kusini maana kapigana vita kaikomboa Ecuador, kawakomboa Peru, kakomboa Venezuela, nchi karibu 6. Lakini alipomaliza kazi yeye bwana na udogo wake, *interest* yake ilikuwa ni katika kujifunza namna gani ya kuendesha serikali. Kahama kwao akenda Ufaransa kwa shida lakini aende akajifunze namna gani ya kuendesha serikali. Moja anasema mwenyewe alilojifunza Ufaransa ni Mapinduzi ya Uingereza.

Waingereza walipindua mwaka 1649, chini ya kiongozi wao Oliva Kromuel, wakadumu na mapinduzi yale wakesha akaondolewa Mfalme. Wakaanzisha *Republican Form of Government,* Oliva Kromuel akafa mwaka 1658 bada ya miaka 9. Kafa mwaka 1658 Waingereza mwaka 1660 baada ya miaka miwili tu wakenda wakamtafuta Mfalme aliko Ufaransa arudi awatawale. Kwa sababu *Oliver Cromwell* hakuanzisha misingi imara ya *Republican form of Government,* ndio maana Waingereza wakarudi katika mfumo wa Ufalme. Hilo anasema ndio moja nililojifunza. Na yeye baada ya kumaliza kazi yake akapewa heshma ya kulihutubia Bunge la Venezuela tarehe 15 Februari mwaka 1819.

Akasema,

> "Nyinyi Wabunge ndio wenye dhamana ya nchi, sisi tumepindua, sisi tumekomboa, lakini nyinyi ndio wenye dhamana ya nchi. Nawaomba muipe nchi hii serikali iliyotulia. Serikali inayojali haki, serikali inayojali watu, serikali itakayoendeleza matunda ya Mapinduzi, serikali ambayo itakuwa inaweza ikaleta amani na utulivu. Akamalizia kuwambia mimi nimeshamaliza kazi yangu na anzeni kazi yenu"

Ndivyo alivyowambia, na hayo hakuyasema juzi wala jana, kawambia mwaka 1819 tarehe 15 Februari. Alichosema ni kwamba lazima nchi iweke misingi imara ya kuendesha nchi. Vyenginevyo hatuwezi kwenda.

Mhe. Spika, mimi naomba niwatanabahishe wenzangu kwamba boksi, mfuko, mkoba huu utatudhuru. Tusimamishe tutafute misingi ya muungano, na tuisimamie hiyo na tuitetee hiyo, tuhakikishe kwamba hiyo imepatikana, ndio muungano wetu utakuwa na salama na ndio muungano wetu utadumu. Sio kwa njia nyengine, sidhani kama kuna njia nyengine mbadala zaidi ya hiyo kwa kweli.

Mimi nimefurahi kusikia kwamba nimepata fununu kwamba Waheshimiwa Wajumbe hapa watafundwa zaidi, watapatiwa zaidi mambo hayo. Kwa kweli nashukuru sana na Mwenyezi Mungu ajaalie jambo hilo lifanikiwe.

Mwisho baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naomba kukushukuru sana kwa kunivumilia, lakini niwaombe Waheshimiwa Wajumbe muipitishe hoja hii bila ya buti, na leo kuna Mufti wengi kule juu, Mashekhe kwa heshima yao na kwa heshima ya Waziri basi muipitishe bila ya shida. Mhe. Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana

Mhe. Spika: Mhe. Mwanasheria Mkuu tunakushukuru, hotuba yako leo imetimiza Kanuni ya kutumia dakika 30 na nyongeza 10 na 10 nyengine nikakuongezea, kwa sababu ya umuhimu wa mambo ambayo umeyazungumza. Baada ya hayo, sasa naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, ili niweze kutoa majumuisho ambayo yametolewa na Wajumbe Wawakilishi kwa muda wa siku mbili.

Mhe. Spika, kwanza napenda nitoe shukurani zangu za dhati kwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu ambao walichangia hotuba yetu na shukurani hizi ni kwa sababu mbili. Kwanza michango yao takriban mingi ilikuwa ni michango ambayo inasaidia wizara yetu. Pili ilikuwa ni michango ambayo inaturekebisha pale ambapo tumekosea.

Vile vile Waheshimiwa Wajumbe walitoa pongezi sana kwangu mimi pamoja na wafanyakazi wangu wote. Kwa hivyo, kwa niaba yao na mimi naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa maelezo yao hayo pamoja na michango yao.

Mhe. Spika, hotuba yetu ilichangiwa na Waheshimiwa Wajumbe 21 ambao hawa walichangia kwa kuzungumza na kuna Wajumbe 7 walitoa michango yao kwa maandishi.

Mhe. Spika, nichukue nafasi hii kuwajata Wajumbe waliochangia kwa kusema kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Wanu Hafidh Ameir

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk,

Mhe. Abdalla Juma Abdalla,

Mhe. Ismail Jussa Ladhu

Mhe. Subeit Khamis Faki

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa

Mhe. Suleiman Hemed Khamis

Mhe. Rashid Seif Suleiman

Mhe. Asha Bakari Makame

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali

Mhe. Mussa Ali Hassan

Mhe. Mansoor Yussuf Himid

Mhe. Saleh Nassor Juma

Mhe. Salmin Awadh Salmin

Mhe. Hamza Hassan Juma

Mhe. Hija Hassan Hija

Mhe. Jaku Hashim Ayoub

Mhe. Omar Ali Shehe

Mhe. Ali Mzee Ali

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad

Mhe. Abdalla Moh'd Ali

Mhe. Spika, kwa upande wa waliochangia kwa maandishi ni Waheshimiwa Wajumbe 7, naomba niwataje kama hivi ifuatavyo:-

1. Mhe. Ismail Jussa Ladhu

2. Mhe. Asha Abdu Haji

3. Mhe. Salma Mussa Bilali

4. Mhe. Bikame Yussuf Hamad

5. Mhe. Fatma Mbarouk Said

6. Mhe. Ashura Sharif Ali

7. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi

Mhe. Spika, michango yote hii ambayo imezungumzwa. Kwa kweli kulikuwa na mambo 6 ambayo ndio mambo yaliyojadiliwa. Jambo la kwanza katika maelezo yao na Waheshimiwa Wajumbe wengi, walizungumzia kuhusu upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa, kwa nini watu wanaopindukia umri vyeti vyao hawapati, na zaidi wakasema kwamba kuna watu hivi sasa katika ule utaratibu wa utoaji wa vyeti umekuwa na urasimu mkubwa sana hali ya kwamba vyeti vyao hawavipati.

Mhe. Spika, suala hili la vyeti kama tulivyolizungumza kwenye hotuba yetu, ni kweli tulisema kwamba utoaji wa vyeti vya kuzaliwa hapo mwanzo ulikuwa na matatizo katika sehemu mbali mbali.

Kwanza tulisema matatizo haya mbali ya kuanza ofisini kwetu, pia yalikuwa yako katika wilaya. Sasa baada ya kufanya utafiti na kufuatilia kwa kina kabisa, tukagundua kwamba katika Wilaya zote za Unguja na Pemba kulikuwa na vyeti takriban karibu 10,000 ambavyo bado havijachukuliwa au hawajavipata wenyewe.

Mhe. Spika, hali hii utakumbuka katika kipindi cha Baraza lililopita, lilikuja swali kuhusu jambo hili, na mimi niliahidi kulifanyia kazi na tutalikamilisha. Kwa kweli nina furaha kusema kama nilivyosema kwenye hotuba yangu kwamba utaratibu huu sasa tumeukamilisha.

Vile vile kama watu wanajaribu kusikiliza redio na kuangalia *television* tulitoa matangazo kiasi wiki mbili nyuma, kwamba vyeti hivi sasa viko tayari

na watu wote wanaombwa kwenda kuchukua vyeti vyao, kwa bahati mbaya Mhe. Spika, kwamba watu bado hawajaitikia wito huo.

Kwa hivyo, hivi sasa ninavyozungumza tunavyo vyeti ambavyo kwa Wilaya ya Mjini na Wilaya ya Magharib, yaani Mkoa wa Mjini Magharibi kuna idadi ya vyeti 5,553, ambavyo tayari vimeshatiwa saini na viko tayari kwa ajili ya kuchukua wenyewe, lakini bado hawajenda kuvichukua.

Kwa upande wa Wilaya ya Kati kuna vyeti 20, Wilaya ya Kaskazini "A" kuna vyeti 775, Wilaya ya Kaskazini "B" kuna vyeti 55 na Wilaya ya Kusini kuna vyeti 27. Mhe. Spika, hivi ni vyeti ambavyo tayari tumeshavikamilisha na kuvitia saini na vinasubiri wenyewe kwenda kuvichukua. Kutokana na hali hiyo, naomba sana wananchi wetu waende katika maeneo yanayohusika kwa ajili ya kwenda kuchukua vyeti vyao.

Kwa upande wa Pemba Mhe. Spika, Wilaya ya Wete kuna vyeti 758, Wilaya ya Chake-Chake kuna 621, Wilaya ya Mkoani kuna vyeti 1,057 na Wilaya ya Micheweni kuna vyeti 709. Kwa hivyo, suala hili la vyeti Mhe. Spika, kwa kweli lilikuwa na matatizo, lakini sasa nakuhakikishieni kwamba matatizo hayo yameondoka na ndio maana hivi sasa bado tunapiga kelele na tunasisitiza kwamba wale wote ambao hawajapata vyeti vyao basi tafadhalini nendeni mkachukue vyeti vyenu maeneo ambayo yanahusika.

Suala la *late registration* hili kweli linamatatizo na lazima tuwe wagumu kidogo. Maana tumegundua kwamba kwa kutumia *late registration* kuna mambo matatu yanayotokea.

Kwanza kuna watu ambao sio Wazanzibari wanajaza hizi fomu wanakwenda kwa Masheha na kupitia maeneo hayo zinaletwa fomu zimeshakuwa *sign* kama mtu ameshatoa chochote kule, halafu sisi tunatoa cheti cha kuzaliwa kwamba yeye ni Mzanzibari hapa kumbe mtu yule si Mzanzibari wala hakuzaliwa Zanzibar. Kama inatokea matatizo kama haya lazima tuwe *serious* kidogo ili tuzuie udanganyifu huu. Kwa sababu unapotoa vyeti aina hii baadaye tunaweza tukapata sisi wenyewe tukamchagua mtu hapa kuwa Rais kumbe ni Mkenya au kumbe ni mtu kutoka sehemu nyengine. Kwa hivyo hilo ni tatizo moja.

Lakini la pili tumegundua kwamba hasa katika vijana wetu hawa, wanapotaka kuajiriwa kwa mfano kwenye jeshi au kwenye polisi wanaambiwa umri usiozidi miaka 22 kwa mfano. Lakini yeye umri wake ni miaka 25, kwa hivyo anachokimbilia anafanya *late registration* kuonesha kwamba umri wake sasa ni miaka 21 na hizo zipo nyingi. Hiyo nayo imetufanya kidogo tuwe *very serious* katika kufanya au kutafiti mtu ambaye ana *apply late registration*.

Lakini hata hivyo Mhe. Spika, tumejaribu kupunguza masharti ni tofauti na yale masharti ambayo yalikuwepo zamani. Lakini hata kama tumepunguza masharti lakini bado tuna *scrutinize* sana ili mtu ambaye anapewa cheti cha *late registration* anakuwa kweli anahusika na *late registration*. Tatizo jengine ambalo lilizungumzwa au lilokuwepo zamani ni kwamba hawa kutoka Pemba ilikuwa *late registration,* Pemba huwezi kupata lazima utoke Pemba uje Unguja na ukija Unguja unakaa wiki mbili pengine unarudishwa kutokana na fomu ile haikujazwa vizuri, mtu anapata shida anakwenda anarudi, anakwenda anarudi.

Tukaamua na huu ndio msimamo ambao upo hivi sasa ni kwamba mtu yoyote anaye *apply late registration* kutoka Pemba hatakiwi tena aje Unguja. Anachofanya anakwenda Wete Afisi yetu pale, anajaza fomu, kuna watu maalum. Wanaomjazia na utaratibu wote unakamilika kule halafu Afisi wetu kutoka Pemba analeta fomu zile zinashughulikiwa na baadaye vyeti vyake vinapelekwa Pemba. Kwa hivyo ule utaratibu wa mtu kutoka Pemba kuja huku sasa umemalizika.

Mhe. Spika, kwa maana hiyo basi, napenda niseme kwamba utaratibu huu hivi sasa ndio unaofanyika. Hivi juzi tulijaribu kuzungumza na wafadhili au maendeleao na tukaanza kufanya mradi ambao kama tutafanikiwa tumefanya kama *pilot project* tukifanikiwa basi inaweza ikapunguza sana upatikanaji wa vyeti kwa urahisi. Mradi ule ambao hivi sasa tumefanya ni *pilot project* kwa Mkoa wa Mjini Magharibi. Kwa mfano mtu amezaliwa hospitali baada ya hospitali kutuletea *retuns* katika hospitali yetu. Utaratibu umeandaliwa kwamba *returns* zile zinakuwa *computerised* katika *system* maalum ambayo cheti chake anaweza akapata ama siku ile ile anapopeleka ile *returns* au kwa kuchelewa ni siku ya pili.

Hii tumeshaanza kwa Mkoa wa Mjini Magharibi na itaanza rasmi Julai mwaka huu. Ninachoomba kwamba tutizameni mfumo huu ambapo naamini utasaidia sana watu wetu kupata vyeti vyao kwa haraka zaidi. Ile *system* ya kusema kwamba vyeti sasa vinapigwa katika *type writer* za zamani, yote hii imekuwa *technical consideration* na utaratibu huu sasa utafanya vile vyetu tuvione vizuri sana.

Mhe. Spika, baada ya kuzungumza hilo katika suala la vyeti naomba sasa nizungumzie suala la Mahakama. Kwa kwali nashukuru wachangiaji wengi walizungumza suala hili na wakatoa maelekezo yao na muongozo wao ambao yote tutayachukua kwa kuyafanyia kazi. Lakini kuna masuala ambayo yalizungumzwa napenda kidogo niyazungumze.

Kwanza Mhe. Salmini hasa alisema kwamba hawa Mahakimu wameshapata nyongeza ya mshahara, wameshapata kila kitu kwa nini kesi zinachelewa. Ni kweli Mahakimu wamepata nyongeza, lakini suala la ucheleweshwaji wa kesi halipo Mahakamani peke yake. Kesi ina mikono mingi, kesi ipo Mahakamani, kesi ipo kwa Mkurugenzi wa Mashtaka, kesi ipo kwa polisi, kesi ipo kwa jamii. Mambo yote manne haya basi haya ndiyo yanayofanye kesi yende haraka au isinde haraka si Mahakama peke yake.

Kwa mfano kesi inaweza ikawa ipo Mahakamani, lakini ushahidi haujakamilika, hatuwezi kumlaumu polisi. Kwa sababu polisi anapoita watu kuwahoji, jamii yetu nayo ina matatizo, anasema hayo anamuachia Mungu tu basi kwa hivyo ushahidi hatoi. Kwa hivyo mahakamani sisi hatuwezi kumuhukumu mtu ikiwa hatuna ushahidi wa kutosha.

Kwa mfano unaweza ukapeleka kesi ambayo inataka uchunguzi fulani, uchunguzi ule upo kwa Mkemia Mkuu, Mkemia Mkuu bado hajamaliza mfano mchele ni mbovu au mambo kama hayo. Sasa kama Mkemia Mkuu hajamaliza uchunguzi wake Mahakama haiwezi kutoa adhabu au kutoa hukumu. Kwa hivyo vikundi hivi au watu hawa ambao wote kwa pamoja ndio wanaoweza kuendesha kesi.

Nakubali kwamba kesi zinachelewa wakati mwengine sana na kutokana na hayo hivi karibuni tulikutana na vyombo vyote ambavyo vinahusu uendeshaji wa kesi, Mahakama, Polisi, Mwanasheria Mkuu, DPP, Mkemia Mkuu, wote hawa tukaa pamoja na kujaribu kujiuliza tufanye nini ili kesi angalau tuweze kuzipeleka haraka.

Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako kwamba tumekubaliana baadhi ya mambo ambayo naamini yatasaidia sana katika kupeleka kesi zetu kuzifanya haraka haraka. Hata suala la kesi ambazo zinachelewa zile za Mahabusu au kutoka Chuo cha Mafunzo. Yote hayo tuliyazungumza na kuona kwamba matatizo kwa mfano kwa watu wetu ambao wapo katika vyuo vya mafunzo pengine kuna matatizo ya upotevu wa mafaili au pengine faili halionekani. Matatizo kama haya yote tuliyazungumza na tukahakikisha kwamba tumeweka system ambayo haya yote yanatizamwa kwa kila mwezi, Kamati hii ambayo nimeizungumza ya kuharakisha kesi inakutana kutizama na kujadili kweli kama kesi zinakwenda au zinachelewa na kwa misingi gani.

Suala la pili ambalo lilizungumzwa ni suala la Jaji Mkaazi Pemba. Mhe. Spika, kama wewe ni shahidi basi utakuwa ni shahidi kwamba suala hili hata mimi binafsi nililizungumza sana katika vipindi vilivyopita. Kwa nini hatuwi na Jaji Mkaazi Pemba. Nilikuwa nasema hivyo kwa sababu ya kesi ambazo

tulikuwa tunahisi kule ziko, lakini wakati ule kesi zilizokuwepo tulikuwa tuna matatizo mawili makubwa.

Kwanza kulikuwa kuna mrundikano mkubwa wa kesi za rufaa, lakini pia ule uwendaji wa Mahakimu au wa Majaji Pemba ulikuwa haupo. Kwa mfano Jaji anaweza akakaa miezi sita au zaidi bado hajenda Pemba. Kwa hivyo bila shaka kesi zile zitarundikana. Kwa hivyo matokeo yake utaona kesi zile ni nyingi sana.

Lakini la pili Mhe. Spika, baada ya kuyatizama haya na lile lengo la kusema tupeleke Jaji Mkaazi Pemba itabidi tutizame *cost wise* je kuna uhalali kwa hivi sasa kupeleja Jaji Mkazi Pemba. Tumechukua *statistics* za kesi zote zilizokuwepo Pemba hivi sasa baada ya Majaji kwenda Pemba kwa kipindi kilichopita na kumaliza kesi hizi za rufaa na kesi nyingi ambazo zilikuwepo. Kesi za jinai zilizokuwepo Pemba ni 9 na kesi hizi ambazo Jaji anatakiwa azishughulikie. Moja ya kesi hii ilifunguliwa tokea mwaka 2006 na nyengine ilifunguliwa 2008 mbili 2010 na tatu 2011 na mbili 2012.

Mhe. Spika, kwa kweli kumpeleka Jaji Mkaazi Pemba akishakukaa kule Pemba akashughulikia kesi 9 tu, kwa kweli tutaonekana hatukufanya kitu cha maana na haiwezekani. Kwa sababu ile gharama ya kukaa kule kwa kusikiliza kesi tisa mwaka mzima itakuwa haiwezikani. Kwa hivyo Jaji huyu ni bora kumtumia hapa ambapo panamrudikano wa kesi. Pale ambapo kesi zinatokea ndio pale kila mara Jaji mmoja anakwenda ku – *clear* zile kesi mbili au kesi tatu.

Lakini wengine wakasema je, kumpeleka Jaji Pemba na kumuweka kule si gharama bora vile kumpeleka Pemba kuliko kuliko kumuweka kule kule. Si gharama kwa sababu gharama ya kumpeleka Jaji Pemba kusikiliza kesi zile mbili au tatu zilizopo kwa wingi inachukua shilingi laki 7 au 7.5, kwa mwezi na ukimuweka Jaji pale gharama ambazo zitapatikana karibu ni milioni 2. Nimefanya hesabu hiyo kwa hivyo *cost wise* ile ni bora kwenda akarudi na anarudi huku kufanya au kushughulikia kesi nyengine.

Mhe. Spika, mbali na kesi hizo kwa mfano kuna kesi za madai vile vile ni tisa. Kesi za rufaa zilizopo hivi sasa ni kesi 5. Kwa hivyo hizi zote Mhe. Spika, hazikidhi kumpeleka Jaji akawa ni Jaji mkaazi kwa Pemba.

Mhe. Spika, nawaahidi pale ambapo kesi zitakuwa ni nyingi na mimi upande mmoja naomba zisiwe nyingi kwa sababu kule itakuwa watu hawana *commonality* kubwa. Lakini kila zikiwa nyingi ndio *commonality* inazidi sasa kama kesi ni kidogo ina maana kwamba ile *society* ni bado ni nzuri na

inajiheshimu katika mambo haya. Lakini hapo ambapo kesi zitakuwa nyingi basi naahidi kwamba Jaji Mkaazi Pemba tutampeleka.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo lilizungumzwa katika suala la Mahakama ni kwamba je, tutumie utaratibu gani kuhakikisha kwamba maamuzi yanatolewa haraka. Hili nimeshalizungumza kwa sababu uamuzi kutolewa katika kesi katika Mahakama haraka inategemea vyombo hivi vyengine navyo ikiwa vitajitahidi katika masuala mengine, Mahakama itakuwa haina sababu kwa nini kesi haihukumiwi haraka haraka, ikiwa mashahidi wapo, ikiwa muendesha mashtaka yupo, ikiwa polisi yupo, Jaji lazima atasikiliza kesi.

Lakini unaweza ukenda katika kesi muendesha mashtaka hayupo, unaweza ukenda katika kesi shahidi hakuja au hataki kuja. Kwa hivyo yote hayo ni mambo yanayochelewesha uendeshaji wa kesi zetu. Tujue tu kwamba kuna sheria ambayo inasema kwamba ikifika siku 60 kwa mfano basi kesi ile inaweza ikafutwa kwa misingi ya kwamba ushahidi ukipatikana inaweza ikaitwa tena kesi ile.

Mhe. Spika, kuna suala ambalo lilizungumzwa kwamba ni kesi ngapi za waliotaka kuolewa Mahakamani zilifunguliwa na ngapi walioozeshwa na wangapi hawajaozeshwa. Ni kesi zinazohusiana na Makadhi, naomba nitalizungumza baadaye. Lakini kuna suala moja ambalo ni kubwa na naomba nilizungumze kidogo kwa kuchukua nafasi. Ni suala la Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, kwa nini hawajapata mishahara ya nyongeza ambayo Mhe. Rais au Serikali ilitoa.

Mhe. Spika, ni kweli Mahakimu wa Mwanzo hawajapata nyongeza. Si kwamba wamedharauliwa. Tatizo lililotokea ni kwamba katika utaratibu ule wa utoaji wa nyongeza za mshahara na haya ndio matatizo ya hizi ITs zetu, ITs ukizi *feed* kwa mtu Mwenye digirii kwa mfano mshahara wake uwe huu kwa hivyo wale na Mahakama ya Mwanzo ina Mahakimu wa aina tatu. Kuna hakimu mwenye cheti, kuna hakimu mwenye diploma na kuna hakimu mwenye digrii, wote ni Mahakimu wa Wilaya ya mwanzo.

Kwa hivyo uki-*compute* pale hakimpi mwenye digrii mshahara wake utakuwa shilingi laki nne sawa sawa na mwenye digrii mwengine. Mwenye diploma itakuwa pengine shilingi laki tatu, sawa sawa na mwenye diploma mwenye shughuli nyengine na mwenye cheti mshahara wake utakuwa shilingi laki mbili kwa mfano na kidogo sawa sawa na mwenye *certificate*. Kwa hiyo utaratibu ule ukasoma vile na watu wakaanza kulipwa na ikaonekana kwa wakati ule pengine hakimu huyu kazidi. Sasa hilo lilikuwa ni tatizo.

Mimi nakubali na ndio maana tukaliendea mbio mpaka hivi sasa tumefika pahala pazuri. Baada ya kuonekana hayo hatukukaa kimya tukasema suala la Mahakimu wa mwanzo ni suala ambalo ni tofauti na mtu mwenye *certificate* au mwenye diploma au mwenye digirii. Kwa sababu ule ni ujuzi maalum na kuna watu wale hakimu, jaji, hakimu wa Mkoa, hakimu wa Wilaya, na kula wale. Hakimu wa Mkoa na Hakimu wa Wilaya hawa wako katika kada nyengine. Lakini na hawa ni Mahakimu kwa hivyo mshahara usiegemee katika *certificate* yake au katika diploma yake au katika digirii yake, hivyo tutakuwa tumekosea. Mshahara u–*base* katika ule ujuzi ambao anatakiwa aufanye na ujuzi wake ule ni uhakimu.

Suala hili tulikuwa tunabadilishana mawazo sisi na Wizara ya Utumishi. Lakini kwa sababu ule muda kidogo ulikuwa mkubwa, Utumishi wakasema hebu tutoweni hili posho kwanza. Likatolewa posho kwa kila hakimu nafikiri shilingi laki nne na kidogo mbali na ule mshahara wake ule ule aliokuwa anapata. Posho hili lililotolewa tukasema hili posho hata kama limetolewa lakini bado ule mshahara bado hatujauweka. Lazima tu-*base* katika mshahara kwa sababu mshahara baadaye utachukua mambo mengi.

Mhe. Spika, tukazungumza suala hili na kwa bahati ikaja ile siku ya *law day* tukam- *brief* Mhe. Rais na Mhe. Rais akakubali, tukazungumza na Wizara ya Utumishi, tukakubaliana kwamba sasa tujaribu kuweka ile *format* ya chanzio cha mshahara wa hakimu wa Mahakama ya Mwanzo, *irrespective* kwamba yeye ana digrii ana diploma au ana *certificate*. Hapo ndipo tulipofika na hayo ndiyo tuliyokubaliana na hayo yapo tayari kuchukuliwa hatua. Baada ya kufika hapa mimi binafsi niliwaita Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo nikawaelezea haya na tukakubaliana.

Mimi sioni kama kuna tatizo lolote, kitu ambacho nakubali kwamba tumeshelewa lakini hata kuchelewa, hichi kitu kimeshafanyika au kitafanyika katika utaratibu huo, mimi nikawaomba wastahamili tukimaliza hii bajeti suala hili litamalizika. Kukawa na suala la *arrears* zao. Yote hayo si kwamba tumenyamaza kimya, tukazungumza. Kwa sababu *arrears* hizi mimi binafsi naona kwamba mshahara kwa mfano Mhe. Rais alisema mshahara uanze Oktoba, wale vijana wetu bado hawajapata mshahara wao. Hakuna sababu kwa nini wasipewe *arrears* zao.

Mhe. Spika, mimi sioni sababu kwamba hili ni tatizo, tatizo lipo kwamba wamechelewa lakini kuchelewa ndio *system* ya Serikali. Katika jambo ambalo kwa nchi nzima wanalifanya lazima kutakuwa na wengine kidogo watasahauliwa, wengine watafanywa hivi lakini marekebisho yao yanakuja. Kwa hivyo hilo ndio jibu ambalo naweza nikalisema kwa uhakika.

Hapa naomba Mhe. Salmini Awadh nimjibu katika lile swali lake alilosema kwamba kuna fedha zimepanda sana kutoka shilingi milioni 50 mapaka shilingi milioni 400 na kidogo. Ni kweli ni kutokana na sababu hiyo hizi fedha ni posho la hao Mahakimu pamoja na posho la Mahakimu wa Wilaya na Mahakimu wa Mwanzo na Masekreteri. Mahakimu wa Mkoa kwa mfano wapo wanane, kuna posho la mafuta la kila mmoja. Hili posho la mafuta ukizidisha mara 8 halafu zidisha mara 12, Mahakimu wa Mahakama wa Wilaya hivyo hivyo kuna posho la mafuta, hawa wapo 14 ukizidisha posho la mafuta mara 14 mara 12, makaazi, kuna Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo 13, ambao hawa ni hilo posho ambalo nilisema wamepewa zidisha mara 13 kwa mwezi, zidisha mara 12. Halafu ukiacha Jaji Mkuu posho lake, ukiacha matarishi hawa 32, ukiacha makarani hawa. Sasa hili posho lote ukipiga total linakuja katika *figure* hiyo. Kwa hivyo hizi pesa hazikuzidishwa kwa sababu ya kuzidishwa tu, zimezidishwa kwa misingi hiyo, kutoka milioni 50 na kwenda milioni 400 na kidogo.

Mhe. Salmin naomba nielezee hivyo katika suala hilo. Mhe. Spika, nije katika suala ambalo dada yangu Mhe. Asha Bakari alilizungumza. Mhe. Asha Bakari namshukuru sana kabisa. Na mimi sina jibu la kumjibu isipokuwa nikumwambia kwamba namshukuru. Kwa sababu maelezo yote aliyoeleza yamenisaidia mimi na Wizara yangu na watendaji wangu kuwa *very serious* katika masuala ya Wakfu na Mali ya Amana. Haya tulikuwa tunayafanyia kazi, lakini matatizo ya watu wetu Mhe. Spika, ni kwamba wanahisi kama kwamba sisi kwamba tunawaonea, tunawapandishia zile bei, au tunafanya mambo kama hayo kwa wingi. Lakini Mhe. Asha Bakari ameelezea vizuri na mimi namshukuru. Amenipa kisu na kisu kile nilikuwa nacho lakini kilikuwa ni kibutu, lakini kakinowa kanipa na nyama *Inshallah* nitaikata vizuri.

Mhe. Bi Mwajuma Faki Mdachi, yeye alizungumzia suala la wanaume ambao wanaoa wake wanne au watatu lakini hawa wawili au mmoja hawajulikani na familia nyengine. Sasa huyu mwanamme akifariki vipi mirathi itakwenda kwa wale watoto wa yule mke ambaye hajulikani.

Mimi nafikiri jibu si gumu, ni kwamba inapotokea hivyo, kwanza tujue mwanamme atabeba jukumu ikiwa anaficha na jukumu hilo atajibu mwenyewe kesho tukenda tukijaaliwa. Lakini la pili huyo mwanamke ambaye anapata hilo basi Mahakama zetu zipo, atakwenda na ushahidi wake na Mahakama za Kadhi zitaamua. Ndio maana ya kuwekwa Mahakama za Kadhi. Sasa naomba linapotokea hilo basi Mahakama zetu tuzitumie naamini Mahakimu wetu watalishughulikia vizuri ipasavyo.

Lakini kuna suala jengine ambalo Mhe. Ismail Jussa Ladhu alilizungumza suala la Wakfu wa Sharifa bint Suleiman bin Masoud. Hii ni nyumba ambayo

Wizara ya Mawasiliano imekodi kama ni Wizara yake. Ni kweli nyumba hii au Wizara ya Mawasiliano inadaiwa hivi sasa milioni 36 za kodi.

Ni kweli kwamba kulikuwa kuna matatizo ya utekelezaji wa ule wasia uliowekwa. Baada ya kuona madeni haya Wizara ya Mawasiliano tulikaa pamoja na Kamisheni ya Wakfu, tukalijadili hili na tumekubaliana. Hivi sasa tunashukuru Wizara ya Mawasiliano kwamba kila mwezi wanatulipa milioni 5 kwa kila mwezi, fedha hizi tunazozipata ndio tumo katika kutekeleza huo wasia aliouwacha marehemu Bi Sharifa bint Suleiman bin Masoud. Tatizo lilikuwepo na lipo kwa sababu hili deni bado halijakamilika, lakini kwa makubaliano hayo. Fedha ambazo tunapata tunajaribu kuzitekelezea huo wasia ambao umewekwa.

Mhe. Rashid Seif, naweza nikasema tu kwamba Kamisheni ina lengo la kuanzisha *data base* na imeshaanza, hivi sasa tunayo kidogo lakini tunaendeleza kufanya hizo *data base* ambazo itasaidisa sana katika shughuli za mirathi zaka na sadaka, hija pamoja na shughuli nyengine. Tayari hatua za awali tumeshaanza kuchukua. Hata katika hotuba yetu tumeeleza hayo na tutaendelea. Kwa sababu masuala haya tumeanza hivi karibuni lakini tunaendelea ili tuweze kupata *complete data base* ya shughuli hizi.

Kuna suala la Mhe. Makame Mshimba, mirathi ya marehemu Fatma Makame Mkombe. Mhe. Spika, tatizo hili ni kubwa kidogo, lakini kwa kweli linatokana na warithi wenyewe. Mirathi hii ya marehemu Fatma Makame alifariki 2004, lakini mirathi ilifunguliwa kupitia Sheha wa Kwahani tarehe 19/9/2005. Warithi walioripotiwa ni mume, watoto wanaume watano, wakike watatu. Mali alizowacha ni nyumba mbili ambazo zipo Mbuyu Pacha na Kilimani na Shamba mbili zipo Mchangani na Kinduni.

Maelezo ya awali yaliyochukuliwa kutoka kwa ndugu Saleh Mohammed Juma, kwamba marehemu amewacha nyumba ambayo ni ya shirika yeye na ndugu yake ambaye ni Bi Mwajuma Makame. Kwa hivyo mirathi hii ilikuwa ina watu wawili sasa, ndugu yake Bi Mwajuma Makame na yeye alipendekeza nyumba zigaiwe na kila mmoja apewe nyumba yake yaani huyu aliyefariki na huyu Bi Mwajuma.

Mhe. Spika, sasa wakafika warithi wa Bi Fatma, wanaume watano na wanawake watatu pamoja na Bi Mwajuma huyu mwenye urithi wa ushirikiano. Walipotoa maelezo ya awali walikubali kwamba mali zigaiwe baada ya kutiwa thamani na dalali wa Serikali. Baada ya hapo walikubaliana Bi Mwajuma apewe nyumba ya Kilimani na warithi wa Bi Fatma wapewe Mbuyupacha na Shamba zote zikatiwe thamani ikisha zigaiwe.

Mhe. Spika, lilotokea baadae, baada ya kutumwa barua kwa hawa warithi za wito, mara nyingi ile mirathi ikamilishwe na Bi Mwajuma apate haki yake lakini warithi hao hawakufika. Wakati huo Sheria ilikuwa haimpi mamlaka Katibu Mtendaji kumlazimisha mtu afike ofisini. Kipindi hicho, lakini baada ya kufanyiwa sheria hii kubadilishwa Katibu Mtendaji sasa ana mamlaka ya kumwita mtu yeyote kwamba afike ofisini. Lakini kipindi hicho kila wakiitwa hawa warithi hawataki. Sasa kama mtu hataki kuja unamwita haji, hatuwezi kurithisha.

Tunawaomba hata leo waende tutawarithisha lakini ni matatizo yao wenyewe sio matatizo ya Ofisi yetu. Leo wakenda au kesho wakenda nawahakikishieni kwamba tutawarithisha. Lakini ni lazima waheshimu mwito, sasa wengine hawaheshimu mwito. Wakishakuona kwamba wao wameshakubaliana huku basi, kwa hivyo hilo ni tatizo Mhe. Spika, na kwa kutumia nafasi hii naomba si kwa warathi hawa tu lakini hili ni tatizo kwa warathi wengi kwamba wanapoitwa hawendi.

Lililojitokeza jengine ni kwamba hawa warathi lile faili lililofunguliwa ilikuwa ni la Marehemu Fatma Mkombe ambapo yeye si mrithi. Kwa vile warathi wa Bi Fatma hawakuwa wanatoa mashirikiano sasa yule Bi Mwajuma yeye akachukua hatua za kwenda kutengeneza waraka. Waraka huu sio waraka ni *statutory declaration* yaani ni ku-*declare* tu kwamba haya ndiyo tuliyokubaliana mimi na mrithi mwenzangu. Ule wakati wowote mimi naweza nikaufuta, si waraka ni ku-*declare* na hiyo tume *declare* kwa sababu hawakwenda warathi, siku watakayokwenda *statutory declaration* tutatoa warathi kwa mujibu wa mirathi itakavyoendeshwa. Kwa hivyo tunaomba wahusika wafike huko kwa kufanya shughuli hizo.

Jambo jengine Mhe. Spika, ambalo lilizungumzwa nahisi ni muhimu kulizungumza ni suala la Bitha. Katika mazungumzo baina ya Mhe. Ismail Jussa alizungumzia suala la bitha. Bitha kwa ufupi ni kwamba watu wanapokwenda Hijja kuna Kikundi au jamii moja ambayo inakubalika kushughulikia masuala ya Hijja Saudi Arabia. Wenzetu wa Saudi Arabia wao wanatambua vikundi hivyo viwe vinatokana na Serikali. Kwa hivyo Tanzania kikundi ambacho kinatokana na Serikali ni Wakfu na Mali ya Amana, Tanzania Bara hakuna kikundi hicho. Lakini kwa sababu Wakfu na Mali ya Amana ni cha Zanzibar lakini ni Tanzania kwa hivyo hawa watu wa Zanzibar katika kikundi hicho cha Wakfu na Mali ya Amana hawa ndio wanawajibu wa kuitwa kwamba ni Bitha. Ni kikundi ambacho kinahusika na suala la Makka na Hijja.

Tatizo liliopo hapa ni kwamba tukisema kwamba kikundi hichi kuna wengine walikuja wakasema kwamba kikundi hichi labda kila mtu awe na chake.

Tanzania Bara iwe na chake na Zanzibar iwe na chake. Huo si ushauri mzuri kwa sababu wakiwa na chao kule na sisi tukiwa na chetu, suala lile lile la *foreign relations* ni Tanzania, hichi chetu kitatupwa. Bora hivi sasa sisi ndio tunaokiongoza Rais wa Bitha anatoka kwetu, kule tumechagua tu, tuendelee nacho. Najua kuna matatizo na matatizo haya hivi sasa yameshatufika. Juzi nilikutana na hao wenzetu wanaoendesha shughuli za Hijja, vile vikundi.

Tatizo ni kwamba kwa mfano, hivi sasa Saudi Arabia wameshaleta barua kwamba tupeleke idadi ya mahujaji wetu, Wazanzibari tuko tayari tumeshajua hivi sasa lakini wenzetu mpaka leo bado na sasa tatizo ni kwamba tukipeleka mahujaji kwa mfano Zanzibar tunakwenda tuseme 900, kule tukishapeleka *it means* wale kule Tanzania Bara sasa hawawezi kwenda kwa sababu kule ndio watakuwa wameshafunga. Sasa wenzetu siku zote wanachelewa hili ndio tatizo ambalo linatupa shida. Tunajitahidi Mhe. Spika, kuzungumza nao lakini matatizo kama hayo tunaendelea kuyashughulikia.

Lakini suala la Bitha Mhe. Spika, ndio kama hivyo lilivyo ingawa kwa muundo uliopo imesaidia kuratibu shughuli za hija lakini kuna matatizo kama hayo ambayo bado tunayakabili na tutatizama hatma yake tutafika pahala gani.

Mhe. Spika, nije katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Kulikuwa na mambo matano ambayo yalizungumzwa na mimi nitayasema haraka haraka. Kwanza Usajili wa Kituo cha Sheria na Utafiti kwa kweli hili tunalishughulikia, na tunalishughulikia kwa sababu ili kituo kipate jina hasa kitambulike, kuna mambo mengi lazima tuyafanye. Kwa mfano tupeleke zile *syllabus* zetu kule mitaala, tupeleke *Board of Directo*r na mambo kama hayo, sasa haya yote tunakamilisha ili tuweze kupeleka kunakohusika, na halafu tupate *accreditation* ya kituo hicho.

Chuo kupatiwa ruzuku na Serikali mapema iwezekanavyo na ADB iendelee kukisaidia Chuo tatajitahidi kufanya hivyo. Lakini kulikuwa na suala la Pemba na Afisi ya DPP, kweli Afisi ya DPP Pemba ni ndogo na napenda kulitaarifu Baraza lako Mhe. Spika, sasa Afisi ile wameshahama na wameshahamia katika hiyo Afisi mpya ilioko karibu na jengo la mahkama.

Kwa hivyo kuna hili suala la ucheleweshaji wa kumalizika kwa kesi kama nilivyosema mwanzo kwamba ni suala linalotokana na sababu nyingi lakini tutajitahidi kulifanyia kazi ili angalau kesi zetu ziwe zinakwenda haraka haraka.

Na la mwisho ilikuwa ni maslahi ya wanasheria ya Afisi ya DPP ni kweli DPP nayo ilikuwa maslahi yake ni kidogo, tukazungumza na wenzetu na

tunashukuru tulipata msaada kidogo, ingawa ni kidogo lakini tunajaribu kuzungumza tena ili tuweze kurekebisha masuala haya na kama alivyosema Mhe. Mwanasheria Mkuu lengo letu ni kuwa na sheria ambayo itajumuisha wanasheria wote wa Serikali na kila kada itakuwemo humo katika sheria na hapo ndio kila mtu atajua hasa utaratibu wake wa maslahi yake pamoja na mambo kama hayo.

Tume ya kurekebisha sheria ni kwamba tuliulizwa orodha ya sheria ambazo zinataka kurekebishwa. Mhe. Spika ni vigumu kusema kwa sababu kwanza Tume sisi tunapeleka kila Wizara tunawaambia hebu twambieni katika Wizara yenu kwa mfano Wizara ya Kilimo katika hizo sheria zenu mnazosimamia kwa mfano suala la wizi wa mazao na masuala mengine inayoshughulikiana na sheria kama zile tuambieni mnahisi kuna sheria ambazo zinataka kurekebishwa? Sasa ile *return* ya Wizara bado haijakamilika.

Lakini hivi sasa Mhe. Mhe. Spika, mimi hapa ninazo kiasi sheria 20 ambazo zinataka kurekebishwa na hizo zinaweza zikazidi kutetegemea Wizara zita-*respond* vipi. Lakini katika uharaka wenyewe sheria ya vileo na sheria ya Serikali za Mitaa ndizo ambazo tumezipa *priority* na zitashughulikiwa katika kipindi hiki ambacho tunakwenda nacho.

Lakini sheria nyengine tunazo na tunatizama au tutatizama ule utaratibu hasa wa namna gani ya kurekebisha sheria hizo hatua kwa hatua. Ninachopenda kusema ni kwamba urekebishaji wa sheria ni mkubwa una-*involve society*, *stakeholders* kwa hivyo tutajitahidi kuharakisha katika suala hili.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo limezungumzwa ni suala la Mashekhe pamoja na Makadhi na mambo kama hayo. Kama nilivyosema mwanzo kwamba suala hili kwanza tuliulizwa katika uamuzi wa Mahkama katika kesi za madai, halafu kukawa na suala la Mahkama ya Kadhi ya Wilaya ya Makunduchi kulikuwa na kesi 20 ambazo hazijatolewa maamuzi ni kwa sababu gani. Mhe. Spika, naomba niseme tu kwamba Mahkama ya Kadhi ya Makunduchi kulikuwa na kesi 19 na mpaka jana kesi zote zimeshatolewa maamuzi hakuna kesi ambayo imebakia.

Mhe.Spika, suala la Makadhi nalo lilizungumzwa ninaamini kwamba katika utendaji lazima kutatokea hitilafu moja, mbili, mimi ninawaahidi kwamba tutazidi kuchunguza ili tutizame kama kweli kuna matatizo ya Makadhi basi hatua tutazichukua. Ninajua nimepata fununu na hizo nimeshaanza kuzifanyia kazi za Kadhi ambaye alisema Mhe. Jussa kuchukua muda wake mrefu kuzungumza na watu waliokuwa hawahusiki. Ninao Ofisini huo uchunguzi

nimeshaanza kuufanya lakini bado sijawa katika *position* ya kusema katika suala hilo, lakini ninaahidi kwamba tutalichukulia hatua.

Suala jengine lililozungumzwa ni suala la Mufti, Mufti hatujamdhalilisha, lakini utaratibu ni kwamba kiongozi anapoteuliwa na Rais sasa mambo mengi yanafanywa kutoka Ikulu. Suala la gari ya Mufti ni moja katika masuala haya na ninawahakikishieni gari iko baharini hivi sasa na wakati wowote inaweza ikafika. Kwa hivyo hatuna wasi wasi kwamba Mufti wetu tutampatia kipando.

Kuhusu suala la Vyuo vya *Qur-an* hivi sasa Mhe. Spika, tuna vyuo karibu 2000 ambavyo tumevisajili. Sasa kusema vyote hivi tunataka kuwapa ruzuku siwezi kusema hivyo Mhe. Spika, tutaji-*commit* sana. Lakini tunachofanya, tunafanya utafiti kidogo na kutokana na sadaka ambazo zinawekwa katika Wakfu na Mali ya Amana hili pia linaweza kuwa moja ya kuwasaidia hawa wenzetu ambao wanafanya shughuli hizo za kidini.

Mhe. Spika, jengine ambalo nilizungumze kwa kifupi ni suala la Mhe. Mussa la UAMSHO. Mhe. Spika, UAMSHO ni sawa sawa na Jumuiya nyengine yoyote kwa mujibu wa sheria ina shughuli zake na inafanya shughuli zake. Mimi au Wizara yangu ina sheria hii nambari 6 ya mwaka 1995 pale ambapo tunahisi kwamba Jumuiya iliyosajiliwa siyo ya UAMSHO tu ikiwa inakwenda kinyume na yale matakwa yaliyosajiliwa basi hiyo tunatakiwa tuchukuwe hatua. Na kuchukua hatua kuna utaratibu wake huamki tu siku moja ukasema nachukua hatua za kufunga itakuwa sivyo, hatwendi sawa sawa na sheria. Kuna utaratibu unawaandikia barua, unawapa onyo, wakikataa kuyafuata hayo basi unachukua hatua za kufunga. Na hiyo mimi nasema tutafanya hivyo si kwa UAMSHO tu lakini kwa yoyote tutachukua hatua hizo kisheria kama nilivyochukua hatua ya kuwaandikia barua siku ya tarehe 20 June, 2012 nikawaandikia UAMSHO kwa nini wanakwenda kinyume na maadili au na utaratibu na *objects* na *reasons* zile ambazo wameandikishwa.

Sasa ukishafika hapo mimi sioni mtu anayetoka akasema kwamba kwa nini sijawafutia, siwezi kufuta ovyo ovyo, wala hakuna Mussa wala Vuai atakaekuja akanambia nifute, sifuti lazima nifuate utaratibu wa kisheria. Huo nitafuata na yeyote UAMSHO, aliyekuwa kalala akifanya nanii tutawafutia moja kwa moja. Kwa hivyo Mhe. Spika, nilikuwa naomba niseme hivyo kwamba NGOs nyengine zozote zile tunaweza tukazifuta ikiwa zitakwenda kinyume na matakwa au na utaratibu ulioandikwa.

Mhe. Spika, nije katika masuala mawili ya mwisho la kwanza ni suala ambalo Mhe. Mwenyekiti wa Baraza lako Mhe. Mahmoud alilizungumza suala lile la mafungu. Mafungu yale yote Mhe. Spika, ni mafungu ambayo yametokana na kuongezwa majukumu pamoja na maposho ya kujikimu. Kwa hivyo

ukitizama kwa mfano kifungu 142237 kutoka milioni saba mpaka milioni thalathini na nane, kwanza hili hapa ni ongezeko la mapato yaani mwaka jana sisi tulisema tutapata milioni saba lakini kutokana na utaratibu ambao tumeweka hivi sasa, tunahisi kwamba tutapata fedha nyingi. Kwa hivyo sisi tunaipa Serikali milioni thalathini na nane, kwa hivyo sioni kwamba hili lina matatizo.

Lakini la pili kutoka milioni mbili mpaka milioni kumi ongezeko katika kifungu hiki ni kweli mwaka jana tulikuwa na milioni mbili, lakini hivi sasa kuna madeni ambayo tulikuwa tunayo na ndio tukaona kwamba milioni mbili na hivi sasa tumeongeza watu *employment* imeongezeka kiasi watu wawili watatu kwa hivyo ndio ikapanda hivi kutokana na hilo kulipia deni ambalo tunalo. Mhe. Spika,kuna ongezeko jengine kutoka milioni nne mpaka milioni kumi na mbili kifungu 220506 hii ni kupanda kwa gharama za usafishaji na hii kwa mfano, maana yake milioni nne hii Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ilikuwa inafanya shughuli zake kwa milioni nne, lakini tujuwe tu kwamba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ina jengo jipya jengo limezidi na usafi itabidi uzidi mwahala chungunzima, kwa hivyo ndio maana tukapandisha kutoka milioni nne mpaka kumi na mbili ninafikiri hili si fedha nyingi sana ambazo Mheshimiwa alikuwa anauliza.

Kifungu 220201 hii inatokana na *bill* ya maji kutoka milioni moja mpaka milioni tatu, maji sasa yamepanda na kutokana na hivyo na utumiaji na kutokana na uongezekaji wa shughuli zile kwa hivyo ndio tukahisi ili tukawa-*safe side* kutoka milioni moja laki mbili mpaka milioni tatu si ongezeko kubwa sana.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo sasa naomba nichukuwe nafasi kidogo kuzungumza jambo la mwisho, na hili ni suala la katiba. Mhe. Spika, watu wengi wamezungumza suala la Katiba ninawashukuru sana, kwa sababu ninajua imani yao ni kuisaidia nchi hii. Lakini katika suala la katiba kuna suala kidogo lilijitokeza la *East African Federation*. Suala hili alilizungumza Mhe. Jussa ni kweli yeye kasikia uvumi uvumi, kwamba kuna mkataba umeandikwa *East African Federation*, tuwe na mkataba sasa wa hiyo *federation* nimeuona, lakini nilipouona nikasema kwamba hao walioandika pengine walikuwa ni vijana wanajaribu kujifundisha *drafting*, basi. Maana yake ikiwa mtu anajifundisha ataandika hata mimi nilipokuwa nikijifundisha *drafting* nilikuwa nikiandika tu *an act to power* kwa Serikali ya Kenya na nini wala Kenya sikujui. Kwa hivyo hawa msiwachukulie ni watu ambao wanajifundisha *drafting* wala wasiwashughulishe hata kidogo. Kwa sababu haiwezekani na mimi nasema hayo kwa sababu *position* yangu inanifanya niitetee nchi yangu na nitaendelea kutetea haiwezekani kwa nchi tano hizi

zijiingize tu katika mambo ya *federation* bila Zanzibar kujua haiwezekani hata siku moja.

Kwanza lazima tujuwe kuwa Tanzania kuna Tanganyika na Zanzibar na hapa tuna matatizo lazima tuya-*solve* matatizo yetu kwanza tujuwe msimamo wetu wa Kizanzibari halafu kama ndio tunataka kufanya *federation* basi tutakwenda na sisi wenyewe tutajua. Lakini ufanye *federation* kilimo hakihusu, elimu haihusiani na Muungano, mambo ya michezo haihusiani na Muungano, afya haihusiani na Muungano sasa kule ende Dr Mwinyi wa Muungano a-*represent* Zanzibar kama ni Wizara ya Afya haiwezekani hata siku moja lazima na sisi tuwe na msimamo wetu na tujue kwamba hii ni Zanzibar, na haki zake ni zipi na utaratibu wake utakuwa vipi.

Sasa mimi ninafikiri baadhi ya watu hawajui matakwa ya katiba. Katiba ya Jamhuri ya Muungano kifungu cha 98 kinaeleza wazi mambo gani au utaratibu utachukuliwa ili kitu ambacho kinataka kupitishwa kipitishwe kwa kuchukulia maanani nchi mbili hizi Tanganyika na Zanzibar. Moja ukisoma kifungu cha 98 (1) (b) kuna mambo ambayo lazima Zanzibar ikubali kwa *two third* na Tanganyika au Tanzania Bara ikubali kwa two third hayo yapo katika katiba. Lakini je tutizameni kwa mfano ukisoma hapa kwenye katiba orodha ya pili, hii orodha yenyewe ina matatizo, maana yake unaposema kwa mfano mambo ambayo mabadiliko yake yanahitaji kuungwa mkono na theluthi mbili ya wabunge wote kutoka Tanzania Bara na wabunge wote kutoka Zanzibar.

Sasa sikilizeni hayo mambo kuna la kwanza kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano, lazima sote tukubali, sasa hapa tunachofanya ni kuiondoa Jamhuri ya Muungano yaani tuiue kabisa twende kwenye federation haiwezekani. Lakini la pili imesema humu madaraka ya Serikali ya Zanzibar, Mahkama Kuu ya Zanzibar na idadi ya wabunge kutoka Zanzibar ndio hayo mambo yanayoongeza kero. Kama hatujayatatua haya tutakwendaje kwenye *federation*, wewe leo madaraka ya Serikali ya Zanzibar tuamuliwe na wabunge kutoka Tanganyika *never, never, never over my dead body* ndio watafanya hivyo hata siku moja haiwezekani. Maana yake sisi Serikali ya Zanzibar watu wa Bara huko watuamulie madaraka yetu ya Serikali ya Zanzibar ndio walivyoandika. Sasa haya ni matatizo tuyaamueni matatizo yetu kwanza na hapa napenda nim-*quote* Mhe. Rais wa Zanzibar kuna kitabu hichi tulitolewa mambo kumi ya msingi tunayopaswa kuyazingatia. Kila mtu ninafikiri aligaiwa hiki.

Namba 2 anasema tuweke maslahi ya taifa mbele kuliko maslahi yetu binafsi. Maslahi ya Taifa lazima yawe mbele kuliko maslahi yetu binafsi na akaendelea heka heka za kuleta maendeleo mahali popote zinahitaji mshikamano, moyo, ari na uzalendo wa hali ya juu bila kujali tofauti za aina

yoyote katika maumbile ya binaadam. Kila mmoja hana budi kuweka mbele maslahi ya taifa kuliko maslahi yake binafsi. Hali hiyo bila shaka itaweza kuleta mabadiliko ya haraka na maendeleo ya nchi. Wazungu wanasema *such delicious statement* hii aliyoitoa Rais wa Zanzibar tuifateni hii, kama mtu atasimama kwa ubinafsi hatutofika pahala na hatimae tutazidi kuidhoofisha Zanzibar kiuchumi, kimaendeleo tusifanyeni hivyo hata siku moja tusifanyeni hivyo.

Kwa hivyo katika huu mchakato wa katiba mimi ninachosema ni kwamba sisi sote tunawajibika si Serikali peke yake hata kidogo sisi sote tuliomo humu na walioko nje. Lakini zaidi sisi tuliomo humu wawakilishi, moja ya kazi ya wawakilishi ni kuwaelimisha wananchi wake wa jimbo. Kila mwakilishi anatakiwa ende katika jimbo lake akaseme jamani ee kuna mchakato wa katiba hivi sasa mchakato huu tunachokitaka ni hiki, ni hiki, ni hiki. Ni jukumu letu wawakilishi twendeni tukaseme nini tunakitaka.

Kwa mfano tunaweza tukasema je, hii Zanzibar katika hali tuliyonayo tunaridhika na utaratibu huu tulionao. Ikiwa haturidhiki wewe unatakiwa uzungumze katika jimbo lako na huridhiki kwa nini kwa sababu hii, na hii na hii. Je, katika huu mfumo tulionao Zanzibar yetu imekaa kama ni Zanzibar au ni kijisehemu tu cha Muungano. Hiyo 1964 ilikuwa ni sehemu tu ya Muungano au ilikuwa ni nchi. Na tulipoungana tuliungana nchi mbili zenye mamlaka sawasawa, si hoja Zanzibar kuwa ni ndogo na Tanganyika kuwa ni kubwa kwa watu milioni arubaini huku watu milioni moja, lakini ni nchi. Kuna nchi ina watu laki moja nilikwenda *Seychelles* kule watu laki moja na sitini ndio nchi nzima hiyo ina Rais wake, ina kila kitu chake lakini inatambuliwa.

Basi watu laki moja na sitini wanatambuliwa nje sie watu milioni moja tusitambuliwe mnakubali hivyo, mimi sikubali hata siku moja sikubali. Wala mimi kama ni Waziri wa Katiba na Sheria sioni raha na wala sitokubali kwenda nje chini ya mwamvuli wa Waziri wa Katiba wa Jamhuri ya Muungano. Nende na mikogo yangu kama ni Waziri wa Katiba na Sheria wa Zanzibar. Sasa kama hayo hatujayasema na wa kusema ni sisi tutaipoteza nchi yetu. Ni wajibu wetu sote kuelimishana hayo nini tunakitaka ili Zanzibar iwe ni nchi, ili Zanzibar iwe inaeleweka. Lakini hayo narejea tena kama alivyosema Mhe. Rais hayo lazima tushirikiane tuwe wamoja na ubinafsi tuuondoe, tukifanya hivyo tutafanikiwa tukifanya vyengine tutaharibikiwa ni vizazi vyetu vitakavyo tuhukumu. Mhe. Spika, baada ya kusema hivyo napenda nisisitize kwamba Zanzibar itajengwa na Wazanzibari wenyewe, lakini Wazanzibari lazima tushirikiane tuwe wamoja.

Lakini la mwisho la kumalizia Mhe. Hija alisema kwamba Tume hivi sasa iko Pemba, lakini kule Pemba kuna baadhi ya majimbo kuna eneo moja tu ambalo wameitwa kukutana. Kwanza napenda niseme kwamba suala la Tume Wizara ya Katiba na Sheria haihusiani sana lakini tunahusika kwa njia moja kwamba tunasaidia katika shughuli ya kuimarisha Zanzibar yetu. Sasa pale ambapo yanatokezea matatizo kama haya naomba tuarifiane. Mhe. Hija ameniarifu, nimewapigia wale wakanipa ratiba hii ninayo ni kweli kwa Jimbo la Kiwani kuna sehemu moja tu kitu ambacho si kizuri. Nimewasiliana na hilo litarekebishwa na litafanyiwa kazi.

Lakini katika suala jengine la Tume kuhusu majeshi kwamba wanapewa nafasi ya kutoa maoni yao pia tulilizungumza majeshi au vikosi vya ulinzi nao watapata nafasi ya kutoa maoni yao lakini katika kambi zao. Hii inaweza ikaleta tatizo ni kwamba mkubwa akeshakusema anataka Serikali sita basi wale majeshi wote watasema Serikali sita kwa ndio amri ya kijeshi. Mhe. Hamza anajua alikuwa jeshi yeye kwa hivyo baada hii kuiona tukazungumza tukasema watuwatendea haki wale askari wa chini. Kwa hivyo lililokubalika ni kwamba wale maofisa watakuwa sehemu yao tofauti na wale kruti wote watawekwa sehemu yao tofauti na wale. Kwa hivyo kila mtu atoe hoja zake anazozitaka. Na hiyo si kwa Zanzibar tu tunafanya majeshi *headquaters* kwa mfano Tume ilipokwenda Kusini vikosi vyetu vilikuwa vinataka kutoa maoni wakaambiwa aa maoni ya askari au jeshi yatakuwa *headquaters* tu. Kwa hivyo watakapokuja Mjini Magharibi watafanya hapa jeshini na headquater ya Polisi kama walivyofanya Bara katika *headquaters* 2.

Kwa hivyo tusiwe na wasiwasi sana hawa askari watapata kutoa maoni yao kwa mujibu anavyotaka hakuna kikwazo cha kuona mkubwa wake yupo atasema kile anachokitaka hiyo haitakuwepo.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, nawaomba niwashukuru wajumbe sana kwa ustahmilivu wao na nawaomba niwaombe radhi kwamba si yote ambayo nimeyazungumza kwamba nimekidhi haja ya kuwajibu waheshimiwa wote. Lakini nimejitahidi na inshaalla yale ambayo hatukuyazungumza ninawahakikishieni kwamba tutayafanyia kazi na kwa faida ya kuendeleza Zanzibar yetu na kwa faida ya vijana wetu na kwa faida ya watoto wetu.
Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri tunakushukuru kwa majumuisho hayo, nimejaribu kutoa muda wa kutosha ili uweze kufafanua mambo mbali mbali na kuleta wepesi kwenye hatua inayofuata baada ya hapa.

Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Katiba na Sheria kwa

mwaka 2012/2013 wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza lako tukufu limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kupitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

Fungu 14 Mahkama Kuu Zanzibar

Kifungu 0201 – Utawala Unguja	Sh. 53,500,000
Kifungu 0301 – Ofisi Kuu Pemba	Sh. 18,500,000
Jumla ya Fungu:	Sh. **72,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 36 Wizara ya Katiba na Sheria

Kifungu 0011 – Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali	Sh. 395,000,000
Jumla ya Fungu:	Sh. **395,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 14 Mahkama Kuu Zanzibar

Kifungu 0201 – Utawala Unguja	Sh. 2,026,920,000
Kifungu 0301 – Ofisi Kuu Pemba	Sh. 843,980,000
Kifungu 0601 – Afisi ya Kadhi Mkuu	Sh. 274,100,000
Jumla ya Fungu:	Sh. **3,145,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 15 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar

Kifungu 0201 – Utawala Unguja	Sh. 83,760,000
Jumla ya Fungu:	Sh. **802,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naomba anapotusomea hizi kurasa kidogo atulie kwa sababu tunamfuata yeye, sasa tunakuwa hatuzioni.

Mhe. Mwenyekiti: sawa sawa.

Fungu 35 Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka

Kifungu 0201 – Utawala Unguja Sh. 685,800,000

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, msomaji wa vifungu anasoma haraka haraka asome taratibu ili tuweze kufahamu. Kwa sababu akisoma haraka matokeo yake hakuna tunachokisikia Mhe. Mwenyekiti. Usione kwamba hatuna kitu cha kuzungumza tunayo mengi hapa, lakini anakwenda kama charahani parapapa sasa sijui hivi tunakwendaje.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, wakati wa kupitisha vifungu tuwatafute watu wenye uwezo wa kusema ili tuelewe.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa, tutajitahidi twende kwa taratibu ile charahani itabidi tushone kwa ile bandi kubwa.

Kifungu 0202 – Kituo cha Mafunzo na Utafiti wa Sheria	Sh. 100,000,000
Kifungu 0301 – Ofisi Kuu Pemba	Sh. 193,200,000
Jumla ya Fungu:	Sh. **979,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 36 Wizara ya Katiba na Sheria

Kifungu 0011

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa ya kuweza kuchangia katika sehemu hii. Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia nilimuomba Mhe. Waziri atupe maelekezo juu ya suala

zima la Mahkama za Tanzania. Nilipokuwa nachangia nilimwambia kwamba tuna Mahkama ya Zanzibar, tuna Mahkama ya Tanzania na tuna Mahkama ya Rufaa. Lakini katika Mahkama Kuu ambayo ni Mahkama ya Rufaa Mzanzibari ni mmoja kati ya wafanyakazi 16 ambao wamo katika Mahkama ile. Sasa nilitaka kujua kutoka kwa Mhe. Waziri lakini alipokuja hapa naona sikumsikia katika majibu yake aliyoyatoa. Ni sababu zipi zilizopelekea hata ikabidi kwamba tuna mfanyakazi mmoja tu kutoka Zanzibar ndani ya Mahkama Kuu hata tukashindwa kuweza kumpeleka katika maeneo mengine kama vile Afrika Mashariki ambapo napo pia pana kitengo ambacho kinataka mwakilishi kutoka maeneo yetu. Naomba maelekezo.

Mhe. Mwenyekiti: Sina hakika kama fungu lenyewe ndio hili, kwa sababu hili fungu la Mrajis Mkuu wa Serikali ambapo sio pahala pake. Eneo la Mahkama Kuu ambalo pengine ungeweza kusema kitu inaonekana tulikwishalipita.

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nitasubiri Idara ya Sera na Mipango.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpe taire Mhe. Waziri manaake huku *backbencher* kumeingia homa kote. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kwa kuwa nanyanyuka kwa mara ya kwanza nataka kumshukuru sana Mhe. Waziri kwa ufafanuzi wake wa kina na utulivu nadhani ndio maana hakuhitaji kiringe kilikuwa kinatosha kiringe cha pale mbele kutufanya tusiwe na hoja nyingi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, bila shaka hawezi kuyajibu maswali yote tuliyomuuliza na alitupa fursa ya kuweza kutaka ufafanuzi katika maeneo mbali mbali. Sasa Mhe. Mwenyekiti, katika maeneo ambayo niliyachangia eneo moja ambalo nilihoji lilikuwa linahusu Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali na hasa katika suala la bajeti ambayo imetengewa ofisi hiyo ukilinganisha ile ya Unguja na ya Pemba. Sasa naliuliza hapa kwa sababu linahusika kote kote.

Mhe. Mwenyekiti, najua kuna *support* yake ya Pemba lakini naliuliza hapa kwa sababu huu mgawanyo wa bajeti naona hauna ulinganifu sasa naogopa nisingoje Pemba likawa hili limeshapita. Sasa naomba Mhe. Waziri anisaidie kwa nini bajeti hizi mbili za ofisi hizi ambazo zinafanya kazi najua Makao Makuu yako Unguja lakini zinafanya kazi zinazolingana na hasa nilisema katika mchango wangu kwamba ukitizama Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali kwa upande wa Pemba ina matatizo mengi, mahitaji mengi, lakini fungu yote yamepungua kidogo pengine kwa sababu ya kuanzishwa ile Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo, lakini naona kile kiwango na uwiano kupungua ina tofauti

kubwa sana, hivyo naomba Mhe. Waziri anisaidie. Je, katika bajeti hii atazingatia yale mahitaji ya Ofisi ya Mrajis Mkuu kwa upande wa Pemba ambayo wanayahitaji.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti nakushukuru, ni kweli bajeti ya Mrajis Mkuu wa Pemba ni ndogo sana na hii ni ndogo makusudi kwa sababu katika utaratibu wetu wa safari hii Mrajis Mkuu wa Serikali *mainly* atakuwa yuko Unguja, wale *staff* wote wa Mrajis Mkuu wa Serikali ambao tulikuwanao katika kipindi kilichopita sasa wale wako katika ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo. Kwa hivyo, pale itakuwa ni mtu mmoja tu ambaye anafanya pengine shughuli ndogo ndogo kwa sababu ile shughuli hasa ya Mrajis Mkuu wa Serikali sasa itakuwa iko huku zaidi kuliko kule Pemba. Kwa hivyo, *actually* Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali Pemba unaweza ukasema kwamba itakuwa haipo zaidi kuliko Mrajis Mkuu wa Vizazi na Vifo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Waziri kwa maelezo yake lakini mimi naomba anisaidie tu kwamba, pamoja na kuwa shughuli zimepungua sana lakini bado ziko baadhi ya shughuli ambazo zitaendelea kufanywa na Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali. Labda nitoe mfano ili nieleweke Mhe. Mwenyekiti.

Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria na Utawala kamati yako Mhe. Mwenyekiti, moja nililoligundua kule ni tatizo la usafiri basi najua masuala ya vizazi na vifo yana ofisi yake sasa, lakini yako masuala kwa mfano tulikuwa tukilalamikiwa hata katika masuala mfano ya usajili wa ndoa na talaka ambayo bado yanahitaji kufuatwa vijijini na jiografia ya Pemba tunaielewa sana. Kwa hivyo, naomba anisaidie katika hii bajeti wamezingatia haja ya kuwapelekea usafiri Kisiwani Pemba na hili alizungumza kama ninavyosema ni katika bajeti ya Unguja kwa sababu kama alivyosema Makao Makuu ya Ofisi hii yako hapa Unguja. Sasa naomba anisaidie Mhe. Waziri wamelizingatia hilo.

Kwa sababu yeye mwenyewe Mhe. Waziri atakuwa shahidi hatujafika lakini nalinganisha tu, akifika Ofisi ya Mrajis Mkuu Pemba utakuta kuna maeneo mengi yana *zero*, *zero*, ni kama vile zile shughuli za ofisi zimeondoshwa kabisa. Kwa hivyo, nilikuwa naomba angalau hili la usafiri anisaidie kwa sababu hili ni moja katika kilio chao kikubwa sana. Katika uwiano wa bajeti hizi mbili baina ya Makao Makuu Unguja na ile ya Pemba.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali Pemba itakuwa *almost* haipo kwa sababu shughuli zake kutokana na huu mfumo ambao tumefanya hivi sasa zote zitakuwepo hapa. Alipotoa mfano wa ndoa na talaka zile zote ziko katika

Mrajis wa Vizazi na Vifo, sasa kule kutakuwa hakuna shughuli hata moja na ndio ukaona maziro ziro yote kule, zile kazi ndogo ambazo zitakuwepo wale wale Mrajis wa Serikali wa Vizazi na Vifo ndio watazifanya na ndio utaona kwamba fungu limekwenda katika Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo Pemba. Lakini Mrajis Mkuu wa Serikali itakuwa haipo hasa kwa sababu ya huu utaratibu mpya ambao tumeuanzisha.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na kwa sababu ofisi hii imeanzishwa karibuni mimi nilichukua kwa mujibu wa jina lake lilivyo kwamba ni Ofisi ya Msajili wa Vizazi na Vifo, lakini kwa maelezo yake hayo Mhe. Waziri naomba tuendelee na kwa sababu tuna nafasi kutumia Kamati yetu kufatilia zaidi nafikiri tutafatilia. Labda nitaomba maelezo kuhusu usafiri sasa kwa huko kulikohamishiwa tukifika katika hiyo idara. Namuomba Mheshimiwa tuendelee ahsante sana.

Kifungu 0011 – Ofisi ya Mrajis Mkuu Mkuu wa Serikali Sh. 249,674,000
Kifungu 0012 – Ofisi ya Mrajis Mkuu Pemba Sh. 15,999,000
Kifungu 0301 – Ofisi Kuu Pemba Sh. 165,331,000
Kifungu 0401

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, naomba kupata majawabu ya yale maombi niliyokuwa nimeomba.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, bado mimi nilikuwa nafikiria kwamba suala lake liko kwenye Mahkama, lakini kwa faida ya Waheshimiwa Wajumbe naomba nilijibu hivi. Kuna Mahkama Kuu ya Zanzibar na kuna Mahkama Kuu ya Jamhuri ya Muungano, Mahkama Kuu ya Zanzibar ina mahkama zake ambazo ni Mahkama ya Mwanzo, Mahkama ya Wilaya, Mahkama ya Mkoa na Mahkama Kuu na huku upande mwengine kuna Mahkama za Kadhi. Mahkama za Tanzania Bara zimeanza hivyohivyo, Mahkama ya Mwanzo mpaka Mahkama Kuu. Sasa hivi ni Mahkama tofauti, kila mtu ana *jurisdiction* yake na si suala la Muungano, lakini Mahkama ya Rufaa ni suala la Muungano.

Lakini Mahkama ya Rufaa kuna utaratibu wake wa uajiri wa majaji, kuna *qualification* zake, sasa *qualification* hizo mtu anapozipata ndio anaweza akateuliwa. Kwa mfano, ameteuliwa Mhe. Augustino Ramadhan kwa sababu alikuwa ana-*qualify,* ameteuliwa Mhe. Mbarouk kwa sababu ana-*qualify*, alikuwepo Mhe. Ali Omar kwa sababu ana-*qualify,* lakini majaji ambao waliopo hivi sasa huwezi tu kuwateuwa Mahkama ya Rufaa kwa sababu zile *qualification* zao bado hazijafika kuteuliwa. Sasa hicho ndio kikwazo chetu sisi, hivyo uteuzi huo unakwenda kwa ngazi hizo na ndio maana kwa hivi sasa tuna jaji mmoja tu wa Mahkama ya Rufaa Mhe. Mbarouk kwa sababu ya

qualification zake na hapo ambapo majaji wetu wata-*qualify* basi naamini kwamba watateuliwa. Nakushukuru.

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimeridhika kwamba Mhe. Waziri ametujibu kuwa hatuna majaji wenye *qualification* ambao wanaweza kuingia kufanya kazi ndani ya Mahkama ya Rufaa. Kwa msingi huo vile vile hatuna majaji wa kuweza kufanya kazi katika *East Africa*, ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, niendelee kuomba radhi unajua leo Mhe. Waziri itabidi tupige taire na hilo sio tatizo la meza yako, meza yako haina tatizo lakini Mhe. Waziri kidogo amefanya mambo lakini ndio utu uzima.
Mhe. Mwenyekiti, nilihoji kuhusu ratiba ya Tume, Mhe. Waziri nimemfahamu lakini sijambo jepesi kama anavyolifikiria kuwa tume itarekebisha. Kwa mujibu wa Katiba zote na Sheria haki ya kupata habari na kutoa maoni ni haki ya mwananchi, kwa hivyo nataka anambie nikitoka hapa kwa sababu Tume iko Pemba na leo imeanza Chake Chake keshokutwa inakwenda Kiwani angalau niwe na jibu gani kwamba itarekebishwa nikae hivyo hivyo au ikifika ile siku ya tume hatukurekebishiwa wananchi wa Kiwani wamlaumu yeye kwa sababu yeye ndio Waziri wa Katiba na Sheria.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba Mamlaka ya Tume hayako katika Wizara ya Katiba na Sheria, lakini tunachofanya ni mawasiliano ya karibu baina ya Wizara ya Katiba na Sheria na Mamlaka ya Tume. Baada ya kuleta tatizo hilo mimi nikawasiliana nao kwa ile ile kusaidia na kulinda haki za nchi yetu, wameniletea hii na atiba hizi Mhe. Mwenyekiti, zimetolewa kwenye magazeti si kitu cha siri hata yeye akitaka baadae mimi nitampa hii. Lakini ninachosema ni kwamba kama kuna tatizo lolote kwa mtu yeyote, kwa mjumbe yoyote akiniona mimi nitawasiliana nao na tukishawasiliana wanarekebisha.

Kwa mfano Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Abdalla Juma wa Chonga nae alikuwa na matatizo hivyo hivyo akanielezea tukawasiliana nao na wakarekebisha. Na Mhe. Hija Hassan amenielezea tumewasiliana nao na watarekebisha. Kwa hivyo, naamini kwa sababu ya mahusiano yetu yaliyo ya karibu yalivyo kama kuna tatizo lolote bado napenda niseme tena mtu yoyote anaweza akawasiliana na mimi na mimi nitawasiliana nao na wao watarekebisha.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi namfahamu Mhe. Waziri lakini na mimi huyo katibu amenipigia simu, lakini bado anasisitiza kwamba Kangani ni Kiwani mimi nasema Kangani ni Mtambile, Mtambile kuna Mtambile yenyewe, Kengeja na Kangani; Kiwani Shehia sita zina kituo

kimoja. Kama wamewasiliana na kama yeye katibu wa tume ndio amempa jibu sahihi kama Waziri kwa nini asimwambie kwamba nitaweka shehia nyengine aongeze angalau ya pili, kama hajamwambia leo wakati tume iko Pemba atamwambia lini na nikimkosa leo simpati tena. Kwa hivyo, wawasiliane anambie kaambiwa lini na shehia gani.

Mimi nimesema Shamiani kama kisiwa kuvuuka bahari ya kwanza, bahari ya pili, ya tatu itakuwa vigumu kwa nini kituo kingine hakiwekwi pale Mwambe ili Kisiwa cha Shamiani waje pale Mwambe, lakini Mhe. Waziri akinambia kwamba watawasiliana nikimkosa leo nitayapata lini majibu na tume hainisubiri mimi. Kama wao si jambo lao wao ndio tuliowatuma na Mwanasheria Mkuu kwenda kusikiliza masuala ya Zanzibar kuhusu tume hii nani hasa tumkamate tupate ratiba sahihi.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, Kangani si Kiwani kama alivyosema nakubaliana naye, matatizo yaliyojitokeza kwa wale waandaaji wa ratiba pengine Pemba ni kugeni kwao wao kwa hivyo, wame-*confuse* baadhi ya majina. Mhe. Hija tulikuwa pamoja tukazungumza na leo Katibu wa Tume kenda Pemba kufanya marekebisho haya na yeye anajua kama kenda Pemba *time* za mchana kasafiri kwenda huko. Sasa tuamini kwamba Katibu wa Tume atayarekebisha haya badala ya kituo kimoja bila shaka hayo maeneo ya visiwa yatakuwa *considered* kama alivyoniahidi katibu naamini atafanya.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina tatizo na kumuamini Mhe. Waziri namuamini sana, lakini Mhe. Mwenyekiti, Tume hii inaongozwa na Jaji Warioba Tume yenye wataalamu wakubwa, sidhani mimi majibu haya kwamba tuamini ndio yatatosha kurekebisha hiyo ratiba na hasa kwa vile anasema hata wao hawahusiki vyema, si bora angelinambia tu kwamba ndio yale yale katika kero za Muungano tuliache. Kwa sababu ikiwa wao hawakuhusika kiasi hicho leo ananambia mimi tuamini labda Mhe. Waziri anambie kwamba ni miongoni mwa kero za muungano ili wananchi wote wa Jimbo la Kiwani waende hiyo sehemu moja wakagombanie huko kutoa maoni. Naomba anambie tumalize.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, siwezi kumwambia hivyo kwa sababu naamini Katibu wa Tume kwa sababu ni Mzanzibari ana uchungu wa Zanzibar na suala hili tumelizungumza pamoja naamini atalitekeleza. Kwa hivyo, siwezi kumwambia vyengine vyovyote.

Mhe. Mwenyekiti: Labda mimi niongezee jambo moja tu kwamba hii tume ni mamlaka kamili. Kama kuna mapungufu wajibu wetu ni kuwapa taarifa kwamba kuna mapungufu moja, mbili, tatu kwa kutegemea sasa wao

warekebishe kama vile mifano aliyotoa ya Mhe. Abdalla Juma Abdalla. Kwa hivyo, hapa hawezi akarekebisha ratiba yoyote, ni kuwaarifu ili watekeleze wajibu wao wa kuandaa ratiba kama watarejea baadae na uwezekano huo upo. Mimi nadhani ni kitu ambacho hapa hawezi Mhe. Waziri akatoa majibu zaidi ya kuwaarifu kwamba kuna mapungufu kadhaa tunakuombeni mrekebishe hayo. Nadhani hiyo ndio hali halisi.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubaliana na busara zako na hayo ndio mapungufu mengine kwa Wazanzibari, kwamba hata ukitoa maoni wanabinywa seuze hiyo kupiga kura ya maoni. Kwa hivyo kwa sababu tumeona hilo na Waziri wa Katiba na Sheria yupo, sawa lakini aone kwamba Wazanzibari wanalo kosa kutoa maoni seuze hayo maoni yenyewe kuthaminiwa. Maana kutoa maoni ni jambo rahisi kuliko maoni yenyewe kuthaminiwa. Ikiwa hili la kusema linakatazwa linabinywabinywa, watu elfu ishirini wakaekewe kituo kimoja ni dhahiri Wazanzibari wanaendelea kubinywa maoni yao.

Kwa hivyo madhali limeonekana na serikali na serikali ndio nyinyi, tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, naona Mhe. Mwakilishi anapotosha, kwa sababu hii ratiba kuna majimbo mengine yana vituo vinne. Kuna wengine wanakosea kama walivyokosea la Mhe. Abdalla Juma Abdalla tukazungumza nao wakalirekebisha. Kuna hili la Mhe. Hija kuna kituo kimoja kwa sababu wali-*confuse* wale baadhi ya maeneo walifikiria kwamba yapo katika jimbo lake, na hayo tulizungumza mimi na Mhe. Hija na Katibu wa tume, na akakubali kuyafanya hivyo kurekebisha.

Sasa kama yeye alikuwepo na akasema mbele yake kuwa atarekebisha na akenda Pemba kwa suala hilo na mengine. Sasa kuna tatizo gani la kuchukua au la kutochukua kwamba yeye hatorekebisha. Sasa ndio nikasema mimi sitokubaliana na yeye kwa sababu suala lilitokea la Chambani na Chonga tukalirekebisha, na hili limetokea Katibu amekubali kulichukua.

Sasa matatizo pengine wale wali-*confuse* majina, ni wageni hawajui. Maeneo mengine wameyatia katika majimbo mengine ambavyo sivyo. Baada ya kuyaona hayo ndio tukachukua hatua ya kuyarekebisha na hayo wakahakikisha kwamba watarekebisha.

Mhe. Mwenyekiti: Kama ni wajibu ninadhani Waziri katimiza wajibu wake kuiarifu tume ili ichukue hatua ya kufanya marekebisho. Ninadhani tuombe muda wa kuongeza.

(Baraza lilirudia)

KUONGEZWA MUDA WA BARAZA

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamo wa Pili wa Rais): Mhe. Spika, ninakushukuru kwa kunipa fursa hii kuliomba Baraza lako tukufu kwamba, kwa sababu majadiliano bado yanaendelea, muda wetu wa kawaida unakaribia kumalizika naomba tuweke Kanuni kando ili tupate muda wa kumaliza mjadala huu mpaka hapo utakapomalizika.

Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja ilikubaliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA MATUMIZI

Mhe. Mwenyekiti: Tunamalizia hoja ya tatu kwenye fungu hili kwa kumwita Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa uadilifu wako kwa sababu upande wako au upande wa kushoto ilikuwa tayari umeshatoa nafasi mbili. Sasa upande wa kulia ilikuwa hujatoa nafasi. Kwa hivyo ninakushukuru kwa hilo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia ninataka niwapongeze Mashekhe waliokuja leo, maana yake vifungu vingi tulikuwa hatuvioni. Sasa zile tasbihi...

Sasa Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nilikuwa ninataka ufafanuzi kidogo kwa Mhe. Waziri, kimsingi majibu yake yameniridhisha lakini tatizo naomba niliseme, kwamba Mawaziri wanawajibika kwa pamoja.

Siku ya Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora mimi nilihoji haki za Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo, lakini Mhe. Waziri kwa ukali na hasira akasema hatulipi *arrears*, kwa kweli lugha ile kidogo ilikuwa si nzuri hasa kwa Waziri ambaye anasimamia Utawala Bora.

Lakini leo ninashukuru Mhe. Waziri amekiri kwamba kulikuwa kuna haki ya Mahakimu wetu wa Mahakama ya Mwanzo, na kwa kweli kwa kuwa kosa sio lao na ile haki na wao walikuwa wanastahiki kupata. Ninadhani leo Mhe. Waziri katujibu vizuri.

Sasa nilikuwa naomba kauli moja ifutwe ya Waziri mmoja ibakie kauli ya Waziri mmoja ili tujue, isijekuwa anatupa kauli nzuri ili tupitishe fungu halafu matokeo yake hakuna kitakachokuwa. *Hansard* watakayoirudia ile hatulipi *arrears*.

Sasa nilikuwa hapa Mhe. Waziri atuthibitishie jee Mahakimu wake hawa ataweza kusimamia haki yao ili na zile *arrears* ambazo walizozikosa wazipate. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, katika maelezo yangu nilisema kwamba kulikuwa kuna matatizo, na matatizo hayo tukayazungumza baina ya wizara yangu na Wizara ya Utumishi wa Umma.

Na ni kweli Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma alisema kwamba hatutolipa *arrears*, hiyo ni kwa sababu katika maelezo binadamu unaweza pengine hakuelewa au hakufahamu yale masuala na wale hawakuajiriwa siku ile ambayo wanapewa mshahara wao.

Wale waliajiriwa sawa au wakati *arrears* zilipoongezwa mwezi wa Oktoba na wao walikuwa kazini. Sasa ni binadamu baada ya kufahamishana na yeye akakubali. Kwa hivyo bado mimi ninasema kwa sababu mimi ndio Waziri ninayehusika na wizara hii tutasimamia, kwa sababu wale ni watu wa *profession* yangu, mimi nitakuwa sijafanya haki yangu kama sijawatetea hawa.

Kwa hivyo bado ninamuhakikishia kwamba vijana hawa au Mahakimu wetu hawa tutatetea haki zao ili kuhakikisha kwamba na wao wanawekwa sawa sawa na watumishi waliopata nyongeza yao mwezi wa Oktoba.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mhe. Waziri kwa kauli yake hiyo na ninashukuru vile vile kwa kumuombea radhi Mhe. Waziri aliyezungumza kitu ambacho hakijui.

Sasa wasia wangu tu, nilikuwa ninaomba Waheshimiwa Mawaziri, sisi kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, moja katika majukumu yetu ni kuwauliza maswali na wao wanapotujibu wasitujibu kwa hasira, watujibu kwa utulivu ili kile wanachokijibu ajue siku ya pili asije akakosolewa kwamba katujibu bila ya kufanya utafiti na kujua alichotujibu.

Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru kwa hilo na naomba tuendelee.

Kifungu 0401 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	Sh.172, 860,000/=
Kifungu 0501 Afisi ya Mufti Unguja	Sh.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia nilimuomba Mhe. Waziri kuhusu suala la Vyuo vya Kiislamu, kalijibu lakini pamoja na majibu yake anayojibu basi Mhe. Waziri ninamuomba kama waangalie hata kama ni kuwekea mradi au NGO ambayo itawasaidia walimu wa vyuo, kwa sababu walimu wetu hawa wana kazi kubwa, kama walimu wa skuli wanavyo kazi basi na wao wana kazi kubwa ya kuwaelimisha watoto wetu.

Kwa hivyo na wao wana haki ya kufikiriwa pamoja na kasema kwamba ni watu 2000 lakini kasema kwanza atafikiria. Kwa hivyo mimi naomba kama hata kama ni kuwakusanya au kuwawekea NGO ambayo itakuwa na mchango wa kupata fedha za kuwasaidia wao, lakini Mhe. Waziri atujibu hivyo kama watawasaidia walimu wa vyuo kwa sababu suala hili tumeshalipigania mara nyingi, kila bajeti inapokuja tunalizungumza lakini ni sawa sawa na Madiwani wetu, tunapowapigia Madiwani na hawa walimu wa vyuo basi inakuwa ni sawa sawa majibu yake.

Naomba Mhe. Waziri anipe majibu.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, tulisema au nilisema kwamba vyuo ambavyo Afisi ya Mufti imevipitia ni karibu 2000 au zaidi ya 2000. Haina maana kwamba walimu ni 2000 inawezekana ikawa walimu ni 6000 au 10,000 kwa sababu kila chuo kinaweza kikawa na walimu wanne, watano, wengine vyuo vikubwa walimu 10.

Kwa hivyo idadi ya walimu ni wengi sio 2000 inaweza ikawa hata elfu sita mpaka elfu kumi.

Sasa kusema hapa kwamba tutawasaidia kwa kitu fulani haiwezekani, na ndio maana nikasema tumesikia, tutashirikiana hii diwani ya zakka ambayo ipo katika wizara yangu, tutatizama njia gani za kuwasaidia walimu hawa. Nia ya kuwasaidia tunayo, lakini hatuwezi kusema hapa tutawasaidia kwa kuwawekea mradi, watu elfu kumi utaweka mradi gani, haiwezekani mpaka tufanye *study* kwanza halafu tujue tutawasaidia kwa njia gani.

Ninachoweza kusema ni kwamba hilo tunalichukua tutatizama nini cha kufanya, tutashirikiana na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana katika diwani ya zakka ili kuweza kujua walimu hawa tutawasaidia namna gani.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, sijasema kwamba lazima awalipe mwalimu mmoja lakini kila chuo kina mwalimu mkuu. Sasa lile fungu atakalopewa mwalimu mkuu atajua yeye kusaidia walimu wake wadogo.

Lakini walimu wanakuwa na chuo masaa 24 hawana kazi yoyote kwa sababu vyuo vya Qur-an walimu wake ni sawa sawa na hawa walimu wa skuli wanavyopata kazi, kwa sababu watoto wakitoka skuli wanakuwa kwenye madrassa.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, yeye Mhe. Waziri kama atashirikiana na Afisi ya Mufti atwambie kama lishakubalika hilo watapata japo sabuni, si lazima walipwe mishahara ili waweze kujikidhi kwa kufanya kazi zaidi kuwasomesha watoto wetu.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kuwasaidia tutawasaidia inaweza ikawa sabuni, mkate au pilau lakini kwanza lazima tufanye utafiti.

Sasa tukishafanya utafiti na kutizama namna gani ya kuwasaidia. Sasa ndio tutajua tuwape sabuni, mkate au tuwape nini. Lakini ninahakikisha kwamba tutawasaidia.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, kama ameshakubali kama atawasaidia tuendelee. Bajeti inakuja tena mwaka ujao.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Nilipokuwa nikichangia Afisi ya Mufti nililalamikia sana Wizara kwamba Mhe. Mufti hana usafiri wa kuaminika. Mhe. Waziri alisema katika majumuisho yake kwamba kuna mambo mengine ambayo hakuyatolea ufafanuzi pale atayafanyia kazi. Sasa hili ni miongoni mwa mambo ambayo atayafanyia kazi?
Mhe Mwenyekiti: Mhe. Waziri ingawa majibu ulitoa lakini kwa kuongezea.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, nilisema kwamba moja katika suala ambalo hili tumeshalikamilisha ni suala la usafiri wa Mufti, na nikasema kwamba gari ipo baharini. Kwa sababu ya kusema hivyo, ni kwamba gari zimeshaagizishiwa tunasubiri zifike tu ili naye Mufti apate gari.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa ipo baharini sio kwamba imezama.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 0501 Afisi ya Mufti Unguja	Sh. 249, 741,000/=
Kifungu 0502 Afisi ya Mufti Pemba	Sh. 88, 583,000/=
Kifungu 0601	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, niendelee kuwapongeza Mashekhe kwa kazi nzito waliyofanya huko juu, lakini katika mchango nilizungumzia suala la mjadala wa Katiba, na ninashukuru takriban Wajumbe wote wamechangia kwa njia moja au nyengine wameligusa.

Ninataka niseme kwamba nimesikiliza kwa makini majibu au majumuisho tangu yaliyotolewa na Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mhe. Waziri, ninataka niseme kwa dhati kabisa ninawapongeza sana kwa maelezo ya kina, fasaha ambayo yamejielekeza kabisa katika hoja.

Ninadhani leo wananchi wa Zanzibar kiasi kikubwa watapata utulivu, ule wasi wasi waliokuwa nao kiasi fulani katika serikali yao umeshapata majibu.

Hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba katika majumuisho takriban wote wamesisitiza haja ya kila mmoja kutekeleza wajibu wake, viongozi na wananchi. Lakini pia wametupa kazi sisi Wawakilishi tufanye wajibu wetu, tunaupokea Mhe. Mwenyekiti.

Sasa mimi hapa nilikuwa na hoja moja Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba Mhe. Waziri anisaidie. Tulipokuwa tukijadili bajeti ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, tulizungumza suala la haja ya Wawakilishi wenyewe kwanza kuelimishwa, inawezekana Wawakilishi wengi unawapa kazi hii wao wenyewe haya masuala wakawa hawayaelewi vizuri.

Ninashukuru kwamba tulipewa kauli kwamba kuna mradi ambao umeandaliwa kuwapa mafunzo katika sura hii. Sasa nilikuwa naomba tu Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ile kiu ya wananchi ikamilike sasa kwamba angalau Wawakilishi wao katika kupata kauli moja ya kuwaeleza wananchi wa Zanzibar, hili suala la mafunzo haya au semina katika suala hili Mhe. Waziri ninajua alikuwa akishirikiana na Afisi yako Mhe. Mwenyekiti, hebu atusaidie kwamba suala hili linatarajiwa kutekelezwa lini ili tuwahi huu mchakato ambao tayari unaendelea huko mitaani.

Mhe. Mwenyekiti, naomba ufafanuzi kutoka kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru. Mhe. Jussa aliyesema ni kweli na tuliwahi kuzungumza na wenzetu wa Norway na wao tukakubaliana baadhi ya mambo, lakini baada ya kukubaliana hivyo kwa

mujibu wa sheria ya marekebisho ya Katiba, lazima hata katika chombo chetu tupate idhini ya Tume ya mchakato wa Katiba.

Idhini hiyo tumeshaipata na hapa barua imeletwa hivi sasa kwamba Kamati ya Uongozi wa Baraza la Wawakilishi itakutana ili kujadili utaratibu wa kufanyika. Kwa hivyo ninawahakikishia kwamba semina hiyo itafanyika.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ninaamini kila Mwakilishi tutapata faraja ninashukuru afisi yako Mhe. Mwenyekiti, na Afisi yake Mhe. Waziri naomba tuendelee. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Labda nyongeza yake ni ndogo sana juu ya hili, ni kwamba safari tuliyofanya juzi na Katibu wa Baraza la Wawakilishi ilikuwa inahusiana na hili. Na ni kweli tumeshapata baraka za Tume kwamba jambo hili tulianzishe.

Kama alivyosema Mhe. Waziri pale kwamba ile kamati ndogo ya uongozi juu ya jambo hili tunategemea kukaa kesho na keshokutwa tuna *launch* rasmi shughuli hii Mzee Warioba atakuja.

Kwa hivyo nilitaka nitoe taarifa hiyo tu. Hiyo kazi ambayo muliyonituma nikaifanye kwa ajili ya Baraza. Kazi ya mwanzo itakuwa ni kuwaelimisha wajumbe.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ninadhani itakuwa hatutendi haki, nimesimama kwa niaba ya Waheshimiwa Wajumbe Wawakilishi wote kukupongeza na kukushukuru kwa uzalendo wako katika kusimamia masuala ya haki yanayohusu Zanzibar.

Ninaamini chini ya uongozi wako Mhe. Mwenyekiti, chombo hiki kama kilivyofanya huko nyuma maamuzi mazito yaliyotufikisha Zanzibar tulipofika, ninaamini katika hili pia utatuongoza kusimamia maslahi ya Zanzibar na watu wake. Mhe. Mwenyekiti, pokea pongezi za dhati. Ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilipokuwa ninachangia niliomba kupewa ufafanuzi juu ya kifungu nambari 220506, na Mhe. Waziri alipokuja hapa alijaribu kutoa maelekezo na maelezo kwamba pamoja na ongezeko hili lakini ilikuwa kuna jengo jipya ambalo wamehamia kutoka eneo moja kwenda eneo jengine.

Lakini kinachonishtusha Mhe. Mwenyekiti, nimefanya utafiti wa ghafla moja nimegundua kwamba mwaka 2010/2011 taasisi hii ilipatiwa fedha shilingi milioni moja na laki moja, ukurasa wa 44.

Lakini mwaka 2011/2012 ikatiliwa shilingi milioni nne laki moja na kumi na sita, ni asilimia 300 ya mwaka uliopita. Lakini na mwaka huu unaofuata mbele vile vile shilingi milioni kumi na mbili, ni asilimia mia tatu tena.

Sasa nilikuwa naomba maelekezo zaidi katika suala hili. Jee huu uhamiaji ulikuwa katika miaka yote mitatu au kwa mwaka mmoja tu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, naomba Wajumbe waelewe kwamba siku hizi tunakwenda na utaratibu wa wakati. Idara nyingi au Wizara nyingi zinawakodi wasafishaji hawa kwa mkataba.

Sasa mkataba tunamkodisha kwa mwezi mmoja unafika shilingi milioni moja. Sasa hili milioni kumi na mbili kwa mwezi, zinaweza zikawa hata kidogo. Lakini hizi ndizo fedha ambazo tumepewa na Wizara ya Fedha.

Lakini kwa utaratibu wa sasa hivi ninafikiri hapa Afisi ya Baraza la Wawakilishi ukichukua kwa mkataba inaweza ikawa hata shilingi milioni tano kwa mwezi. Sasa kwa mwaka itakuwa milioni sitini.

Sasa naomba Mhe. Mjumbe ajue hivyo kwamba utaratibu huo ni wa kuwakodi hawa wasafishaji siku hizi. Kwa hivyo hiki ni kiwango kidogo Mhe. Mwenyekiti, lakini kutokana na hali hiyo ya keki ambayo tunagaiwa ndio hali ilivyo kwamba ni kidogo. Kama ingekuwa Mhe. Mjumbe ana uwezo ningelimuomba mimi akanipa milioni ishirini hapa.

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee baada ya ufafanuzi huo.

Kifungu 0601 Idara ya Utumishi na Uendeshaji Sh. 566, 653,000/=
Kifungu 07

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi niseme nimefurahi sana na majibu, sana Mhe. Waziri na ni mfano mmoja mzuri sana kujibu masuali kama haya, lakini ninataka kutoa tahadhari kwa Mawaziri wote.

Kilichojitokeza Mhe. Waziri musiridhike na kauli za watendaji wenu. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa leo kidogo nimetahadharika lakini ningekufumulia mabomu hapa hapa kwa sababu wamecheza mchezo mchafu.

Mtu ana miaka 100 anajua neno la *declare*, hebu tujiulize ana miaka 100 atajuaje ku-declare. Hilo moja ninataka nikwambie.

Lakini ninamjua mtu ambaye aliyesimamia kwenye wizara yako amefanya mchezo ule mchafu. Mhe. Mwenyekiti, munatupa pesa za utafiti UNDP ninawashukuru sana, hatufanyi jambo la kuripuka tu, tunafanya jambo kwa utafiti tosha. Kauli ya mwisho iliyokubalika ataitwa mtu kutia thamani wa serikali ili hiyo tathmini ionekane nani *value* yake kubwa na nani yake ni ndogo awe kum-*feed* mwenzake. Watu wameondoka pale lakini vile vile barua hazikufika, ndio kwa sababu ule mchezo mchafu umeshaanza kutendwa sasa zile barua zinazohusika hazikufika, sasa ndio maana wakaona kwa makusudi wamefanya *delay* ile.

Naomba sana Mawaziri musikubali kupewa taarifa hivi hivi, jamani mutuogope sisi tunakwenda nyayo hadi nyayo tunafanya utafiti wa uhakika. Kwa hayo machache Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mhe. Waziri amekubali ku-*with draw* ule mchezo urejeshwe upya basi naomba Mhe. Mwenyekiti, hoja siizuii tuendelee. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Kuna kitu unataka ueleze Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mhe. Mshimba lakini naomba nimuelezee tu kitu kimoja, kwamba mtu wa miaka 100 hajui ku-*declare* inaweza ikawa ni kweli. Lakini ile si kazi yake ni kazi ya wale watendaji pale, anaweza akenda kipofu pale akishakusema kwamba mimi ninataka kufanya hiki na hiki, basi yule mtendaji hiki atajua anachokitaka ni kuandika *statement of declaration.*

Kwa hivyo si lazima yeye ajue lakini wale wataalamu wanajua hiki anachokisema kiandikwe hivyo. Lakini mawazo yake ninayakubali tutafuatilia vizuri. Ninakushukuru.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu nilizungumzia suala la nyumba ya Wakfu ya Bi. Sharifa Suleiman Masoud. Ninashukuru Mhe. Waziri kanipa majibu ya fasaha ya kutosha, jambo ambalo itabidi tumuone Waziri wa Mawasiliano. Kwa hivyo yeye nilitaka kumshukuru tu kwa sababu silo hasa ninalotaka kuligusia.

Ninataka kuligusia hapa Mhe. Mwenyekiti, linahusu hoja ya Kamati. Ninadhani kama Mjumbe wa kamati nina haki ya kulisimamia. Katika hotuba yetu ya Kamati ya Katiba, Utawala Bora tukitoa maoni katika wizara hii kuhusiana na Wakfu na Amali ya Amana, tulitaka maelezo kuhusu nyumba 20 ambazo zilikuwa katika nyumba mpya za maendeleo, na wanufaika wake walikuwa hawajajitokeza hizi nyumba zikachukuliwa na kurejeshwa majenzi.

Sasa siku ya bajeti Mhe. Mwenyekiti, ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati hili suala liliibuka na akatupa maelezo. Lakini nimelazimika kusimamia tena Mhe. Mwenyekiti, ndio maana katika kamati yetu tukaliibua tena, kwa sababu hoja ya Mhe. Waziri wakati ule kwa hoja ya Wizara ya Ardhi lilikuwa limemalizika kwamba litarejeshwa katika usimamizi wa Kamisheni ya Wakfu.

Lakini kuna nukta aliizungumza Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwamba kwa sababu nyumba za Wakfu ni tofauti na nyumba za serikali, kwa hivyo hata upangaji wa kodi.

Nilikuwa naomba nipatiwe ufafanuzi Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri anayehusika na Wakfu kwamba kwanza anithibitishie kuna maelewano ya kukabidhiwa hizi nyumba. Sasa kama nilivyosema Mhe. Mwenyekiti, sisi ni wachungaji hata kama mjumbe wa Kamati ya Katiba nitakwenda kuulizwa kesho kama sikusimamia haki hii. Sasa anithibitishie kwamba jee hizi zinarejeshwa kweli katika wizara yake.

Lakini pili zikirejeshwa, jee Kamisheni ya Wakfu inalo jukumu sasa la ku-*review* kama palikuwa pashafanyika mikataba ya kodi zilizopangwa ili ziwanufaishe Wakfu tofauti na zile kodi zilizopangwa na serikali. Nilikuwa naomba maelezo hayo kutoka kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli naomba radhi sikuweza kulizungumza hilo kutokana na muda. Lakini ni kweli kuna nyumba 20 na hizi hazikuwa 20 tu, zilikuwa nyumba kiasi 70 hivi.

Lakini zile nyengine zote tumerejeshewa na tumeshazishughulikia kwa mujibu wa utaratibu wa mirathi unavyosema. Sasa bahati mbaya hizi 20 ndizo zilizokuwa hazijapatikana, na hazijapatikana kwa sababu wale wenyewe hasa warathi au wanaotakiwa kuwa na zile nyumba walikuwa hawajapatikana.

Tumejaribu kuita kwenye matangazo na nini, bado hawajafika. Kwa bahati Wizara ya Ardhi zile nyumba wakazigawia wapangaji wengine kwa mujibu wa utaratibu wao wa kupangisha.

Tulichosema sisi ni kwamba zile nyumba hata kama zimekodishwa kwa watu wengine lakini bado ni za Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. Kutokana na hilo, kwa hivyo bado tuna wajibu sisi kuzitetea zile nyumba ili hata kama wale wenyewe hawajapatikana kwa mujibu wa utaratibu wa mirathi, ni kwamba zile fedha ambazo tutazipata, tutazipata *Baitil-maal* baada ya kukamilisha utaratibu wote ambao unahusika.

Hilo tumelifanya na kulifuatilia, mimi binafsi nilikutana na Waziri wa Ardhi tukazungumza na yeye akakubali akasema tumuandikie barua na nambari za zile nyumba, nikafanya hivyo na yeye ameshaipokea.

Lakini sasa kuna utaratibu mwengine wa wale kwa sababu zile nyumba zote zimeshakodishwa, mule muna binadamu, muna wananchi wetu, muna Mzanzibari, hatuwezi moja kwa moja tu tukamwambia toka hii nyumba ni ya Wakfu, itakuwa sivyo.

Tunafanya utaratibu mzuri ili yule aliyemo kama ataendelea kubakia akodi, lakini sasa kodi ije Wakfu na Mali ya Amana. Kama alivyosema kwamba kweli kodi zetu sisi kidogo zipo tofauti na kodi ya Wizara ya Ardhi na hilo lote wanajua na tutawaelezea.

Kwa hivyo ninamuhakikishia kwamba kodi za Wakfu na Mali ya Amana zitakuwa ni tofauti na kodi za Wizara ya Ardhi, lakini lazima tufanye utaratibu ili wale wanaokaa katika zile nyumba wao ni binadamu, na tuweze kuwaeleza vizuri na tukubaliane vizuri. Hilo ndilo tunalichukua hivi sasa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru na nimesema mara nyingi kwamba utaratibu wa Baraza letu hivi sasa unabadilika, kwa hivyo ninataka kuchukua dhima kwa niaba ya kamati yetu na ninaamini katika hili Mwenyekiti wangu wa kamati ananiridhia kwamba tutalisimamia hili kuona utekekezaji wa suala hili tunalifikisha hadi mwisho, ili baadae tuje tutoe ripoti katika kamati yetu au katika Baraza lako kwamba kweli tumesimamia haki za watu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee ahsante sana.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ninakushukuru Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia kuhusu Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, nilitaka kuhusu uwekaji wa *data base*. Ninashukuru Mhe. Waziri amenijibu.

Lakini sehemu ya pili ya suala hili sikulisikia kwa sababu nilitaja wasi wasi na masikitiko yaliopo, kwamba baadhi ya nyumba ambazo nyumba hizi nyingi ni kongwe zinafikia wakati kuvunjwa na kupewa baadhi ya

wafanyabiashara. Sasa nilikuwa nauliza tu wale wafanyabiashara wanaopewa kuzivunja na kujenga nyumba nyengine, wanapewa kwa kuuziwa au wanaendeleza ule uwakfu wake wa ile nyumba.

Kwa sababu wengine wanasema kwamba unaondoshwa hasa ule wakfu, basi ninataka kujua hiyo taswira iliyojitokeza kwamba baadhi ya nyumba zinazovunjwa na kupewa wafanyabiashara, zinakuwa ule wakfu wake unaondoka. Jee hilo suala hilo linajulikana na ni kweli.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria za kidini ambazo ninaamini Mhe. Rashid ni muelewa mzuri ni kwamba ule wakfu haufi, hata kama kuna nyumba iliyovunjika basi ile ardhi itakuwa bado ni sehemu ya wakfu.
Mfano mzuri ambao yeye ataufahamu nikimpa ni sehemu ya eneo liliopo katika Msikiti wa Al-halil. Sehemu ile yote mpaka juu Kilimani kule, lile ni eneo la wakfu. Kuna watu wamejenga lakini baada ya kujenga sisi Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana tumewaita wale, tumekubaliana ama kwa kununua ardhi ile ambayo itakuwa kwa utaratibu maalum uliowekwa fedha zile zitakwenda katika Wakfu, au ile nyumba itakuwa ni sehemu ya Wakfu kwa makubaliano maalum.

Kwa hivyo bado fedha au mapato ya maeneo bado Kamisheni yetu ya Mali ya Amana inaendelea kuchukua.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ninamshukuru Mhe. Waziri na tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 0701	Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Unguja	Sh. 364,135,000
Kifungu 0702	Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Pemba	Sh. 95,865,000
Kifungu 0801	Ofisi ya Msajili wa Haki Miliki Unguja	Sh. 120,000,000
Kifungu 0901	Ofisi ya Mrajis Vizazi na Vifo Unguja	

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia niliuliza kuhusu utaratibu wa vyeti vya kuzaliwa kwa wazee. Mhe. Waziri alijibu utaratibu wa vyeti vya kuzaliwa jinsi wanavyojitayarisha upatikanaji

wake. Lakini sasa kuna hawa wazee wetu kama tulivyozungumza kwenye ofisi ya vitambulisho, kuna wazee waliokuwa na umri wa zaidi ya miaka 60 na 70, na yeye alisema kwamba wanaweka vikwazo kwa watu hao ili kuwatambua wageni wanaoingia, ili wasije wakapewa watu vyeti wakajakuwa marais wa Zanzibar na wakati sio Wazanzibari, ni vizuri sana.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atufafanulie kwa hawa wazee ambao wana uhakika na wanajulikana fika, kwa sababu hawa tunawakosesha haki zao nyingi na halafu urasimu huu wa vyeti na bei zake sasa hivi mzee hawezi kuvipata, kwa sababu hayo malipo ya hivyo vyeti ni makubwa. Sasa atuwekee utaratibu mzuri ili wazee wetu wasitaabike wakakosa haki zao, wana haki nyingi wanazozikosa.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atuwekee utaratibu mzuri, ili wazee wetu waliokuwa na uhakika, atuwekee ule utaratibu tu kwamba je, tufuate utaratibu gani ambao kuwa watajulikana kuwa hawa ni wenyeji ili wasipate tabu ya kupata hivi vyeti, kwa hao wazee waliokuwa wameshafikia umri wa miaka 60, 70, 80 na kuendelea. Kwa sababu huko nyuma wazee wetu walikuwa hawana umuhimu wa vyeti, walikuwa hawajui hasa umuhimu wa vyeti. Lakini sasa hivi umekuja umuhimu wa vyeti, kama huna cheti basi hupati haki zako.

Kwa mfano Mhe. Mwenyekiti, kama huna cheti hupati kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, kama huna kitambulisho cha Mzanzibari basi huendi mahakamani kumchukulia dhamana mwanao kama amefungwa, hupati pesa benki, hupati kupiga kura na mambo mengine yote ambayo yako ulimwenguni, hupati kazi. Sasa je, ni utaratibu gani ambao ametuandalia ili wazee wetu wasitaabike.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri nilieleza utaratibu, na utaratibu huu ni kwa vijana, wazee na kwa kila mtu kwamba ikiwa hukuwa na cheti tokea mwanzo, ukitaka kupata cheti cha kuzaliwa ni lazima ujaze fomu ya maombi. Nilichosema ni kwamba ule utaratibu uliokuwepo zamani, kulikuwa kuna maswali mengi tu, yale tumejaribu kuyapunguza. Lakini bado tuna wajibu wa kuhakikisha kwamba huyu mtu ni mzaliwa wa Zanzibar, hata kama ni mzee wa miaka 60, 70 au 80 anaweza akawa sio mzaliwa wa Zanzibar au sio Mzanzibari ni lazima tujuwe.

Kwa hivyo, ninachopenda kusema ni kwamba kwa wazee kama wale kwanza tumewawekea unafuu. Kwa mfano, Pemba hawaji huku kama ilivyokuwa zamani kwa ajili ya maombi, mambo yote yanamalizika huko huko. Pili yale maswali yote yanajibiwa na wafanyakazi wetu, yaani yeye anaulizwa wanajibu, lakini mwisho kuna maswali mengine ukimaliza hapo ni lazima

uende mahakamani ukale kiapo, hayo ni mambo ya urahisi ambayo tumeyafanya. Kwa hivyo, mtu akifanya hivyo, na kwa sababu zile shughuli zote zinafanywa na maafisa wetu, mimi naamini ule utaratibu wa zamani wa usumbufu utakuwa haupo na ndivyo tulivyofanya kuwasaidia hawa wazee. Kwa hivyo, nawaomba wazee wafuate utaratibu huu, maafisa wetu watakuwepo pale, watawauliza maswali pale wajibu, halafu kila kitu kitafanywa na maafisa wetu badala ya wao, wao wataambiwa tu ni lini waende wakachukuwe vyeti vyao.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, hilo jibu analojibu Mhe. Waziri ni zuri sana na ni utaratibu mzuri sana, lakini kuhusu haya malipo ya hiki cheti ni kiasi gani cha malipo, kwa sababu mtu alikuwa mpaka anakipata cheti ni zaidi ya shilingi 30,000 na ni udhia kubwa sana. Sasa na huu utaratibu wa malipo utakuwaje?

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, *late registration* ni kama unapewa faini maana yake cheti cha kawaida ni shilingi 3,500, lakini *late registration* ni shilingi 32,000. Naamini na najua kwamba wazee na watu wetu wengi hawawezi ada hiyo. Lakini hizi ni pesa ambazo zimo katika mchango wa serikali. Hapa mmeshapitisha kwamba mimi natakiwa nipeleke fedha hizi serikalini, na kama sikuzipeleka nitakuja kuulizwa. Suala hili tuliliona na tulilizungumza katika ule utaratibu wetu wa kupeleka ripoti zetu katika kila miezi mitatu, bango kitita maarufu.

Mhe. Mwenyekiti, tulilizungumza suala hili na Mhe. Rais, na Mhe. Rais akaliona hilo na akasema kwamba ili tuweze kulitafakari na kulifikiria basi tuandike waraka wa namna gani tunafikiria, na namna gani tunapunguza na namna gani tukipunguza kutoka 32,000 kwenda, tuseme tu kwa mfano 20,000, ni fedha ngapi zile ambazo serikali itakosa. Kwa hivyo, hilo ndio ambalo tunalifanya hivi sasa ili tulipeleke serikalini, na serikali ikiamua basi wazee hawa au faini hii itapungua kwa kiwango hicho ambacho serikali itakubaliana na hoja yetu au waraka wetu ambao tutaupeleka serikalini.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli majibu yake Mhe. Waziri ni mazuri sana, lakini kwa sababu hawa watu wanakosa haki zao, hivyo namuomba Mhe. Waziri kuwahimiza watendaji wake, huo waraka unaotakiwa kuandikwa basi uandikwe ili hizi haki za watu zipatikane. Jamani sisi kama tunavyozungumza kila upande, na kama viongozi tutakwenda kuulizwa jamani, tutakwenda kuulizwa kuwa tulikuwa tukiwaongoza vipi kwenye ulimwengu watu. Kwa hivyo, kila haki ya mtu basi tufanyeni ili yule mwenye haki apate haki yake jamani. Tuendelee Mhe. Mwenyekiti,

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa nitumie fursa hii sasa niulize lile swali langu ambalo Mhe. Waziri alinijibu kwamba shughuli zile zilizokuwa katika Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali zimehamishiwa katika Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo, hasa katika suala la usafiri.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili nililichangia katika bajeti yangu, lakini nilikuwa nikidhania kuwa limebakia katika Ofisi ile ya Mrajis Mkuu Pemba. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyomwambia Mhe. Waziri kwamba nikiangalia bajeti ya Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo Pemba, nataka nikiri hii kidogo ina uwiano na ile ya Unguja. Lakini tatizo langu nnalosema, wale watu waliokuwa wakifanya shughuli zile za kukusanya takwimu na kupeleka mahitaji ya zile fomu na vitu vyengine walitulalamikia sana kamati kwamba wana tatizo la usafiri na Mhe. Waziri anajua hivyo, tuliwahi kumuambia katika kamati yetu.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili linalohusu usajili wa vizazi na vifo, ndoa na talaka, kwa sababu kule kuna utaratibu huu. Sasa nimeangalia katika bajeti ya Ofisi ya Msajili wa Haki Miliki ambayo sasa ndio inaanzishwa upya Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Makao Makuu hata wao usafiri wenyewe waliowekewa ni ununuzi wa Honda, Vespa na Ciao, kuna milioni 11,500,000. Lakini fungu hilo hilo ukitizama Pemba hakuna kitu kama hicho na walikuwa wakiomba angalau wapatiwe usafiri kama huo wa vespa au wa Honda wa kuwawezesha kuingia katika maeneo ya ndani ya Pemba kutokana na Giografia yake, kuweza kupeleka zile huduma na pia kukusanya zile takwimu. Kwa hivyo, nilikuwa namuomba Mhe. Waziri anisaidie kwamba je, angalau wanafikiri hawa, maana yake katika vifungu ndio halimo, lakini angalau wanafikiria labda katika fungu ambalo liko Makao Makuu ya wizara, kuwafikiria na kuwasaidia chochote hawa, angalau wapate usafiri ili hii dhiki ambayo wanakumbana nayo Pemba iweze kuondoka Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, tumewafikiria, kwa sababu ukitizama kifungu 220401 na 220402 hizi ni gharama za *petrol* na *diesel*. Sasa gharama za *petrol* na *diesel* ni kwamba tumefikiria kuwa kutakuwa na kitu chochote cha usafiri ama cha *diesel* au cha *petrol* na tumetia humu kidogo. Mhe. Mwenyekiti, zaidi ni kwamba wizara yetu Pemba nafikiri yeye ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria, na anajua jinsi tunavyofanya kazi kwa pamoja. Pale ambapo hapana usafiri basi wizara yetu tunajitahidi kuazimana gari na kufanyia shughuli hizi. Kwa hivyo hata hiki kifungu kitatoa mafuta ili kusaidia hiyo gari ambayo tutaazima kwa shughuli hizo.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana naye kwamba ni lazima baadae tujiandae kutafuta usafiri wa kudumu katika Ofisi hii ya Mrajis wa Vizazi na Vifo, nashukuru.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo ya Mhe. Waziri, naamini kwanza tumekifikisha kilio chao katika ofisi hii, na naamini kwamba kwa ahadi yake kwamba atalizingatia kweli wakati atakapokaa na watendaji katika wizara. Kwa hivyo, nimuombe kwamba sio bajeti hii tunaipitisha, zaidi itategemea huruma zake na za watendaji wakuu katika makao makuu ya wizara katika bajeti zao. Lakini angalau katika bajeti ya mwakani basi aone haja ya kuwafikiria hawa kuwa na vipando vyao ili kuwasaidia kuweza kufanya kazi hii ngumu ambayo wanaifanya kama wanavyofanya wenzao waliokuwepo hapa Unguja. Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee, ahsante sana.

Kifungu 0902 Ofisi ya Mrajis Vizazi na Vifo Pemba Sh. 74,138,000
Jumla ya Fungu Sh. **2,394,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na kamati ya matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 46 – TUME YA KUREKEBISHA SHERIA

Kifungu 0201

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru wakati nilipokuwa nikichangia kuhusu Tume ya kurekebisha sheria, nilitoa rai moja na sio kwa sababu ya utashi tu, lakini kutokana na ukweli ulivyo kwamba wananchi wengi hatufahamu sheria. Kuna baadhi ya migogoro inayojitokeza na matatizo inawezekana ni ya kiuendeshaji au inawezekana ni kutokana na upungufu katika sheria.

Kwa hivyo, nilisema kwamba je, kuna uwezekano wa Tume hii, Mhe. Waziri alijibu sana, pamoja na maelezo yaliyokuwa ndani ya kitabu, lakini alipita kule kule kwamba wanakwenda mawizarani na kuwaeleza watu wa mawizarani. Lakini bado wadau mbali mbali hawajatajwa. Nilisema sekta binafsi, wadau wananchi wenyewe. Kwa mfano migogoro ya ardhi.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri anieleze kwamba je, rai hii au uwezekano huu haupo. Kwa sababu sheria nyingi zinawezekana kwamba zimepitwa na wakati, lakini kwa maofisini tu hawajui kwa sababu hata wanasheria wenyewe wengine majaji wanasema sheria nyingi hazitumiki zinabaki ndani ya vitabu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri anipe maelezo

kidogo kwamba je, hii tume ya kurekebisha sheria imezuia kukutana na wananchi na wadau au uwezekano huo upo, ili baadhi ya mapungufu yanayojitokeza, iwe pengine yanaweza kuwa yanatokana na mapungufu ya kisheria, namuomba Mhe. Waziri anipe maelezo ya ziada.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa natoa maelezo yangu nilisema kwamba hatuwezi kusema kwamba ni sheria ngapi mbazo sio nzuri hivi sasa. Nilisema hivyo kwa sababu tumepeleka barua mawizarani, bado hawajatujibu, lakini tunazo sheria 20 ambazo zinahitaji marekebisho.

Mhe. Mwenyekiti, lakini katika kutekeleza majukumu hayo tume inashirikiana na wadau na hata katika kitabu changu hiki, tumesema katika kitabu chetu tunashirikiana na wadau mbali mbali, inategemea ile sheria yenyewe inahusu masuala gani. Kama ni sheria ya kilimo bila shaka watu wa kilimo, wakulima wenyewe na watu kama hao ni lazima watakuwemo. Ndio maana utaona kwamba kuna fungu huku la hiyo kufanya elimu au kukaa pamoja na wadau hao kutizama au kujadili sheria yenyewe. Kwa hivyo, hiyo Mhe. Mwenyekiti, ipo katika hotuba yetu na katika maelezo yetu.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, kama tume iko huru kukutana na wadau na upo utaratibu huo, basi nakubaliana na maelezo yake, tuendelee.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia kwenye kifungu hiki cha tume ya kurekebisha sheria, nilionesha wasi wasi wangu kwamba sheria zetu ziliopo zinajengea wigo *executive* na hatimaye inatuelekeza, ikiwa zitatuelekeza katika *Monarch*. Nilitoa mfano kwamba hivi sasa kufanya *presidential impeachment* ni shida, kwa sababu yeye Rais ndiye anayechagua Mkuu wa Majeshi, Mkuu wa Polisi, Mkuu wa Usalama wa Taifa. Sasa Mhe. Waziri katika hili, yeye na tume wanalionaje hili. Kwa sababu tunazungumzia utawala bora na demokrasia. Je, sheria zetu kwa hili hazihitaji marekebisho, ili kuona kwamba hatuendi kwenye *Monarch* na Rais anaweza kufanya mashaka.

Mhe. Mwenyekiti, Rais wetu tunampenda lakini ili kuelekea kwahala kuzuri zaidi. Je, huoni kama kuna haja ya Rais baada ya kuwateua hawa hii tume yetu ikafanya mabadiliko ya sheria wakathibitishwa na vyombo kama hili Baraza letu la Wawakilishi. Hilo moja.

Pili, Mhe. Mwenyekiti, wakati nilikuwa nachangia hapa katika kifungu hiki, vile vile nilionesha wasi wasi wangu kwamba Rais anaingilia mihimili mingine, yaani sheria zetu zinamfanya Rais aingilie mihimili mingine. Kwa

mfano yeye anakuwa na nguvu ya kumchagua Jaji Mkuu wa nchi. Je, haoni kwamba hivi sasa imeshafika wakati kwa sheria zetu hizi kutoa nafasi kwa huu muhimili wa mahakama ukatayarishiwa mazingira, yaani sheria zetu zikatayarisha mazingira ya kuona kwamba huu muhimili wa mahakama unachagua Jaji Mkuu, badala ya kuwa *appointed* na Rais.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, mimi sioni kama kuna tatizo, kwa sababu sheria sio wizara yangu inayotunga ni wananchi kwa kupitia Baraza la Wawakilishi. Sasa kama wananchi watasema sheria hii tuseme kwa mfano Jaji Mkuu ateuliwe na Rais lakini aje athibitishwe hapa Wawakilishi wakishapitisha sheria hiyo ndio itakuwa sheria. Sasa hilo ni jukumu la wadau, wale wadau wote wanaohusika ni lazima wakae, wakubaliane na watoe maoni yao kuhusu sheria yoyote ile. Kwa hivyo, kwetu sisi yakishatoka yale maoni na mapendekezo, sisi ndio tunawajibika au wajibu wetu sisi ni kuiandika sheria ile, kuipitisha katika vyombo vinavyohusika na baadae kuja kwenye Baraza la Wawakilishi ili kujadiliwa na kupita. Sasa Wawakilishi wakipitisha ndio sheria. Sheria ni chochote ambacho kitapitishwa na Wawakilishi na kutiwa saini na Rais. Kwa hivyo, yote aliyoyasema na kama wao ndio wanavyotaka, na kama watazungumza na wadau wakakubaliana hivyo, ikaja Baraza la Wawakilishi baada ya kupita katika vikao vinavyohusika tukakubali, basi na mimi nakubali.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri asinizonge katika hili, kwa sababu *system* ya nchi yetu ime-*centralize* ikiwa ni pamoja na hiyo *proposal* za miswada. Sasa anatuambia sisi kwamba twende kwa wananchi au wadau. Ni serikali Mhe. Mwenyekiti, ambayo inayokwenda kwa wadau na sio sisi Wawakilishi. Sisi Wawakilishi kazi yetu baada ya hiyo miswada kuletwa hapa ni kuipitisha. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri atuambie je, serikali ina *system* gani katika kuwashirikisha wananchi katika hili. Sio kwamba atusukumizie sisi kazi twende kwa wananchi wawe-*centralize* hii.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, akisoma katika hotuba yangu kwenye ukurasa wa 26. Tulisema kwamba baadhi ya mambo tunayofanya ni kufanya utafiti kwa lengo la kugundua utafiti kwenye sheria mbali mbali. Baada ya kufanya utafiti huo, tukishafanya na kugundua kasoro zile, kinachofuatia ni kwamba utafiti ule sasa wanapelekewa wadau, wadau wao wanasema kwamba kwa mujibu wa haya mapendekezo yenu serikali ndio inayofanya, kwa sababu utafiti unafanywa na tume ya kurekebisha sheria, lakini wakishafanya ni lazima yende kwa wadau, wadau ndio wanasema kwamba mapendekezo yenu hayo hatuyataki au tunataka yawe hivi na hivi, wao wanachukua, wanarekebisha na halafu yanapita katika utaratibu unaokubalika, mwisho ndio yanakuja katika Baraza la Wawakilishi.

Kwa hivyo, Baraza la Wawakilishi na wao wakifika hapa, wanao uwezo katika kamati na katika Baraza zima kusema kifungu hiki kibadilishwe au kifungu hiki kirekebishwe, ili Jaji Mkuu kwa mfano ateuliwe na Rais, lakini baadae athibishwe hapa. Huo ndio utaratibu ambao unafanyika, sasa mimi sifikirii kama namfanyia hadaa kama watu wa Ole, hapana. Huo ndio utaratibu ambao upo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki niwe mgumu katika hili na kwa sababu lisilo budi hutendwa, basi wacha tuendelee.

Kifungu 0201	Utawala Bora	Sh. 271,000,000
	Jumla ya Fungu	Sh. **271,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na kamati ya matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 14 – MAHAKAMA KUU ZANZIBAR

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia katika Idara hii ya Mahakama Kuu ya Zanzibar, nilimtaka Mhe. Waziri anifanyie uchambuzi juu ya ufunguaji wa kesi za Mahakama Kuu ya Kadhi, au Mahakama za Kadhi. Kuna kesi karibu 970 zimefunguliwa katika mahakama mbali mbali, na zipo ambazo zimetolewa uamuzi. Sasa wakati alipokuwa akinijibu Mhe. Waziri, alishindwa kunitolea ufafanuzi juu ya jambo hilo. Kwa hivyo, nataka anipe ufafanuzi. Je, hizi kesi zenyewe ni za aina gani na gani na ni katika wilaya gani, na zipi zimehukumiwa na zimehukumiwa katika hukumu gani.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nilizungumzia juu ya kesi zilizopo katika Mahakama ya Kadhi ya Makunduchi, ambapo humu kwenye kitabu chake alichotuwasilishia kinasema kwamba kesi zilizofunguliwa ni 20, lakini zilizotolewa maamuzi hakuna. Lakini wakati alipokuwa akinijibu, alisema katika Mahakama ya Makunduchi kesi zilizofunguliwa ni 19 na zimetolewa uamuzi zote. Sasa sijui maelezo yapi ambayo yako sawa, ni haya yaliyokuwepo kwenye kitabu au haya ambayo ametueleza wakati akifanya ufafanuzi. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Labda Mhe. Waziri aje asaidie tu, lakini hii ni majengo, tunatengeneza mahakama. Saidia Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kama ulivyosema. Lakini katika kitabu nilielezea utaratibu wote wa kesi ambazo zipo na

zimetolewa maamuzi. Zile zinajumuisha mahakama zote za Unguja na Pemba. Kwa hivyo, anasema tumletee list ya kesi zile zote, kwa leo Unguja na Pemba hiyo itakuwa ni ngumu. Lakini zile ndio kesi ambazo zimetolewa uamuzi na nyengine hazijatolewa uamuzi.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala la kesi ya Makunduchi, ile tulisema Mahakama ya Kadhi wa Wilaya ya Makunduchi, walisema kwamba kuna kesi 20. Mimi nikasema kwamba sio kesi 20. Kesi ambazo hazijatolewa uamuzi na sababu gani pia walikuwa wakitaka. Mimi nikasema kesi zilizoko Makunduchi katika Mahakama ya Kadhi ni kesi 19 zinazohusiana na talaka na ndoa. Kesi hizi zote zimeshatolewa uamuzi sio 20 ni 19, ambazo hizi zote zimeshatolewa maamuzi.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri Mhe. Waziri ametusaidia tuendelee.

FUNGU 14 – MAHAKAMA KUU ZANZIBAR

Kifungu 0201	Utawala Unguja	Sh. 600,000,000
	Jumla ya Fungu	Sh. **600,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na kamati ya matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 15 – OFISI YA MWANASHERIA MKUU ZANZIBAR

Kifungu 0201	Utawala Unguja	Sh. 1,800,000,000
	Jumla ya Fungu	Sh. **1,800,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na kamati ya matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 35 – OFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

Kifungu 0201	Utawala Unguja	Sh. 250,000,000
	Jumla ya Fungu	Sh. **250,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na kamati ya matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 36 – WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

Kifungu 0401

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri atakumbuka katika mchango wangu nilihoji suala ambalo linahusika na *vote* 740000 marekebisho ya msingi, ingawa sikuvitaja kwa nambari lakini niligusia tu. Kifungu kidogo cha 740010, Biashara na kuimarisha Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali *Best.*

Mhe. Mwenyekiti, nilihoji kwamba ukiangalia ripoti ya bajeti ya mwaka jana, mchango wa washirika wa maendeleo, kilichoweza kuingia kilikuwa ni asilimia 5. Nikasema kwenye kamati tulihoji hili, na ni haki ya wajumbe wengine waliokuwa si wajumbe wa kamati ya katiba na sheria kujua nikawaelewesha kwamba maelezo tuliyopewa ni kwamba kuumeni ukishavuka upande wa pili wa bahari huko, walifanya hujuma ambazo zilipelekea kukosekana kwa fedha zile. Kwa sababu wafadhili walisema kwamba fedha hizi zipo mwaka wa fedha haujesha ombeni, upande wa pili kwa sababu ndio unaoratibu, wakakwamisha hatukuzipata.

Sasa nauliza hili Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri anisaidie kwamba wa mradi wa *Best* kimsingi ni mradi ambao unafadhiliwa na washirika wa maendeleo, na serikali zetu huwa zinatoa ile *talk amount* ili kuonesha *commitment* yetu. Sasa kwa mwaka huu wa fedha Mhe. Mwenyekiti, unaona hapa kwamba mradi huu una milioni 100 ambazo ni *government contribution*. Kwenye *foreign* hakuna kitu, jumla ni hiyo milioni 100. Sasa nataka kumuuliza Mhe. Waziri, ndio tufunge mikono kwamba ndugu zetu wa damu wamefanikiwa kutufungia kabisa kwamba hatupati chochote kwa mwaka huu wa fedha. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, sivyo anavyosema Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Kwa kweli mradi wa *BEST* huu ulikuwepo mwaka jana, lakini utaratibu wa mradi huu Wizara ya Katiba na Sheria au wizara nyengine yoyote ile ni kama kwamba wao hawahusiki sana, isipokuwa wanaohusika ni Wizara ya Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Sasa Wizara ya Fedha wanazungumza na wenzao. Huku katika *Donor Community* na Benki ya *ADB* nafikiri ndio inayohusika.

Kwa hivyo, kilichotokea Mhe. Mwenyekiti ni kwamba Wizara ya Fedha wakati wa mwisho mwisho ndio ikatuambia hazikupatikana, kwa sababu sisi tunachukua fedha hizi kutoka Wizara ya Fedha na wao ndio wametuambia kwamba hazikupatikana.

Kwa maana hiyo, kama hazikupatikana sababu zaidi watazijua wao kuliko wizara nyengine yoyote. Lakini ule mradi wa *BEST* haukutolewa fedha. Kwa kuwa shughuli hii lazima tuifanye na tumeshaji-*commit* huku nyuma na ndio maana sisi tukaiomba serikali, ili itoe fedha za serikali.

Sasa kama fedha zile zitapatikana katika kipindi hichi basi hiyo itakuwa katika shughuli nyengine, lakini sisi tutaendelea na mradi huu kwa kutumia fedha zetu za ndani.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, mimi nakumbuka kabisa na nafikiri na Wajumbe wenzangu wa Kamati watakumbuka, kwamba suala hili nililihoji mimi katika Kamati na ni watendaji wa Mhe. Waziri waliotupa maelezo hayo, kwamba mradi huu kimsingi unafadhiliwa kwa ajili ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, ni kweli Wizara ya Fedha wanaratibu, lakini wao wanapata lile fungu kutokana na fungu la jumla la Jamhuri ya Muungano.

Vile vile walituambia kwamba zilikwama kupatikana kwa sababu hiyo niliyoeleza, kwamba tulikuwa tumechelewa, lakini wakaambiwa wakati mwaka wa fedha haujesha basi zipo zilizobakia mnaweza kuziomba, lakini ziombwe na yule mwenye kushikilia fungu ambaye ni Jamhuri ya Muungano, lakini wao wakaambiwa hamuwezi kuziomba tena ndio zikakosekana.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani hakuna haja ya kubishana kwa sababu ni suala ambalo kimsingi haliongezei chochote kama kauli ya Mhe. Waziri, kwamba hii *zero zero* haina maana hakuna mchango wa washirika wa maendeleo, lakini mchango huu unashikiliwa na Wizara ya Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, basi naridhika na kama nilivyosema ni Mjumbe wa kamati nitapata nafasi ya kufualitia huku.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru naomba tuendelee. Ahsante.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia nilieleza kuhusu tatizo la Jumuia ya Uamsho, Mhe. Waziri alisema kwamba amewapa onyo, lakini bado wanaendelea bila ya kibali. Je, hatua gani inayofuata? *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, majibu yalitoka kuhusiana na hili na hapa tuko kwenye bajeti ya maendeleo, nafikiri itoshe na maelezo yaliyotoka. Tuendelee.

Kifungu 0401 – Idara ya Mipango Sera na Utafiti Sh. 3,887,200,000/=
Jumla ya Fungu Sh. **3,887,200,000/=**

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matuumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 46 TUME YA KUREKEBISHA SHERIA

Kifungu 0201	–	Utawala Bora	Sh. 145,000,000/=
		Jumla ya Fungu	Sh. **145,000,000/=**

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matuumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya Wizara yangu bila ya mabadiliko. Sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako liyakubali makadirio hayo. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na makadirio ya Wizara hii ya Katiba na Sheria wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni sana kwa kazi nzuri na mashirikiano makubwa, hatimae tukamudu kupitisha kasma zote. Kwa kweli Waheshimiwa Wajumbe, naona furaha zimezidi kwa kumpitishia Mhe. Waziri kasma zake zote. *(Kicheko/Makofi)*

Baada ya shughuli hiyo nzuri na Waheshimiwa Wajumbe, mlifanya shughuli nyengine hapa ambayo nayo imezaa matunda mazuri sana. Tuliwachangia vijana wetu wa umri wa miaka 20 ambao walikwenda kwenye Mashindano ya Mpira wa Miguu nchini Burundi. Kazi nzuri mliyoifanya kuwachangia vijana hawa, imezaa matunda kwa vijana hawa kuingia kwenye nusu fainali kwa kuwafunga vijana wenzao huko Burundi goli 1 kwa sifuri. *(Makofi)*

Kwa hivyo, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Wajumbe kwa michango yenu, kumbe michango ya Baraza hili huwa inazaa matunda mazuri sana. Hivyo, tuendelee kuwaunga mkono vijana wetu, ili wawe wanashinda katika michezo mbali mbali pale maombi yanapoletwa katika Baraza letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hayo sasa naakhirisha kikao hichi hadi kesho tarehe 18/07/2012 saa 3:00 za asubuhi.

Saa 2:45 usiku Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 18/07/2012 saa 3:00 za asubuhi)